

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Tano – Tarehe 3 Novemba, 2008**

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 54

**Kuratibu Wataalam wa Kitanzania**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu inatumia fedha nyingi katika kuwasomesha wataalamu wa Sekta mbalimbali na kwa kuwa baada ya kufanya kazi kwa miaka michache wataalamu hao huamua kutafuta kazi nchi za nje hasa Botswana, Swaziland na hata Afrika Kusini bila kufidia Serikali kitu chochote.

- (a) Je, ni kwa nini Serikali haianzishi utaratibu wa kuratibu wataalamu hao?
- (b) Je, ni hasara gani Serikali yetu inapata kutokana na uhamiaji huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeliona tatizo hilo na imechukua hatua zifuatazo zenye lengo la kuhakikisha kwamba unakuwepo utaratibu endelevu wa kuratibu wataalamu hao ili waweze kukidhi matarajio ya Serikali. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha mchakato wa maandalizi ya Sera ya Menejimenti ya Uhamaji wa nguvukazi (*Labour Migration Management Policy*) itakayotoa mwongozo wa jumla

kuhusu masuala ya utumiaji wa wataalamu wa Kitanzania waishio na kufanya kazi nje ya nchi yaani (*diaspora*), na kuandaa mazingira yatakayoruhusu Watanzania hawa kuwekeza hapa nchini. Sera hii vilevile, itaweka mfumo mzuri wa Watanzania waishio na kufanya kazi nje na kusafirisha fedha zao kuja hapa nchini (*remittance transfer*) kwa ajili ya kuiendeleza nchi pamoja na kupata ushauri wa kitaalamu (*consultancy*) kutoka kwao pale Serikali itakapohitaji.

(ii) Kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kuanzisha kitengo cha *Cross Border Placement* chenye lengo la kuratibu utoaji huduma za ajira za wataalamu wazalendo ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na:-

Kuandaa mikakati ya kuwavutia Watanzania walio nje ya nchi kurudi nchini kuchukua kazi zinazohitaji ujuzi wa kipekee.

Kuweka utaratibu wa kuratibu wa kudhibiti ajira ya Wataalam Wazalendo nje ya nchi kwa lengo la kuinua pato la Taifa. Hili ni pamoja na kuweka utaratibu wa mawasiliano kati ya Serikali yetu na nchi nyingine Watanzania wapo ikiwa ni pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za wataalamu wazalendo walioko nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, hasara ambayo Serikali yetu inapata kutokana na uhamiaji huo kwa kutokuwa na utaratibu wa kiratibu wataalamu hao ni kama ifuatavyo:-

- Kukosa pato la Taifa.
- Nguvukazi ya Taifa yenye uwezo na ujuzi kuondokana na kusababisha utaalamu ambao ungetolewa na wazalendo kutolewa na wageni tena kwa gharama kubwa.
- Baadhi ya wazalendo kuondoka nchini kunyemelea kwenda nchi za nje na mara nyingine kuleta matatizo ambayo yanaaibisha taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba mikakati ya Serikali ilioanzishwa kuratibu uhamiaji huu itakuwa ni suluhu endelevu ya kuondokana na matatizo hayo na kuhakikisha kwamba wataalamu wazalendo wanaokwenda kufanya kazi nje wanajenyea uwezo Taifa.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa dhamira ya Serikali inayoonyeshwa wazi kwamba ina mpango wa kuanzisha namna ya kuweza kuweka *record* ya hawa watumishi wa Serikali ya Tanzania wanaofanya kazi nchi za nje, lakini suala hili limekwenda muda mrefu tunaseme tutatengeneza mpango na bado hatujafikia mahali hapo.

Je, si vizuri Serikali ikapitisha mpango na ika tekeleza jambo hilo mara moja kwa sababu bado tunapoteza fedha nyingi na raslimali yetu kwa nchi nyingine ambazo hazikuwahudumia hawa watu?

Pili, Nchi kama Pakistan inapata pesa zake nyingi kutokana na wataalamu hata wa *Nuclear Science* wanaopelekwa nchi nyingine kwenda kufanya kazi za kitaalamu katika nchi mbalimbali na Korea nayo pia inasafirisha wataalamu kwenda nchi mbalimbali hata Air Hostess sasa wanakodishwa kutoka nchi ya Korea kwa sababu ni nchi ambayo imejiandaa kusambaza watalamu sehemu mbalimbali.

Je, Tanzania tunashindwa nini ili na sisi tuwe na Benki ya Wataalamu ambao sisi wakienda nje tunafanya mkataba nao ili Serikali wanayokwenda kuifanyia kazi iwe inalipa fedha katika Serikali yetu na sisi tuweze kupata fedha kutokana na gharama tulizoingia kwa hawa Watanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, kama ifuatavyo.

Kwanza, kuhusu suala kwamba kwa nini hili suala limechukua muda mrefu napenda nimhakikishie kwamba mchakato wa kuanzisha sera uko mbioni na punde hiyo sera italetwa katika Bunge lako Tukufu na hivyo utekelezaji uanze kwa haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala kwamba kwa nini tunashindwa kuwa na utaratibu ambao nchi nyingine inazifanya ni kuwa kuwa tulikuwa hatuna Sera, Sheria ya kufanya hivyo na mara Sera na Sheria tutakapokuwa tumezikamilisha kama ambavyo nimemhakikishia kwamba mchakato huu tunaufanya kwa haraka sana ili kuhakikisha kwamba wataalamu wetu wanaokwenda nje.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wetu watakuwa wanaleta fedha zao kiurahisi basi suala hilo litawezekana na ninapenda nimhakikishie kwamba mchakato huu tutaupeleka kwa ari na kasi na nguvu mpya ili utekelezaji wake uwe ni wa haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kazi kwa maeleo ya nyongeza tafadhali!

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongeza kidogo juu ya jibu zuri alilolitoa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi.

Ni kwamba Korea na Pakistan zimefikia hapo alipokuwa akisema Mheshimiwa Mbunge kwa sababu wameshafikia ile *critical mass* ya wataalamu kwa hiyo wanaozalisha ni *surplus*, sisi hapa bado tuna matatizo ya kufikia *critical mass* ya wataalam hata hawa wachache waliopo ndiyo maana tunanyang'anyang'ana na ndiyo maana utakuta bado Waziri wa Kazi analazimika kutoa vibali vingi kwa sababu ya kupata

wataalamu kutoka nchi za nje. Kwa hiyo, hao wachache wanao – *footer through* ndiyo wanaomuunga mkono Mheshimiwa Waziri pale kwamba upo mpango maalum ku – *make sure* kwamba inatakiwa *taken care*, wanaangalia ipasavyo na kuona kwamba nchi inafaidika.

Lakini kwamba huingia katika mikataba kuweza kusafirisha wataalamu bado hatujafikia *critical mass* hiyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi. Kwa swali linalofuata kwa Ofisi hiyohiyo ya Mheshimiwa Rais mambo ya Utumishi nimearifiwa kwamba litaulizwa na Mheshimiwa Mbaruku Mwandoro, kwa niaba ya Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo.

Na. 55

**Mabadiliko ya Wizara Yanayoathiri Mwelekeo wa  
Fedha, Malengo na Watumishi**

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO (K.n.y. MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Katiba ya nchi yetu inampa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuunda au kubadili Wizara mbalimbali.

(a)Je, matumizi na usimamizi wa fedha ambazo Wizara zake zinaunganishwa na unakuwaje?

(b)Je, yale malengo yaliyopangwa awali yanatekelezwa mara baada ya Wizara kuungana na muundo kubadilika?

(c)Je, mgawanyo wa Watumishi kitija unakuwaje mara baada ya mabadiliko ya Muundo wa Wizara.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha za kuendesha shughuli za Serikali hugawanywa kwa kuzingatia majukumu na muundo wa Wizara husika. Iwapo mabadiliko ya muundo yanaunganisha Wizara mbili kuwa moja, fungu la fedha (*Vote*) la Wizara iliyovunjwa huwa halitumiki na badala yake kubakizwa katika kumbukumbu za Serikali kwa ajili ya rejea mbalimbali za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, inapotokea sehemu ya majukumu ya Wizara moja kuhamishiwa katika Wizara nyingine fedha za jukumu hilo (*sub vote*) pamoja na zile za mishahara ya watumishi wanaotekeleza jukumu hilo kuhamishiwa katika Wizara ambapo majukumu hayo yamehamishiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati wa muda wa kati na Bajeti, Wizara ambayo majukumu na Muundo wake umebadilika baada ya kuunganishwa na Wizara nyingine inatakiwa kuhuisha Mpango Mkakati wake ili kuendana na mabadiliko ya majukumu yanayotokanana kuunganishwa huko. Kwa mantiki hii, malengo yaliyopangwa awali yatatekelezwa kwa kuzingatia uhuishwaji huu ambao unazingatia majukumu yaliyoongezwa, kupunguzwa na au kufutwa.

(c) Mheshimiwa Spika, majukumu na muundo wa Wizara yanapobadilika kutokana na kuunganishwa kwa Wizara, Watumishi wanaohusikana mabadiliko haya hupangiwa kazi kwa kuzingatia yalikohamishwa katika Mpango Mkakati wa Wizara mpya. Katika hatua hii, Wizara husika hutakiwa kuhuisha mahitaji yake ya Watumishi (Ikama) kwa kuzingatia majukumu mapya yaliyoongezwa, kuhamishwa au kufutwa.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Wakati wa kikao kilichopita cha Bunge Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na baadhi ya Wabunge walishauri Serikali kuangalia upya uwezekano kuwa na Waziri wa Nchi anayeshughulika na mipango mara baada ya Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha kuunganishwa lakini Tume ya Mipango ikawa chini ya Ofisi ya Rais.

Je, ushauri huo mpaka sasa umefanyiwa kazi kiasi gani?

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kama ifuatavyo:-

Kuhusu ushauri ambao ultolewa tumeupeleka kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu ndiye aliyepewa Mamlaka kikatiba ya kuweza kuunda Wizara kwa mujibu ambavyo anaona inafaa kwa mujibu wa majukumu ambayo yapo kuendana na Serikali ya awamu yake.

Kwa hiyo, bado Mheshimiwa Rais anafanya kazi na pale ambapo ataona inafaa atafanya lakini akina haifai basi tutaendelea kutokuwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulikia Mipango.

### **Tatizo la Maadili Nchini**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. MHE. STANLEY YONO KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tatizo la UKIMWI na RUSHWA hapa nchini ni suala la kimaadili zaidi:-

- (a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kutatua tatizo la maadili nchini?
- (b) Katika juhudhi za kutatua tatizo hilo, kwa nini Serikali isitoe ruzuku kwa Makanisa na Misikiti ili taasisi hizo zishiriki kikamilifu kupunguza tatizo hilo?

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Stanley Yono Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa ufanuzi kuhusu dhana hii inayoitwa maadili. Maadili ni taratibu na kanuni zilizokubalika katika jamii kuwa kama mwongozo wa mahusiano katika jamii hiyo. Ni mahusiano kati ya makundi ya watu na namna wavyoendesha maisha yao. Kwa hiyo kila kundi katika jamii lina maadili yake; kuna maadili yanayowahusu watumishi wa umma, viongozi wa asasi za dini, wanamichezo, viongozi wa umma, wataalamu wa fani mbalimbali na kadhalika.

Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, tatizo la rushwa ni ukiukwaji mkubwa wa misingi ya maadili na uadilifu katika jamii.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kujenga maadili katika jamii ni la jamii nzima na kwa hiyo kwa hapa kwetu Tanzania jukumu la kuifanya jamii iwe na maadili mema ni la wananchi wote; kuanzia katika ngazi ya familia, ukoo, jumuiya hadi ngazi ya Taifa. Maadili mema huanza kujengwa kuanzia hatua ya utotonii kwa binadamu na kuendelea kulelewa na wazazi, shulenii hadi kufikia utu uzima na hatimaye kuanza kujitegemea.

Hata hivyo, Serikali kwa kupitia vyombo vyake mbalimbali imekuwa ikiendesha mafunzo, semina kongamano pamoja na vipindi vya redio na televisheni kwa lengo la kuelimisha wananchi kuhusu maadili mema. Kazi hii ni ya kudumu na itaendelea kufanya. Aidha, katika kuhakikisha kwamba suala la maadili na uadilifu linahimizwa kuanzia hatua ya awali, Serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii pamoja na vyombo vingine vinavyohusika na masuala ya elimu inafanya utaratibu wakuangalia uwezekano wa kulijumuisha somo la maadili katika mitaala ya shule kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu kwa lengo la kuwapa vijana ufahamu wa kuwa raia wema.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la maadili na kujenga uadilifu kwa wananchi wa dini mbalimbali limekuwa ni sehemu kubwa ya mafundisho ya dini zetu zote. Dini zote zinasisitiza kuhusu usafi wa tabia na mienendo ya waumini wao, ukweli uaminifu, kujiheshimu na kupendana. Na kwa hakika kazi hiyo imeendelea kufanywa vizuri na dini zote pasipo kuhitaji ruzuku kutoka Serikalini.

Kwa hiyo, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua mchango mkubwa utolewao na taasisi za dini katika kujenga maadili mema kwa waumini wao na kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa viongozi wa dini na wananchi kwa ujumla tuendelee kushirikiana katika kutekeleza jukumu hilo.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna usemi kuwa katika uongozi wa Umma usafi wa tabia, vitendo na kauli ni nguvu katika uongozi kwa hiyo kichafu hakiwezi kusafisha uchafu.

Je, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Waziri kwamba malezi ambayo yanaanzia kwa wazazi ni muhimu jambo ambalo nakubaliana nalo. Je, si vizuri vilevile hata kwa sisi watu wazima licha ya watoto kuangalia kwamba mienendo yetu vilevile haiathiri lengo hilo kwa sababu kuna wakati katika nchi hii vazi la Hayati Mwalimu Nyerere lilikuwa linajulikana sana na lilipendwa na Watanzania, vazi hilo liliitwa ‘Kaunda’. Kuna wakati Marehemu Oscar Kambona alikuwa anachana nywele kinamna Watanzania vilevile waliiga wakaita *Kambona style*. Kwa hiyo, kiongozi akionyesha aina fulani ya tabia watoto wataiga.

Je, haoni umuhimu wa kujiепusha na vitendo vibaya ambavyo vinasababisha watoto wetu kuiga ?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson M. Makwetta kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana naye kwamba ni vizuri tuwe na maadili mema. Sisi watu wazima ili visije vikaibiwa. Kwa hiyo, nakubaliana na usemi wake.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa tafsiri pana sana ya maadili ambayo amesema inaanzia utotonii.

Na kwa kuwa, muuliza swali na maadili aliyokusudia hapa kuna uhakika wa kwamba amehusisha maadili na rushwa hapa nchini, na kwa kuwa katika *form* za maadili wanazojaza viongozi bado zina matatizo makubwa. Kwa mfano, inaonekana *form* za

maadili tunazojaza viongozi nikiwemo mimi zinamtaka kiongozi kutaja mali alizonazo lakini haziainishi mali alizonazo au walizonazo watoto wake au wake zake au mke wake.

Na kwa kuwa, Serikali ndiyo mfano wa kuonyesha maadili mema. Je, Serikali sasa iko tayari kuzirekebisha *form* zetu za maadili zikaanza kutaja mali alizonazo Mheshimiwa mbunge au wanaohusika wote na kujaza *form* hizo pamoja na mali za watoto wake zinaainishwa katika *form* za maadili ili kulinganisha utendaji bora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimuhakikishie kwamba form za Maadili zinazungumzia pia kutamka mali walizokuwa nazo watoto wako amba wako chini ya umri wa miaka 18. Sidhani kama itakuwa vizuri watoto amba wameshapita umri watoto, *definition* ya watoto wetu katika Sheria mbalimbali ni chini ya miaka 18 kwa hiyo, sijui Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa anazungumzia watoto wa aina gani.

La pili, ninapenda kumfahamisha kwamba *form* hizi pia ziko katika kurekebishwa vipengele mbalimbali ambavyo vimeonekana havikidhi haja. (*Makofî*)

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID :** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kimsingi swal nililotaka kuuliza ndilo hili hili alilouliza Mheshimiwa Mnyaa lakini labda niongeze kidogo tu.

Kwenye hizi *form* za maadili zinavyoitwa pamoja na kwamba tafsiri ya Maadili ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa hapa na *form* zile zinaonekana zinagusa sehemu ndogo na zaidi sehemu ya mali ya mhusika.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hivi sasa pamoja na marekebisho ni pamoja na kurekebisha jina kwamba ziwe *form* za jambo lingine siyo Maadili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojieleza katika swali la msingi maadili ina tafsiri nyingi. Kwa hiyo, maadili kwa upande wa Viongozi tunazungumzia maadili ya jinsi walivyopata mali zao. Kwa hiyo, pale kinachotafutwa kujua ni kwamba hatumii nafasi yake kwa kujiletea utajiri kutumia ile nafasi ambayo wananchi wamemkabidhi. Kwa hiyo, maadili ya pale ni hayo na maadili ambayo tunazungumzia kwenye jamii ni mengine.

Nadhani kama tukiweka maadili ya kila kitu katika ile form nadhani itakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 57

### **Kuleta Madaktari wa India Nchini**

**MHE. PINDI HAZARA CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi sana nchini wanaenda kutibiwa nje ya nchi hususan India.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuingia mkataba na India ili kuleta madaktari (*Flying Doctors*) na vitendea kazi kutoka India?
- (b) Je, Serikali ina takwimu za wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi kwa gharama za Serikali?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakukaribisha hapa Bungeni. (*Makofi*)

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Mbunge wa Viti Maalam, lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuanza kwa kutoa ufanuzi wa dhana nzima ya *Flying Doctors*.

Mheshimiwa Spika, Kuna hospitali kadhaa hapa nchini ambazo hazifikiki kwa urahisi na hazina madaktari bingwa.

Serikali kwa kushirikiana na Shirika la AMREF ambalo Makao Makuu yake yapo Nairobi inao utaratibu wa kuwapeleka madaktari katika hospitali hizo kwa ndege, madaktari hao hukaa siku tatu hadi tano wakiwaona wagonjwa, kufundisha madaktari na wauguzi na watalaan wengine wa afya na kufanya upasuaji.

Huduma hii inaitwa *Flying Doctor Service*. Ikiwa swali la Mheshimiwa Mbunge lilikuwa linawalenga madaktari hawa, napenda kusema kwamba Serikali haina mpango wa kuwaleta madaktari hawa kutoka India, kwani madaktari wetu wanakidhi haja isipokuwa kinachohitajika ni kuboresha upatikanaji wa pesa zaidi

(a) Hata hivyo, Serikali ina mkataba na Hospitali za Apollo za India toka mwaka 1999, mkataba huu ndio unaoelekeza matibabu ya wagonjwa tunaowapeleka huko nchini India. Katika makubaliano mapya ya miaka mitatu, 2008 – 2011 Madaktari Bingwa kutoka India watakuwa wanakagua wagonjwa wanaotarajiwa kupelekwa India na kushauri tiba inayohitajika, kufundisha watalaan wetu na kuwaona wale waliowatibu ikiwa ni pamoja na wale waliowafanyia upasuaji nchini India. Zaidi ya hapo Hospitali za Apollo wanakamilisha makubaliano kati yao na shirika la Hifadhi ya Jamii NSSF ya kujenga Hospitali ya kisasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili likikamilika litapungua idadi ya wagonjwa wanaolazimika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu lakini vile vile watalaan wetu watapata fursa ya kupata mafunzo katika hospitali hiyo. Hospitali hiyo inategemewa kuwa na vifaa vya kisasa na watalaan wengi toka Hospitali hizo zilizoko India.

(b) Takwimu za wagonjwa waliopolekwa kutibiwa nje ya nchi kwa gharama ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2006/2007 jumla ya wagonjwa 241 walipelekwa kutibiwa nje ya nchi kwa gharama ya Tshs. 2,340,000,000. Mwaka wa fedha 2007/2008 wagonjwa 232 walipelekwa nje ya nchi kutibiwa kwa gharama ya Tshs. 2,321,404,094.20. Kuanzia mwaka 1998 hadi sasa Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii imepokea maombi ya rufaa

2,540 kati ya hao wagonjwa 1,579 tayari wametibiwa kwa gharama ya Tshs. 10,029,296,779.00.

**MHE. PINDI HAZARA CHANA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha.

Kwa kuwa amesema upo utaratibu wa kuanzisha hospitali hapahapa nchini ningependa kujuza zoezi hilo linatarajiwa kuanza lini na vilevile linatarajiwa kukamilika lini?

Kwa kuwa, hospitali hiyo itakuwepo hapa nchini na kama alivyosema Waziri zipo hospitali nyininge ambazi ziko mbali sana, Waziri atakubaliana nami kwamba mara zoezi hilo la hiyo hospitali inayojengwa itakapokamilika kuwa na mahusiano ya karibu sana na hospitali za wilayani ikiwa ni pamoja na hospitali ya Wilaya ya Ludewa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pindi Chana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba mchakato umefika mbali kwa maana tuko katika hatua ya kuwekea mikataba kati ya NSSF na hospitali za Appolo, tumeshatambua kiwanja karibu na chuo na siwezi kutaja ni tarehe gani lakini niseme huko tulikotoka ni mbali kuliko huko tunakokwenda. Nina imani kwamba katika miezi kadhaa tutaona majengo yanaanza kujengwa pale.

Swali la pili ilikuwa kuweka mauhusiano kati ya Hospitali ya Ludewa na hospitali hii tunayojenga. Mheshimiwa Spika, mimi ninadhami tungeiacha hii ifanye kazi za utaalamu kwa sababu tuna muundo mzuri wa rufaa kutoka hospitali zetu za Wilaya kwenye hospitali za Mikoa. Tumewahi kusema hapa kwamba nia ya Serikali sasa hivi ni *ku-up grade* hospitali za Mikoa ziwe hospitali za rufaa na kuanzia mwaka jana tumekuwa tukitenga fedha kuongeza miundombinu karibu shilingi milioni 600 kwa kila hospitali. Halafu vilevile tuko katika hatua nzuri tu ya kupata wataalamu wa kutosha.

Kwa hiyo, mategemeo yangu ni kwamba hospitali ya Ludewa ambayo na mimi naifahamu ni kuweka uhusiano mzuri kati ya hospitali hiyo na hospitali ya Iringa ambayo pia inakarabatiwa vizuri.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba zipo Huduma za Madaktari, (*Flying Doctors*), huduma za Madaktari wanaoruka kwa ndege hazikusambaa katika nchi nzima na zinakwenda katika hospitali chache nchini. Je, ni

kigezo gani kinachotumika cha kuteua hizo hospitali ambazo zinatembelewa na *Flying Doctors* na tufanye nini ili huduma hiyo iweze kufika Mpanda na Mkoa wa Rukwa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, utaratibu huo kama nilivyosema upo ingawa utekelezaji unaweza ukawa mgumu kutohana na matatizo ya hapa na pale hasa upatikanaji wa ndege. Tumekuwa tukitegemea ndege kutoka Shirika la AMREF ambao Makao Makuu yake yako Nairobi na Madaktari wanaoruka kwenda kwenye hizi hospitali wanatoka kwenye hospitali zetu za rufaa. Kwa hiyo tumegawa Tanzania katika zoni 4, kwa mfano Hospitali ya Bugando ndio imepewa jukumu la zoni hiyo ikiwemo ya Mpanda.

Sasa kama hawajafika Mpanda ni kitu ambacho tutakiangalia lakini vile vile inahitaji kuwepo na haja yaani Mpanda waoneshe kwamba wana wagonjwa ambao wanashindwa kuwapeleka katika Hospitali za Rufaa na kuomba hiyo huduma na hiyo huduma muombe katika hospitali ambayo inaangalia ukanda huo.

**SPIKA:** Naona tuendelee na swali linalofuata la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ingawa kabla sijamwita Mheshimiwa Mbunge wa kuuliza swali napenda kumshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwamba amejali kuona kwamba mimi sikuwepo Bungeni na kwa umri kama wangu kama Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii anakujali basi ni rehema. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 58

#### **Mabalozi Wanawake**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

- (a) Je, kuna Mabalozi wanawake wangapi wanaoiwakilisha nchi yetu katika Balozi za nchi za nje?
- (b) Je, ni Mabalozi wangapi wanawake wa nchi za nje wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI(K.n.y.  
WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Mabalozi wanawake wawili wanaoiwakilisha Tanzania huko nje ya nchi. Mabalozi hao ni:-

1. Mheshimiwa Balozi Mwanaidi Sinare Maajar (London, Uingereza).

2. Mheshimiwa Balozi Nyasugara P. Kadege (Nairobi, Kenya).

(b) Ni Jamhuri ya Ireland na Canada pekee ndizo zinazowakilishwa na Mabalozi Wanawake mionganoni mwa nchi zenyewe uwakilishi hapa nchini.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na kuishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia Mabalozi hao ingawa ni wawili wanawake na naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya 2005/2010 katika ukurasa wa 149 nanukuu ina kipengele cha wanawake inasema “(a) Kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010. Kama ilivyokwishaazimiwa na Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji huu wa ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005/2010 naomba kumwuliza Waziri ina mpango gani maalum wa kuongeza asilimia hiyo ambayo imeingizwa katika ilani yetu ya uchaguzi kwa kuteua Mabalozi wanawake sambamba na Mabalozi wanaume wawe sawa sawa. (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara ya Muungano na vile vile Zanzibar ni sehemu ya pili ya Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka pia wa kuteua Mabalozi kutoka Zanzibar kwa sababu sijawahi kusikia Mabalozi wanawake kutoka Zanzibar na wanawake wa Zanzibar na wao wana uwezo mkubwa na ni wasomi wazuri wa kila kitu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anijibu hilo swali? (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na dhamira njema ya Mheshimiwa Rais wetu ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na sote tumeona mifano yake hatua mbalimbali wanazochukua katika kuleta uwiano wa uongozi kati ya wanawake na wanaume na mifano katika Baraza lake la Mawaziri na teuzi nyingine mbalimbali. Naamini kutokana na dhamira hiyo hiyo Mheshimiwa Rais wetu ataendelea kuiona ngazi hii ya Mabalozi wanawake kutuwakilisha katika nchi za nje.

Aidha, nina hakika suala la Mabalozi wanawake kutoka Zanzibar ni ushauri mzuri. Mheshimiwa Rais ndiye mwenye mamlaka hayo ataangalia kwa kina maana kama nilivyosema na dhamira njema ya kuhakikisha kwamba uwiano huu unafikiwa kama ambavyo Ilani yetu imeonyesha. Ahsante sana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza suala dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa wanawake sasa uwezo huu wa utendaji wanao na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imesema kabisa ifikie asilimia 50 kwa 50. Je, Waziri sasa yuko tayari kwenda kutoa ushauri kwa Waziri wake wa Mambo ya Nje kufikisha ushauri kwa Rais ili na wanawake hao wapewe kuwa Mabalozi nchi za nje kuiwasilisha nchi yetu?

**SPIKA:** Nadhani wanawake wateuliwe kuwa Mabalozi, sio wanawake wapewe Mabalozi.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa ufanuzi mzuri. Kwa kuwa amenitaja niwe kiungo cha kuwasilisha ushauri wake kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje namhakikishia kufanya hivyo.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda mrefu nafasi za Mabalozi wanawake imekuwa aidha ni moja au ni mbili. Na kwa kuzingatia kwamba wanawake wengi hapa nchini ni wasomi wazuri na uzoefu wanao. Je, ni sababu ipi ya msingi au ni vigezo vipi vinavyotumika kuwateua hao Mabalozi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba mamlaka ya uteuzi wa Mabalozi iko chini ya Mheshimiwa Rais. Na kwa sababu leo akinamama wengi wamesikika wakilia kilio hicho nina hakika Mheshimiwa Rais amekisikia na naamini kama nilivyosema dhamira njema ipo kwa hiyo tumpe muda Mheshimiwa Rais kutekeleza wajibu huo.

**SPIKA:** Ahsante bado tuko Wizara hiyo hiyo swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga Mbunge wa Tabora Mjini. Naomba nikukaribishe Bungeni kwa sababu ulikuwa nje ya nchi kwa matibabu. Naona unaonekana kuwa umerudi na afya njema zaidi. Karibu sana.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunikaribisha Bungeni baada ya safari ya takriban miezi miwili huko India kwa ajili ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako ningependa vile vile kabla ya kuuliza swali niwafahamishe wapiga kura wangu wa Jimbo la Tabora Mjini kwamba nimerejea, Mwenyezi Mungu amenijalia niko katika afya nzuri na ninaanza kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ama baada ya kusema hivyo sasa nina heshima ya kuomba nipaye majibu ya swali Na. 59.

Na. 59

### **Sera ya Mambo ya Nje Kuhusu Diplomasia ya Uchumi**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sera ya Tanzania ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inasisitiza Diplomasia ya kiuchumi:-

- (a) Je, ni vigezo vipi vinavyoashiria kwamba utekelezaji wa sera hii unafanikiwa?
- (b) Je, ni wataalam wangapi katika fani za uchumi, biashara na masoko wamepelekwa kufanya kazi katika balozi zetu za nchi za nje hususan Uingereza, Marekani, Afrika ya Kusini na kwingineko ili kufanikisha utekelezaji wa Sera hii?

### **NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, vigezo vifuatavyo vinatumika kama viasharia kwamba utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje inayosisitiza Diplomasia ya Kiuchumi inatekelezwa:
  - (i) Kukua kwa vitega uchumi kutoka kwa wawekezaji wa nje (*Foreign Direct Investments (FDI's)*) ambapo imekuwa kwa asilimia 9.7 kati ya mwaka 2001 – 2007.
  - (ii) Kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaokuja nchini ambapo katika mwaka 2007 jumla ya watalii 719,031 walitembelea Tanzania.
  - (iii) Kupunguziwa kwa kiwango kikubwa cha deni letu la nje.
  - (iv) Kuwepo na hali ya usalama na amani ndani ya nchi yetu, nchi jirani za zile marafiki katika Jumuiya kama *AU, SADC, EAC, NAM* na nyinginezo kama mazingira mazuri ya kuendesha shughuli za kiuchumi na maendeleo.(v)Kukua kwa Biashara kati yetu na nchi washirika.

(vi) Kuongezeka kwa misaada ya kiufundi (*technical assistance*) kutoka kwa nchi wafadhili na zile rafiki.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kutekelezaji wa Sera Mpya ya Diplomasia ya Uchumi, Tanzania Wizara imeweka mikakati na imeshaanza kuitekeleza na kuhakikisha kuwa kila Ubalozi unaofunguliwa ikiwa na pamoja zilizopo zinakuwa na Maafisa wenye fani za uchumi, biashara na masoko ili kuweza kutekeleza vyema malengo yaliyopo kwenye Sera Mpya ya Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika Ubalozi wetu wa London, katika Kituo cha Biashara (*London Trade Centre*) kinasimamiwa na Mkurugenzi wa Kituo ambaye ana fani ya Biashara na Masoko. Aidha Ubalozi wetu wa New York na Pretoria Afrika ya Kusini tumepeleka wachumi ambao wataungana na Maafisa wengine wa Ubalozi. Hata hivyo jitihada zinafanywa kuhakikisha kuwa kila Ubalozi wetu unakuwa na wataalam wenye fani ya uchumi, biashara na masoko. Hivi karibuni wataalam 25 wa fani hizo watategemewa kupelekwa katika Ofisi zetu za Ubalozi katika nchi mbalimbali ulimwenguni.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa anayekaimu kwenye Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa majibu aliyyoatoa. Sasa ningependa kuuliza masuala mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza katika eneo ya viashiria, vinavyoashiria kwamba Diplomasia ya Kiuchumi inazaa matunda, mimi ningependa kuto Kubaliana na majibu haya kwa sababu kila kigezo alichokisema kina eneo maalum ambayo inashughulikia na sio Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Kwa mfano kukua kwa *Foreign Direct Investments Centre*, kukua kwa utalii ni eneo la Wizara ya Utalii, Maliasili pamoja na *Tanzania Tourist Board (TTB)* ili mradi kila eneo alilolisema ninaweza nikalizungumzia katika msingi hiyo. Nilichokitaka mimi ni kwa kiasi gani Balozi zetu zinahusika katika kuleta hali hii ya mabadiliko haya. Nitatoa mfano Ubalozi wa India upo.....

**SPIKA:** Tafadhali Mheshimiwa nenda kwenye swalii.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Swalii la msingi ni kwamba Balozi zetu hazina wataalam na haziendeshwi katika utaalam wa Diplomasia ya Kiuchumi. Sasa swalii ni kwamba ebu tuonyeshwe kwa kiasi gani Serikali iko *serious* kutekeleza sera hii ya Diplomasia ya Kiuchumi kwa kuziwekea Balozi zetu wataalam wa uhakika wa kufanya mambo hayo, mimi bado hapo sijapata jibu la uhakika?

Mheshimiwa Spika, La pili, ni kwamba katika kuliendeleza lile la kwanza tuiseme tu Balozi zetu tunawapeleka watu wa fani hizi na fani hizi. Yako maeneo muhimu ambayo kama vile .....

**SPIKA:** Mheshimiwa unaonekana una ushauri mzuri pengine ungeuweka kwa maandishi unaweza kuwa msaada mkubwa kwa Serikali. Lakini kwenye kipindi cha maswali ungekwenda moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Naomba kufahamu katika eneo la *World Bank* pamoja na *E.U.* Serikali inafanya nini kuhakikisha kwamba tuna uwakilishi wa kuweza kupambana na mambo mazito yaliyopo katika Balozi hizo mbili Washington na Brussels?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba Serikali yetu ni moja tunafanya kazi kwa pamoja Mabalozi wale wako pale kuwakilisha nchi yetu kwenye sekta mbalimbali. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ndiyo inaleta taratibu na kuunganisha. Kwa hiyo inapotokea viashiria vya namna hii vinavyoendeleza sekta mbalimbali maana yake ni kwamba Tanzania inapiga hatua na ile Diplomasia ya Kiuchumi inazidisha kuitangaza Tanzania na ndiyo maana zinasaidia hizo sekta nyingine kufanya kazi yake vizuri.

Hata hivyo nilimwambia katika jibu langu la msingi kwamba hivi sasa zinachukulia hatua za kupeleka wataalam wenye fani ya biashara, masoko na fani nyingine kwa nia njema kabisa ya kuongeza uwezo katika Balozi zetu ili isaidie hilo suala zima la Diplomasia ya Uchumi katika Balozi zetu na hatua hizo kama nilivyomweleza karibuni zimeanza kutekelezwa. Kwenye maeneo muhimu kama vile *World Bank* na EU ambapo uwakilishi wetu upo pale Ubalozi wetu upo makini katika kusimamia mambo haya na kama nilivyomwambia mwenye jibu la msingi kwamba wataalam wengine wanaongezwa katika kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa Kaboyonga uyaone maendeleo makubwa yanayofikiwa ya Tanzania kutokana na jitihada hizi za Diplomasia ya Uchumi.

Na. 60

**Serikali Kusaidia Nguvu za Wananchi Kujenga Shule**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Mkoa wa Singida wameitikia kwa nguvu mpango wa MMEM na MMES na kujenga majengo ya Shule za Sekondari za Kata, hosteli, nyumba za walimu na madarasa:-

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa fedha za bati na mbao ili kuunga mkono juhudhi hizo za wananchi katika kumalizia majengo ya hosteli kwenye sekondari hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kuwapongeza sana wananchi wote kwa jumla wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Singida kwa kujitolea kujenga majengo ya Shule za Msingi na Sekondari za Kata, Hosteli na Nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka Serikali inaunga mkono juhudhi za wananchi kwa kuchangia fedha za ujenzi wa majengo mbalimbali ya shule yakiwemo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Fedha hizo hutolewa kadri bajeti itavyoruhusu ili kusaidia kukamilisha ujenzi wa majengo hayo. Wizara yangu inawashirikisha viongozi wa Mikoa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wakati wa kugawa fedha za ujenzi wa majengo ya Shule za Sekondari kama vile fedha za madarasa, nyumba za walimu, hosteli, maabara. Viongozi wa Mikoa na Halmashauri ndio wanaoamua ni shule zipi zipate madarasa na zipi zipatiwe nyumba, na kadhalika.

Kwa hiyo ni imani yangu kuwa wakati viongozi hao wanagawa fedha za ujenzi, watatoa kipaumbele kwa shule zenyе majengo ambayo hayajakamilika yakiwemo majengo ya hosteli.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu yanayotia moyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunahimiza sana suala la Masomo ya Sayansi kwa vijana wetu hasa katika karne ya sasa. Katika maeneo mbalimbali tumekubaliana kwamba lazima kuwe na vishawishi vyta kuwafanya watoto wetu wasome masomo yasayansi. Na kwa kuwa maabara ni chombo muhimu au ni nyenzo muhimu ya kufundisha watoto wetu masomo ya sayansi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba katika sekondari hizi ambazo zinajengwa na wananchi basi Serikali ikasaidia kujenga maabara na kutoa vifaa vinavyostahili katika maabara zetu kuwawezesha watoto wetu kujifunza sayansi nadharia na kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa tumekubaliana kwamba katika kila Wilaya sasa tuangalie uwezekano wa kujenga *High Schools* katika kila Wilaya kwa maana kwa

mfano Singida tunajenga shule mbili katika jimbo langu na jimbo la mwenzangu Mheshimiwa Nyalandu. Je, Serikali itatusaidia vipi sisi wa Singida Kusini kwa maana ya Ikungi *High School* na kwa maana Ilongelo *High School* kuweza kukamilisha majengo yale ya *High School* ili watoto wengi sasa wanamaliza *Form IV* waweze kupata nafasi ya *Form V* na kuendelea?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumwarifu kwamba katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Wizara yangu imetenga maabara 10 kwa kila Mkoa. Hivyo ni jukumu la viongozi wa Mkoa Singida na mikoa inayohusika kuamua au kupendekeza ziende kwenye shule zipi kwa makubaliano yao wao wenyewe.

Kuhusu suala la pili utaratibu wa kujenga Shule za Kidato cha Tano na Sita Wizara Elimu na Mafunzo ya Ufundi imetengeneza mpango wa Elimu ya Sekondari awamu ya pili na kwamba itatekelezwa kwa kujenga shule mbili kwa kila Wilaya. Hivyo endapo mpango huo utakapoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 nashauri wenzetu wa Mkoa wa Singida na Wilaya husika waone misaada hiyo au fedha hizo zipelekwe kuimarisha kule ambako juhudzi za wananchi zimeanza.

Na. 61

#### **Mafunzo ya Ualimu Kwa Mwaka 2008**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitangaza nafasi za mafunzo ya ualimu kwa mwaka 2008 na wananchi wengi walituma maombi yao; na kwa kuwa, kuna upungufu mkubwa wa walimu nchini:-

- (a) Je, wanafunzi wangapi wamechaguliwa kuijunga na mafunzo hayo ya ualimu kwa mwaka 2008 na wanatoka Mikoa gani?
- (b) Je, kutoka Wilaya ya Liwale wamechaguliwa wangapi ikizingatiwa kuwa walimu wengi wakipangiwa huko hawaendi kuripoti?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya wanachuo 15,321 walichaguliwa kijiungu na Mafunzo ya Ualimu mwaka 2008/2009, kati yao wanachuo 6,171 wamejiungu na mafunzo ngazi ya cheti na 9,150 wamejiungu na mafunzo ngazi ya Stashahada.

(b) Kulingana na tangazo zaidi ya maombi 61,000 yalipokelewa na nafasi zilizokuwepo vyuoni ziliwa 15,321. Uchaguzi wa wanachuo wa kijiungu na Mafunzo ya Ualimu hauzingatii Mikoa au Wilaya wanazotoka waombaji.

Sifa zinazozingatiwa ni viwango vya ufaulu ambapo waombaji ngazi ya cheti walitakiwa wawe na ufaulu usiopungua divisheni IV alama 28 na waombaji wa Stashahada walitakiwa wawe na ufaulu usiopungua *Principal pass* moja na *Subsidiary* moja. (*Makofi*)

(c) Walimu 20 walilipwa jumla ya shilingi 4,311,000/= ikiwa ni malipo ya madeni yaliyohakikiwa mwezi Februari, 2007. Aidha, zoezi la kuhakiki madeni ya walimu wengine wa Liwale limekamilika. Madai yaliyowasilishwa ni ya walimu 131 yenye thamani ya shilingi 136,981,590/=.

Madai yaliyokubaliwa baada ya uhakiki ni ya walimu 96 yenye thamani ya shilingi 108,887,270/=. Madai haya yatalipwa mwezi Novemba, 2008.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza, nina maswali mawili.

La kwanza kwa nini Serikali haiwi wazi kuelezea jinsi gani *posting* za ualimu mwaka huu umekuwa. Kwa kuwa umeleta mkorogano mkubwa sana na mimi mwenyewe nilimkabidhi Naibu Waziri mhusika orodha ya vijana kutoka Liwale ambao wana sifa hizo zote na kwamba wachaguliwe hasa kwa kuzingatia kwamba maeneo ambayo elimu iko duni kama Liwale au Mikoa wa Lindi na kadhalika wapewe *priority*. Sasa hivi Serikali imelitupa, hilo la kwanza.

La pili, kuhakiki kwa madeni kulianza muda mrefu sana, lakini kila siku kukicha ni kuhakiki. Hawa wataanza kulipwa lini maana yake madeni haya yanayozungumziwa sasa hivi yanazidi ku-*pile up* tungeweza kupata taratibu ambazo *format* ya kulipwa madeni yale itakuwa lini vinginevyo ninawashukuru sana walimu wa Liwale kwa kutojiungu na mgomo vinginevyo matatizo ni makubwa hasa Wilaya zilizoko pembezoni.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali izingatie na naomba jibu sahihi kwa hayo?

**SPIKA:** Kwa faida ya wale ambao wamekuja tu humu Bungeni kushuhudia shughuli Wizara hii ina Manaibu Mawaziri wawili aliyejibu swali la Na. 60 ni Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na anayejibu sasa ni Mheshimiwa Gaudentia Kabaka.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA KABAKA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge alinikabidhi orodha ya majina ya wanafunzi ambao walitakiwa sio ku-postiwa lakini wapate kozi ya ualimu.

Lakini kama nilivyosema maombi tuliyokuwa tumepata ni 60,000 jumla kwa wanafunzi wa Stashahada na *Grade A*.

Nafasi zilizokuwepo ni 15,000 kwa *Grade A* peke yake kulikuwa na nafasi kama 4,000 au 5,000. Kwa hali hiyo waliokuwa wamebaki walikuwa zaidi ya wanafunzi 24,000 na wote hao walikuwa na sifa. Ilikuwa sio rahisi kwa kipindi kile Mheshimiwa alichonipa yale majina kuweza kuyapenyeza ili waweze kupata nafasi wakati tayari tulikuwa *bank* ya wanafunzi ambao walikuwa hawajapata nafasi.

Nashauri Waheshimiwa Wabunge muwaeleze wanafunzi wanaotaka ualimu walete maombi Wizarani kwa kuandika na kutumbukiza katika nafasi ambazo tumeweka maalum kwa ajili ya maombi haya badala ya kusubiri Waheshimiwa Wabunge wachukue orodha wailete Wizarani. Hii inatupa shida unakuta sisi tumeshapeleka wanafunzi vyuoni na nafasi zimeshajaa na tutaendelea kulaumiana, kwa hiyo naomba huu utaratibu ufuatwe.

La pili, kuhusiana na madeni ni kweli kabisa kwamba hamna mahali popote ambapo pesa italipwa kwa mdai bila ya kuhakiki kwamba kuna viambatisho muhimu vinavyohusiana na madai yake na vile viambatisho vimepitishwa na Mamlaka husika kabla hujalipa na ndiyo maana kwa Wilaya ya Liwale kati ya walimu 131 ni 96 tu ndio wanaostahili kulipwa, kama Wizara isingehakiki maana yake ingelipa madeni hewa.

Kwa hiyo, tunahakiki ili kuhakikisha kwamba kila anayelipwa analipwa fedha ambayo ni halali na si vinginevyo. Kwa hiyo naomba tukubaliane na uhakiki na kama nilivyosema mwezi Novemba walimu walibaki wa Liwale watalipwa.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii niongezee kidogo kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda kujibu hasa swali linalohusu, kuhakiki kwa madai ya Walimu.

Napenda nitumie nafasi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tuliunda *task forces* tano kwenda kwenye Kanda tano za Tanzania kuhakiki katika kila Wilaya. Kati ya Halmashauri zetu 133 mpaka Ijumaa Saa kumi walikuwa wamemaliza kazi katika Wilaya 126 zilikuwa zimebaki Wilaya saba.

Ninategemea kabisa kwamba mpaka mwisho wa kesho tutakuwa tumemaliza uhakiki wote wa Tanzania nzima. Kuanzia mwezi huu tutaanza sasa kulipa madai hayo na hatutakuwa na matatizo tena na haya madai ya Walimu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, natumaini Serikalini mnatengeneza utaratibu sasa wa kudumu ili lisiwe jambo la kujirudiarudia linaleta shida kidogo. Tunaenda kwenye swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa William Shellukindo wa Bumbuli.

Na. 62

### **Uharibifu wa Alama za Barabarani**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imejitahidi sana kufanya matengenezo muhimu mfano barabara Kuu ikiwa ni pamoja na kuweka alama za majina na vijiji kwa mfano barabara ya Morogoro hadi Dodoma.

(a)Je, Serikali imeona jinsi alama za majina ya vijiji zilivyochezewa hasa kutoka kijiji cha Dumila (Dumi) hadi Mtana (Mtanana)?

(b)Je, Serikali inatazamia kuchukua hatua gani kukomesha uharibifu huo wa alama za barabarani nchini kote?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekiah Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwishaliona tatizo la kufutwa kwa maandishi kwa baadhi ya alama barabarani na pia alama nyingine kung'olewa kabisa tatizo ambalo limejitokeza kwa nchi nzima. Alama hizi zimekuwa zikifutwa ama kung'olewa na baadhi ya wananchi wachache wasiokuwa waadirifu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo hili la uharibifu wa alama za barabarani, Wizara yangu kupitia Sheria mpya ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007

kifungu 31 (2) imeweka adhabu kali kuchukuliwa kwa yoyote atakayeharibu alama za barabarani ikiwa ni pamoja kulipa faini ya shilingi zisizopungua laki mbili au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Aidha Wizara yangu inaendelea na mpango wa kutoa elimu kwa njia ya redio na televisheni na kutembelea vijiji vilivyoko kando kando ya barabara zote nchini kwa lengo la kuwaelemisha wananchi juu ya umuhimu wa kutunza alama za barabarani. Katika kutekeleza mpango huu viongozi wa vijiji na wananchi wanapewa majukumu ya kuwa walinzi wa alama za barabarani.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote wasaidie kuwaelimisha wananchi kwenye maeneo yao muhimu wa alama za barabarani.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ninahisia sijui kama ataungana na hisia zangu kwamba kuna uwezekano wa uharibifu huu wa alama hizi katika barabara ya Morogoro Dodoma una malengo ya kijambazi ili wasafiri wa magari wanapopata shida wasiweze kuwasiliana na vyombo vya ulinzi na usalama, mathalani katika kijiji cha Maguha ile ‘ha’ imefutwa. Kwa hiyo, jina linasomeka Magu?

Swali la pili, kwa kuwa katika hisia zangu hizo zinaweza kuwa pengine ni njia mojawapo ya kuhalalisha masuala ya ujambazi. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya Wizara yake kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kulifanyia uchunguzi wa ndani tatizo hili katika barabara hii ambayo inapitwa na Waheshimiwa Viongozi wengi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliana naye kwamba hisia zake zinaweza kuwa sahihi kwa sababu hawa waharibifu wanaweza kuwa wanafanya uharibifu huo wakiwa na malengo mbalimbali likiwepo na hili moja ambalo ameliwekea hisia Mheshimiwa Mbunge. Lakini hisa zingine zinasema kwamba alama hizi za barabarani zinazong’olewa kutokana na biashara ya chuma chakavu, kwa hiyo hisia zinaweza zikawa nyingi. Kwa hiyo napenda nikubaliane naye kabisa kwamba Wizara yangu itashirikiana na Wizara nyingine zinazohusiana na suala zima la kuzuia uhalifu nchini lakini pamoja na suala zima la kuzuia hizi biashara za chuma chakavu na vyombo vingine vyote vinavyohusiana katika kutatua tatizo hili.

**MHE. MAGDALENA SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa alama hizi za barabarani zinasaidia sana kuongoza madereza; na kwa kuwa kwa baadhi ya maeneo mengine alama hizi zinapokuwa zimeondolewa Serikali inachukua muda mrefu sana kuzirudishia na maeneo mengine pia wajenzi wa barabara wanaweza matatu lakini hawaweki alama mwanzoni;

matokeo yake magari yanaparamia matuta bila kujua na hasa nyakati za usiku suala ambalo linasababisha ajali.

Serikali sasa inampango gani kuhakikisha kwamba kunakuwepo na ulinzi wa kutosha pale ambalo alama zinapotolewa barabarani ziweze kurudishiwa na maeneo ambayo barabara zinajengwa alama ziwepo ili kuashilia mbele kuna tuta au mapito mengine?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba alama hizi zinapoondolewa barabarani zinahatarisha maisha ya watumiaji barabara.

Sasa suala la kucheleta kurudishia alama hizi sisi tunalichukulia ni jambo la msingi sana na tutatoa maelekezo kwa vyombo vyetu vinavyohusika ili alama hizi ziweze kurudishiwa mara moja zinavyoondolewa. Lakini kama nilivyosema kikubwa hapa ni kuhakiki kwamba wote wanaohusika na maeneo yale alama hizi zinaporudishwa zisiondolewe tena.

Lakini kuhusu suala la matuta napenda nieleze tu kwamba suala la matuta kuwekwa barabara tulikuwa tumeshaelezwa kutoka kipindi kilichopita kwamba utaratibu wa kuweka matuta barabarani nataka uwe ni wa unifomu nchi nzima na tumeshatoa maelekezo sana hivi kwamba uwekaji wa matuta utakuwa unafanana nchi nzima na hiyo itakwenda sambamba na uwekaji wa alama kuonyesha kwamba hapa kuna tuta au hapa watu wanavuka. Kwa hiyo hilo tutaizingatia.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Serikali inajitahidi sana kufanya matengenezo kwa barabara zao kuu ambazo zinasaidia wananchi kuondokana na usumbufu wa uharibifu wa barabara hizo. Ninaomba Serikali wakati wa Bajeti ilikubaliana na sisi Mkoa wa Tabora kwamba itafanya matengenezo ya barabara kutoka Manyoni, Itigi Tabora. Kwa kuwa hivi sasa mvua zinatarajia kuanza Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kuondoa hisia kama zilizokuwa za Mkoa wa Morogoro kwa kutengeneza sehemu korofii ili magari yaweze kupita kwa wakati wote wa masika na kiangazi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Bajeti yetu ya miundombinu tuliahidi barabara hii ya Itigi Tabora itaanza kufanyiwa matengenezo. Niseme tu kwamba ahadi ile ilifuata mara moja baada ya hapo fedha zikatengwa na hivi sasa mchakato unaendelea kuhakikisha kwamba angalau utengenezaji huo uweze kuanza. Lakini kwa kuwa fedha zilikwishatengwa basi yale yote yanayozingatiwa katika ujenzi wa barabara yatatiliwa maanani.

## **Barabara ya Bagamoyo – Pangani – Tanga**

### **MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH aliuliza:-**

Kwa kuwa, barabara ya Bagamoyo – Pangani –Tanga ni barabara muhimu kwa kuunganisha nchi za Afrika Mashariki; na kwa kuwa hivi sasa barabara hiyo inafanyiwa upembuzi yakinifu ili kupata gharama halisi ya ujenzi:-

- (a)Je, barabara hiyo itajengwa ikiwa chini ya miradi ya Afrika Mashariki?
- (b) Je, usanifu wa barabara hiyo utahusishwa na daraja la mto Pangani?
- (c) Je, ni nani anagharamia usanifu huo na utakamilika lini?

### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swal la Mhesimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Barabara ya Bagamoyo Pangani hadi Tanga ni moja ya barabara zilizoainishwa chini ya mtandao wa barabara zinazokusudiwa kujengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani *ADB* kuititia miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kazi ya usanifu wa barabara hiyo unayojumuisha pamoja na daraja la Mto Pangani imekwishaanza kwa kugharamiwa na fedha za Tanzania. Kazi ya usanifu inafanyiwa na Kampuni ya Kihandisi ya *United Engineering and Technical Consultancy Ltd. (UNITECH)* ya *United Arab Emirates* ya Dubai kwa gharama ya shilingi milioni 663 na inatarajiwa kukamilika mwezi April 2009. Kazi hiyo ikishakamilika itakabidhiwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa hatua za ujenzi.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri niipongeze Serikali kwa hatua inazozichukua kuhusu barabara hiyo; na kwa kuwa barabara hii itakabidhiwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya utekelezaji. Je, Serikali itakubaliana na mimi sasa kuwashauri Afrika Mashariki kwamba kama ni Ujenzi wa barabara utagharamiwa na *ADB* likijumuishwa na daraja la Mto Pangani, anaweza kukubaliana na mimi kwamba sasa Daraja mkatafuta Wabia au watu wangine wakaijenga kwa utaratibu wa *Build Operate and Transfer (BOT)* ili tulipe road toll katika daraja hilo?

La pili, kwa kuwa kivuko cha Pangani ni sehemu ya barabara ya Tanga Pangani Bagamoyo na naishukuru Serikali kwa hatua ilizozichukua katika kukamilisha tatizo la kivuko cha Pangani Je, Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwamba kuna haja Mjumbe kutoka Kamati ya Miundombinu na mimi mwenyewe kwenda kujiridhisha na kazi inayoendelea huko Denmark ili tuweze kuhakikisha kwamba shughuli zinakwenda

vizuri. Mimi nipo tayari kujigharamia nusu ya usafiri huo kwenda huko?  
(*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la kwamba tushauri wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mtakapoanza kujenga barabara ujenzi wa daraja uchukue sura ya *BOT* naomba tuwe na subira muda utakapofika tutaendeleana kushauriana kwa sababu Mheshimiwa Mbunge bado tupo naye nadhani hatua hiyo ikifikiwa tutaendelea kushauriana na wenzetu tuone namna nzuri ya utekelezaji wa wazo hili ambalo mimi nauilunga mkono.

Hili la pili la kutaka kwenda kuangalia ujenzi wa zile parts za kuja kujenga kivuko cha Pangani kutuma Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu pamoja na Mbunge mwenyewe, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba maadam sasa hivi hatujapata mashaka ya kuonyesha kwamba kazi hii itakuwa na wasi wasi kwa sababu tulikubaliana kwamba atengeneze itakapofikia mwezi Mei 2009 kazi hii itakuwa imekamilika, mimi nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira sisi tunaendelea kufuutilia na tutaendelea kutoa taarifa hatua kwa hatua kabla hatujafikia uamuzi wa kupeleka Mjumbe mmoja pamoja na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ambaye yupo tayari kujigharamia nusu ya gharama; lakini tusubiri kwanza tuone kazi itakavyokuwa inakwenda.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kufuatana na barabara hii ya kutoka Bagamoyo Pangani hadi Tanga ambayo kwa kiasi kikubwa unapozungumzia Bagamoyo barabara hiyo inapita hasa kwenye Jimbo la Chalinze. Pamoja na upembuzi yakinifu unaofanywa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ifikapo Aprili 2009 itakuwa umekamilika na kwa kuwa wananchi wa Sadani eneo ambalo barabara hiyo itapita kuelekea Pangani wana wasiwasi jinsi gani barabara hiyo itakavyokuwa imepita kwenye maeneo yao. Je. Mheshimiwa Waziri anaweza kunifamisha na Bunge lako Tukufu upembuzi yakinifu huo wa kujenga hiyo barabara utapitia Sadani au nje ya Sadani.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi huo usanifu ndiyo unaendelea kwa hiyo ni mapema mno mimi sasa hivi kuanza kutoa matamko hapa kwamba itapita njia hii au ile. Mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tu kwamba muda tulionao mpaka 2009 Aprili si mrefu sana. Kwa hiyo, tutajua barabara hiyo inatapitia wapi lakini kwa sasa hivi nadhani sitakuwa tayari kueleza inapitia maeneo gani.

Na. 64

#### **Utoroshaji wa Nyara za Taifa**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 31 Januari 2008 niliuliza swali juu ya usafirishaji wa Nyara za Taifa zilizolewa *Ivory Room* kinyume na utaratibu na kisha kukamatwa Taiwan:-

- (a) Je, ni mitambo gani inayothibitisha sehemu meno ya ndovu yanapotoka?
- (b) Je, wako wapi na ni nani watu saba amba ni watuhumiwa wa kesi ya kuhujumu uchumi (*EC-2/2006*) ya tarehe 15/09/2006 iliyofunguliwa na Serikali katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Tanga?
- (c) Je, ni kwa nini Serikali ilifungua kesi kwa watu hao na wakati ilisema haina uthibitisho kuwa nyara hizo zilitoka Tanzania?

#### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII aliuliza:-**

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ujangili katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia, wanasyansi wamegundua matumizi ya chombo kinachoita *DNA Analyser* ambacho kinaweza kusoma *DNA* kutoka kwenye sampuli za meno ya ndovu. Pia picha za *DNA* hulinganishwa na picha za *DNA* zilizosomwa kutokana na Ndovu walio hai katika maeneo mbalimbali. Picha za *DNA* za meno ya Ndovu yaliyokamatwa zikifanana na za ndovu waliohai katika maeneo fulani huonesha uhusiano wa meno husika.
- (b) Na (c) Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge anavyotambua suala la meno ya Ndovu yaliyokamatwa nchini Taiwan bado liko Mahakamani likisubiri uamuvi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 64 (1) (c) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 inayosema: “*Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuvi wa Mahakama.*”

Hivyo namuomba Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi Mahakama itakapotoa uamuvi. Hata hivyo kwa kuwa kesi hii ni ya Jamhuri, Serikali inamuomba Mheshimiwa Mbunge kama ana taarifa za nyongeza zinazoweza kusaidia Jamhuri kufanikisha kesi hii asaidie ili kulinda rasilimali za nchi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza wakati huo nikikiarifu kitie chako masikitiko yangu kwa Wizara kwa kukiuka kifungu namba 46 cha Kanuni ukurasa wa 28.

Kesi hii ni ya mwaka 2006 na wakati nikiuliza Januari Wizara ilikubali kwamba haina uthibitisho wa maeneo haya. Sija uliza masuala ya Mahakama namwombwa

Mheshimiwa Waziri anijibu Watanzania saba sasa hivi wako wapi? Kwa sababu wakina Zombe wanaandikwa kwenye magazeti na wanajulikana wanakesi gani. Nilichouliza ni Watanzania hawa wako wapi.

Lakini la pili nilouliza Januari Serikali ilifunguaje kesi wakati haina uthibitisho? Haya ndiyo maswali nayaauliza, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri anijibu maswali yangu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivvyosema kwamba suala lipo Mahakamani kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekiri katika sehemu ya swali lake. Alitaka pia majina ndiyo maana tukasema kwamba katika kuzingatia na kuheshimu uhuru wa Mahakama na ku-*avoid* kutoku-*distort information* mbalimbali tukaona kwamba kwa sasa pengine si vizuri; kwa sababu unaweza kukiona kitu kidogo unaweza ukataja hapa Maiko wakati kule anayeshitakiwa kule ni Mikael na mtu akasema kabisa kwamba mtu akasema kabisa kwamba watu wanaoshitakiwa ni tofatu. Ndiyo maana nikasema pengine si vizuri sana kulizungumzia suala hilo hapa. Lakini kwa kifupi ni kwamba kesi hiyo ambayo ilifunguliwa mwaka 2006 ipo Mahakama ya Tanga na watuhumiwa saba wapo nje kwa dhamana.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa Tanzania ina shehena kubwa ya pembe za ndovu hivi sasa zilizohifadhiwa katika maghala ya idara ya Wanyamapor, Hifadhi ya Taifa na Ngorongoro kutokana na Tanzania kutokuruhusiwa pembe zake nchi za nje. Je Serikali inaweza kueleza ni lini kwa mara ya mwisho Tanzania iliuza pembe zake nchi za nje na nini hatma ya pembe zilizohifadhiwa zenyenye thamani ya mabilioni ya shilingi katika maghala hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna shehena kubwa ya pembe za ndovu iliyopo katika maghala ya Idara ya Wanyamapor hapa nchini. Shehena hizi za pembe za ndovu na nyara nyingine zinatawaliwa na mkataba wa kudhibiti biashara ya nyara na wanyama waliokuwa kwenye hatari ya kutoweka.

Kwa hiyo, uuzaji wake ulishazuiwa na mara nyingi unatawaliwa na vibali ambavyo vinatoka kwenye *Sites* sasa hivi shehena ni kubwa ipo na tumekuwa tukizungumza na hao wenzetu kuona ni lini tunaweza tukauza. Lakini pia hata kununua tu kwa kawaida biashara yenyewe imezuiwa na nchi nyingi za Afrika zina shehena kubwa.

Kwa hiyo, suala la shehena kuwepo ni kweli zipo lakini lini tutauza inategemea na makubaliano ambayo yanaweza yakafikiwa na majadiliano yanayoendelea.

Kuhusu lini kwa mara ya mwisho tuliuza sina kumbukumbu sahihi hapa kuhusu suala hilo lakini ni muda mrefu kidogo umepita kwa kweli.

**Kulinda Njia za Utalii Nchini**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa utalii ni mojawapo ya njia zinazotumika kuongeza pato la taifa. Je, Serikali ya Tanzania ina mipango gani ya kulinda utamaduni, desturi na hulka za Watanzania hususan vijana walio karibu na vivutio vya utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli utalii ni njia mojawapo inayoliingiza taifa mapato hususan fedha za kigeni. Aidha, utalii hutoa fursa za ajira, Serikali hupata kodi, husaidia kukua na kupanuka kwa sekta ya uzalishaji wa bidhaa na biashara zinazohusiana na utalii kama sanaa, matunda, mbogamboga na usafirishaji. Faida nyingine za utalii ni kukuza mahusiano kati ya watu wa nchi na pia huchangia katika kuleta amani na maelewano kati ya wananchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa pamoja na faida nyingi zinazotokana na utalii, kuna athari kidogo zinazoweza kujitokeza. Katika kulitambua hilo Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 imelenga kuendeleza utamaduni wetu kuwa utambulisho wa utaifa wetu. Katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa Serikali imejiwekea mikakati ifuatayo:-

Kukuza na kuhimiza uendelezaji utalii bila kuharibu utamaduni wa nchi.

Kukuza utamaduni wa nchi na utambulisho wa taifa.

Kuhakikisha tathimini ya athari za jamii na utamaduni (*social impact*) inafanywa mawa kwa mara.

Kuanzisha na kuhamasisha miradi ya utalii wa utamaduni kwa lengo la kuwafanya wenyiji husasan vijana kushiriki na kutathimini utamaduni wao. Utafiti mdogo uliofanywa kwa lengo la kutathmini matokeo ya miradi ya utalii wa utamaduni umeonyesha kuwa kuwepo kwa watalii katika maeneo husika kumeibuka ngoma za jadi zilizokuwa zimesahaulika, vyakula vyta asili teknolojia ya asili na mavazi ya kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa kutambua umuhimu wa kulinda tamaduni za wageni na wenyiji, Shirika la Utalii Duniani (*World Tourism Organization*) liliandaa na kutoa mwongozo wa maadili ya Utalii Duniani (*Global Code of Ethics for Tourism*) mwaka 2001. Nchi yetu kama mwanachama iliridhia na kutafsiri mwongozo huo kwa lugha ya kiswahili ili zieleweke vema.

Mwongozo huo wa maadili, unamweleza mtalii mambo yampasayo na yasiyompasa kufanya awapo katika nchi aliyotembelea. Wizara yangu itaendelea kuchapisha na kuusambaza mwongozo huu.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa jamii, wakuu wa mila mbalimbali na viongozi wa dini kuisaidia Serikali katika kuwaelimisha na kuwahamasisha ili wapende na kuzitathimi mila na desturi kwa ajili ya kudumisha utamaduni wetu ambao pia ni kivutio kikubwa cha utalii.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; pamoa na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini amesema utalii unatuletea faida lakini pia kuna athali kidogo. Kwa hiyo wamewahi kuwafanya semina ili kuepukana na hizi athari ndogo na kama wamewahi. Je, kwa Zanzibar wamefika?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, athali zilizopo au zinazoweza kutokea kutookana na utalii kama tulivyosema ni kwa mfano kwenye athari ya lugha mara nyingi wageni wanakuwa hawatumii lugha yetu kwa hiyo inawafanya watanzania waweze kuwasiliana nao.

Kwa hiyo ndiyo hizo athali ndogo; lakini kutookana na utafiti uliofanyika unaonyesha kwamba wageni wengi wanapenda tamaduni zetu; kwa mfano upande wa kaskazini wageni wanapenda sana mavazi ya kimasai na mimi nafikiri ni vizuri nikawatia shime kwamba tamaduni zetu chakula chetu na mavazi yetu wageni wanayapenda sana.

Tatizo linalosumbua ni sisi kukubali kuacha ya kwiga ya kwao ambayo hasa tunayaona kwenye runinga na si kwamba wale wanaokuja hapa ndiyo wanatuletea.

Mpango wa kuelimisha jamii kuhusu kuimarisha utamaduni wetu umeshaanza na tumeanzia upande wa kaskazini na mpango huu unaendelea vizuri kwa kuanzishwa vikundi mbalimbali. Zanzibar ipo katika mpango wa kipindi kijacho.

Na. 66

### **Kuzuia Kilimo cha Pamba Chunya.**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K. n. y. MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA)** aliuza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005 imesisitiza kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo cha mazao na biashara hapa nchini.

- (a) Je, Serikali haioni kuwa kuzuia kilimo cha zao la pamba Wilayani Chunya mwaka 1995/1996 kutokana na kuwepo funza mwekundu katika maeneo hayo ni kutowatendea haki wananchi hao?
- (b) Je, Utafiti amba Serikali iliahidi kuufanya utamalizika lini?
- (c) Je, funza huyo mwekundu mbona ni wa aina ile ile anayepatikana kwenye maeneo yanayolima pamba katika mikoa ya kati na Kanda ya Ziwa.?

### **WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalil la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

(a) Madhumuni ya kuzuia kilimo cha pamba Wilayani Chunya ni kuzuia kilimo cha pamba Wilayani Chunya ni kuzuia kuenea kwa funza wekundu (*Diparopsis Castanea*) kusambaa hadi maeneo makuu ya uzalishaji pamba Kanda ya Magharibi na Mashariki na nchi jirani Kaskazini mwa nchi yetu. Hii ni njia mojawapo itumikayo sehemu nyingi duniani kuthibiti kuenea kwa wadudu waharibifu wa mimea ambao udhibiti wake ni mgumu, na si kutowatendea haki wananchi wa Wilaya ya Chunya kama alivyoulima Mheshimiwa Mbunge.

(b) Wakati tukijibu swalil namba 460 la Mheshimiwa Benson Mpesya, katika mkutano uliopita kuhusu uanzishwaji wa mashamba madogo madogo ya pamba Chunya, tulilifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba katika Wilaya ya Chunya mashamba ya majaribio yalianzishwa tangu msimu wa 2004/2005. Vijiji vilivyo fanyiwa majaribio ni Mpogoro, Mbala, Ifumbo, Magamba, Kanga Galula na Chong'ombe.

Aidha, tulieleza kwamba matokeo ya awali wameonyesha kuwa funza mwekundu ameonekana katika vijiji vyote hivyo isipokuwa kijiji cha Mapogoro. Ilielezwa pia kwamba yameanzishwa majaribio ya kubaini madhara ya funza mwekundu katika vijiji hivyo. Utafiti huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2008.

(c) Mheshimiwa Spika, funza walioko katika maeneo ya Kanda ya Ziwa ni funza wa vitumba kwa kiingereza *American Bollworm* na kwa kitaalam *Helicoverpa Armigera* na funza mwekundu mweupe kwa kiingereza *Pink Bollworm* na kwa kitaalam *Pectinophora gossypiella* na siyo funza mwekundu kwa kiingereza *red bollworm* na kwa kitaalam *Diparopiss Castanea*.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASYA:** Mheshimiwa Spika, namsukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake fasaha sana. Lakini pamoja na hato, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa funza huyu amedumu Wilayani Chunya kwa zaidi ya miaka kumi pamoja na kwamba kilimo cha pamba kimepigwa marufuku.

Je, Serikali haioni kwamba huyu funza kuna chakula anachokula bdala ya pamba na kwamba ingefaa sasa nguvu zielekezwe katika kuangalia anakula nini ili tuweze kukitekeleza hicho anachokula ili kumuua huyo funza? (*Makofi*)

La pili, kwa kuwa wananchi wa Chunya wamehamasika na kuanza kulima mazao mengine ya biashara kama alizeti na ufuta; Je, Serikali inaweza kuwapa kipaumbele maalum wakakopeshwa matrekta na zana zingine ili waweze kuinua kipato chao?

**SPIKA:** Waheshimiwa, tutaendelea endelea kidogo, yamebaki tu maswali mawili tu mafupi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, katika maeneo haya, kuna kitu kinaitwa pamba pori.

Hiyo pamba pori ndiyo chakula ambacho kinalisha hawa funza na ndio maana wanaishi kule. Wanapendelea pamba pori mahali ambapo hamna pamba ile ya kawaida.

Ukilima pamba ya kawaida, wanahama pamba pori, wanenda kwenye ile pamba yenye. Kwa hiyo, ndio maana wanaishi pale kwa sababu pamba pori ipo pale na ndiyo inayowahifadhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kulima alizeti na ufuta, mimi nawatia moyo kabisa wakulima wa Chunya waendeleze kilimo cha ufuta na kilimo cha alizeti kwa sababu kwanza ni rahisi kulima ufuta na ni rahisi kutunza alizeti hata kuliko pamba. Soko la

mazao haya mawili aliyoyataja Mheshimiwa Mwambalaswa ni kubwa zaidi na linaweza kuwapatia manufaa zaidi wananchi wa Chunya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Wilaya ya Chunya katika kuendeleza mazao haya. (*Makofit*)

Na. 67

### **Mtandao wa Wakulima Wadogo**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa Umoja wa Wakulima wadogo Tanzania (MVIWATA) una mtandao nchi nzima na umeonyesha mafanikio makubwa katika kuwaunganisha na kuwapatia wakulima ujuzi mbalimbali juu ya maendeleo ya kilimo cha mazao mbalimbali usindikaji na ugunduzi huo umekuwa na mtandao nchi nzima kiasi cha kwueza kushiriki maonyesho ya Nanenane 2008 kwa kuleta washiriki kutoka nchi nzima:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutumia mtandao huu wa wakulima wadogo katika maendeleo ya kilimo hapa nchini?

(b) Je, Serikali iko tayari kuziagiza Halmashauri zote nchini kushirikiana na mtandao huo katika programu mbalimbali za miradi ya kilimo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, napenda kwanza kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) ni chombo cha kuunganisha wakulima wadogo ili kuwa na sauti moja katika utetezi wa maslahi yao. Mtandao huo ulianzishwa mwaka 1993 na wakulima wadogo wabunifu kutoka Mikoa ya Morogoro, Iringa, Tanga, Kilimanjaro, Mbeya na Dodoma. Hivi sasa MVIWATA imesajiliwa kama asasi isiyo ya kiserikali. Malengo ya MVIWATA ni pamoja na:-

·Kuwezesha mawasiliano mionganoni mwa wakulima wadogo ili kujenga kwa pamoja mbinu na mikakati ya ushawishi na utetezi kwa maslahi ya wakulima wadogo.

·Kubadilishana mawazo, ujuzi na uzoefu juu ya kilimo na shughuli mbalimbali za wakulima ili kuboresha maisha yao.

·Kuwakilisha wakulima wadogo katika mashauriano na Serikali juu ya masuala mbalimbali yanayohusu maslahi ya wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) MVIWATA ni asasi isiyo ya kiserikali na Serikali na Sera ya Serikali ni kushirikiana na wadau wote nchini katika kuleta maendeleo ya nchi, hivyo Serikali iko tayari na imekuwa ikishirikiana na MVIWATA katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) ipo fursa ya kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma mbalimbali kwa wakulima.

Hivyo kwa kutambua mchango wa MVIWATA, Halmashauri za Wilaya zote nchini zinashauriwa kutumia fursa zilizopo chini ya *ASDP* kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADP's*) kushirikisha MVIWATA pamoja na asasi zingine zisizo za Kiserikiali katika kutekeleza programu mbalimbali za miradi ya kilimo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Spika, mwaka huu katika maonyesho ya Nane Nane, Mtandao huu walifanya maonyesho yao na walikuwepo wawakilishi wa kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, mimi nilibahatika kutembelea na niliona mambo mazuri sana ikiwa ni pamoja na usindikaji na kubadilishana ujuzi wanaofanya. Waziri amekiri hapa kwamba ushirikiano huu kti ya Serikali na mtandao huu utaendelea kuwepo. Mheshimiwa Spika, Mbinga na Chunya, Halmashauri zile zimefanya vizuri sana kwa sababu ya mahusiano hayo.

Je, Mheshimiwa Waziri au Serikali iko tayari kuziagiza Halmashauri zote nchini kupitia Mradi wa *ASDP* kuhakikisha kwamba wanashirikiana na Mtandao huu kupitia bajeti tu ya mwaka huu tuliyoitisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hata katika Mradi wa kilimo DADPS ziko fedha nyingi ambazo zinatumika vibaya na Halmashauri kwa kufanya mashamba darasa na vitu vinavyofanana na hivyo ambavyo havina tija; Je, Waziri yuko tayari pia kupitia *DADPS* kushirikiana na Mtandao huu kwa sababu tayri unafanya vizuri na unazalisha mazao na unafanya usindikaji? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwa sababu hata katika jibu langu la msingi nimesema, Halmashauri za Wialaya zishirikiane na MVIWATA ili huduma hii inayotolewa na MVIWATA iweze kuenea nchi nzima. Na mimi nimewahi kutembelea baadhi ya

shughuli ambazo zinafanywa na MVIWATA, kwa mfano katika Mkao wa Iringa ambako nilishuhudia wamejenga masoko na kutoa nafasi kwa wakulima kuleta mazao yao ili yaweze kupata soko badala ya kufuatwa na wanunuzi nyumbani. Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa na huduma nzuri inayotolewa.

Pili, kuhusu suala la fedha kutumiwa vibaya katika Halmashauri na kwamba badala ya kutumiwa vibaya, zitumiwe kwa kushirikiana na MVIWATA. Mimi nadhani fedha zinazokwenda kw nye Halmashauri zinasimamiwa na Halmashauri yenyewe na Halmashauri ndiyo inayoweka taratibu ya namna ya kuzitumia. Ushauri ninaoweza kuutoa ni kwamba washirikiane na MVIWATA ili waone *approach* ya MVIWATA inavyoweza kusaidia wakulima wadogo. Lakini hii haina maana kwamba waache mfumo wa shamba darasa kwa sababu shamba darasa nao ni mpango mahsus wa kusaidia kufikisha maarifa kwa wakulima. Kwa hiyo, hii ya MVIWATA haiwezi kuwa bdala ya shamba darasa.

Na. 68

### **Uzalishaji wa *Sponge Iron*.**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa wizi wa nyaya za simu na umeme kwenye barabara na njia za reli pamoa na mifuniko ya chemba za mifereji ya maji taka na ya mvua mijini kwa sehemu kubwa kunachangiwa na uhaba mkubwa wa chuma chakavu.

Je, kwanini Serikali isitenge eneo la milima ya chuma cha Liganga huko Ludewa ili kuzalisha *Sponge Iron* badala ya chuma chakavu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuanzisha kiwanda mama cha chuma hapa nchini kwa kutumia rasilimali iliyopo Liganga kuzalisha chuma ghafi (*sponge iron*) ili kukidhi mahitaji ya chuma ndani ya nchi na kuzalisha chuma maalum kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya nchi.

Aidha, uanzishwaji wa kiwanda mama cha chuma hapa nchini utachochea maendeleo ya viwanda vingine nchini hivyo kukuza uchumi wa taifa na vile vile kupunguza matumizi ya chuma chakavu. Vilevile ndani ya mwamba wa chuma cha Liganga kuna madini ya *vanadium* na *titanium* ambayo yana thamani kubwa soko la kimataifa kuliko hata chuma.

Hivyo mkakati wa Serikali ni kumpata mwekezaji binafsi mwenye uwezo wa kuzalisha madini yote yanayopatikana ndani ya mwamba wa chuma cha Liganga kwa kuanzia na uzalishaji wa *vanadium* na *titanium* kwa ajili ya kuza katika soko la kimataifa. Utekelezaji wa mradi huu unahitaji mtaji mkubwa sana. Ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kukopa na kisha kulipa madeni, mkakati uliopo ni kuutekeleza mradi huu kupitia wawekezaji binafsi au ushirikiano kati ya sekta binafsi na ya umma.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji kadhaa wakiwemo wa ndani na wa nje ya nchi wamewasilisha maombi yao kutaka kuendeleza mradi huu, hivi sasa Serikali inayapitia maombi yao ili kumpata mwekezaji mwenye sifa zinazokubalika kwa lengo la kuzalisha madini yote yanayopatikana katika Chuma cha Liganga yakiwemo *vanadium*, *titanium* na chuma kwa ajili ya manufaa ya taifa. Serikali pia inalifanya kazi wazo la Mheshimiwa Mbunge, Prof. Mwalyosi la kuona kama kuna uwezekano wa kutumia sehemu ya milima ya Liganga kwa uzalishaji wa *sponge iron* (chuma ghafi) badala ya kutekeleza mradi wote kwa pamoja. Mapendekezo ya wazo hili yameishapita ngazi ya watalaan wa Shirika letu la *NDC* na wale wa Wizara ya Viwanda na yapo tayari kupelekwa Baraza la Mawaziri kwa uamuzi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza licha ya majibu mazuri ya Mheshimiwa naibu Waziri. Kwanza, ninayo barua hapa ambayo aliandika Mheshimiwa Mramba alipokuwa Waziri wa Viwanda na yeze katika barua nilioandikiwa alisema, *NDC* ni lazima ionyeshe matokeo ya mchakato wa kasi mpya ambayo ni kuzalisha *sponge iron* ifikapo 2010. Leo tumebakiza mwaka mmoja, nataka kujua kwa *speed* hii ya pole pole ya Serikali, ni kweli tutaweza kuzalisha *sponge iron* ifikapo 2010? Swali la pili; tumezungumzia juzi kuhusu Kamati ya Madini iliyoweka na Serikali na amehimiza fidia kutolewa mapema kwa wananchi kabla ya kuanza miradi na kuitekeleza. Mchakato huo ulianza katika Mchuchuma na Liganga, sasa hivi umesimama; Je, udhani mchakato huo utaweza kukamilika kabla ya kuanza mradi wa chuma ghafi na mradi wa chuma cha *steel*? Mheshimiwa Spika, asante!.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu, yeze anasema speed ndogo yaani kasi ambayo siyo kubwa; ni kweli Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Mramba aliandika hivyo na ni kweli tunakiri kwamba msimamo wa Wizara yangu ni huo huo kwamba mpaka 2010 tuweze kuonyesha kwamba kuna jambo kubwa limefanyika katika uendelezaji wa miradi hii ya Mchuchuma na Liganga. Sasa kuhusu hiyo hiyo anasema ni *speed* ndogo; sisi tungependa hata mradi uanze leo, lakini lazima tuangalie maslahi ya Taifa, mpaka apatikane mtu ambaye kwa kweli akizalisha pale, atapata faida yeze, lakini Watanzania watapata faida. Kama atakosekana mtu ama watakosekana watu ambao tunakubali kwamba wanafaa, ni afadhali tukachelewa hata miezi miwili/mitatu wakapatikana wale ambao wanafaa, baadae tukaepuka kuja kulaumiana kwamba labda Wizara hatukuwa makini, Serikali hatukuwa makini. La pili; kuhusu hii Kamati ya Madini la ulipaji wa fidia, napenda nimtoe wasi wasi Mheshimiwa Mwalyosi, maana swali hili ameniuliza Ijumaa iliyopita, nimelifuatilia. Kwa kweli nimekuta kwamba mchakato wa ulipaji wa fidia ahujasitishwa bado.

Sasa hivi ni kwamba Shirika letu la *NDC* pamoja na watalaan wa Wizara wanawasiliana na wananchi wa pale Mkomang'ombe ambako ndiko kunahitaji kulipwa fidia na wanachofanya pale kwanza ni kutathmini ni mali ipi inapaswa kulipwa fidia na kwa kiasi gani. Hili litawafanya wananchi kutokuja kulaumu baadae kwamba labda walilipwa kidogo. Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza tathmini hiyo, Wizara yangu itaandika barua Hazina kuomba fedha kwa ajili ya kuwalipa hao wananchi ambaa itabidi waachie miradi hiyo miwili iendelee.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru! Nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa biashara ya chuma chakavu imepamba moto sana hapa nchini. Wale wanaouza chuma chakavu huwa wanavunja madaraja, mifuniko ya kufunikia mifereji ya maji machafu pamoja na hata vibao vya matangazo vya biashara huwa wanavichukua nakwenda kuwauzia wale wanaonuna chuma chakavu. Swali langu ni kwamba Je, Serikali iko tayari sasa kufuta kabisa biashara hii ya chuma chakavu mpaka hapo Serikali itakapotengeneza kiwanda mama kwa ajili ya sponge *iron* kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kabisa na baadhi ya Wabunge ambaa walishalileta suala hili Bungeni kwamba biashara ya chuma chakavu kwa kweli, japoilanzishwa kwa nia nzuri, wapo watu ambaa wanaitumia kwa malengo ambayo sivyo kama tulivyokuwa tumepanga. Na kwa sababu suala hili lina *interests* mbali mbali Wizara yangu imejipanga sasa, hivi tunavyoongea ni kwamba katika Baraza la Mawaziri lijalo, tutawasilisha pale kwa ajili ya kupata ushauri wa Baraza la Mawaziri kuona nini kifanyike, ama kama ni kufuta kabisa hiyo biashara, tuone kwamba kufuta kwake hakutaleta madhara makubwa kuliko faida ambayo itapatikana kwa kuifuta. Lakini vile vile, jambo ambalo nimelisema katika jibu la swali la msingi ni kwamba tutakaporuhusu uzalishaji wa sponge iron kwa huyu mwekezaji ambaye amepatikana, litakuwa ndio ufumbuzi wa kudumu wa tatizo kwa sababu chuma ikishapatikana kwa wingi na kwa bei rahisi, itapunguza tamaa ya watu ya kwenda kung'oa reli namiundombinu mingine ambayo Mheshimiwa Owenya anasema. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Owenya atupe nafasi, Baraza la Mawaziri, siku za karibuni litatoa uamuzi na baadaye Bunge lako Tukufu litaarifiwa rasmi.

**SPIKA:** Mniwie radhi Wabunge, Mheshimiwa Hoogan Singh kwa kawaida haulizi uliz maswali. Sasa leo napata shauku na kwa hiyo namruhusu. Swali la nyongeza Mheshimiwa Hoogan Singh!

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, kuna taarifa ya kwamba huo mlima amekodishwa mtu binafsi. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

**SPIKA:** Majibu! Naona mtu asiyeuliza, siku akiuliza ni hatari tupu! Mmekodisha mlima mzima kwa mtu binafsi? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, hatuna taarifa yoyote katika Wizara yangu au ndani ya Serikali kwamba mlima

huu umekodishwa kwa mtu binafsi, mtu mmoja. Kama nilivyo sema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba mchakato unaendelea. Kwanza, mchakato wa kuzalisha ile chuma pamoa na yale madini ya vanadiaum na titanium kwa sababu yale madini ya aina mbili yana thamani kubwa sana, lakini kutoka na lile ambalo Mheshimiwa Owenya alikuwa ameuliza hapa la chuma chakavu, tukaona kwamba ni afadhali tukatenga kaeneo kadogo hako katumike kuzalisha chuma (*sponge iron*) ambayo haitahitaji kutenganisha hiyo vanadium na titanium kwa ajili ya kuuza katika soko la ndani kupunguza matumizi ya chuma chakavu. Sasa hajapatikana mtu huyo. Kwa hiyo, taarifa hizo napenda nizikanushe kwamba siyo sahihi, akipatikana, atatangazwakwa utaratibu amba o ni wa uwazi na wa ukweli.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Muda wa Maswali umepita kabisa na maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo na kama kawaida tutaanza na wageni wetu wa leo. Mgeni wa Mheshimiwa Juma Killimbah ni Mchungaji, Mzee Thomas Mussa Kipenka, ambaye ni Baba Mzazi wa Katibu Mstaafu wa Bunge, Jaji Kipenka Mussa. Aaah, Mzee, ahsante sana! Karibu sana Mzee Thomas Mussa. (*Makofi*)

Tunashukuru kwamba tunaendelea kufaidi busara na hekima zako za utumishi mwema sana katika nchi hii. Karibu sana baba! (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Pro. Philemon Sarungi ni Waheshimiwa Madiwani wafuata o amba o nadhani watakuwa wanatoka Rarya, Jimbo lake...

**MBUNGE FULANI:** Tarime!

**SPIKA:** Hawa ni wa Tarime?

**WABUGE FULANI:** Eeh!

**SPIKA:** Ooh, ni vema tu! Mheshimiwa Sylvester Mrwa, Diwani wa Manga, Mheshimiwa Anthony Manga, Diwani wa Sirabi, Mheshimiwa Abdi Gasaya, Diwani wa Mriba na Mheshimiwa Eliza Mseti, Diwani Viti Maalum. Ahsante! Karibuni sana, karibuni sana na pole na safari ndefu na bila shaka pole pia kwa kampeni, nasikia ilikuwa kampeni ya nguvu sana huko. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Castor Ligallama ni Ndugu Jungu Pius Jungu ambaye ni msaidizi wake Jimboni. Nadhani ukiwa na msaidizi anaitwa jungu, hata majungu hayawez i kupanya! Karibu sana! (*Kicheko/Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge ni Mheshimiwa Erika Sanga, Diwani Viti Maalum Bulongwa na ni Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Makete. Karibu sana mama! Nakupongeza pia umeavaa nguo nadhifu sana! (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene ni...leo tuna bahati, Mheshimiwa Zeli Mtuta, Diwani Viti Maalum, Kata ya Lumuma na Ndugu Moses Makamba, Mwenyekiti wa Wazazi Kata hiyo hiyo ya Lumuma. Karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Zuleikha Yunnus Haji ni Bi. Safia Juma ambaye ni mama mzazi wa Mkurugenzi wa NSSF, Dr. Dau. Na Bi. Ashura Juma, nadhani ni ukoo mmoja. Karibuni sana!

Mwisho, tunao wanakwaya 34 kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Kipawa Dar es salaam, ningeomba wasimame! Ahsante sana. Karibuni sana kutoka Kipawa. Natumaini mnaendelea na kazi yenu njema ambayo tunaifahamu na sisi wengine amba ni madhehebu yenu, tunaifahamu sana kazi mnayoifanya. Kama mmekuja na kanda, basi baadaye msaidizi wangu atakuja kununua, iwe ya CD au nyingine yoyote. Karibuni sana na mbarikiwe sana.

Matangazo ya kazi zetu sasa; Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira, m Kutane leo tarehe 3/10/2008 saa 5.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani mna wageni maana ukumbi huu ni mkubwa.

Kwa hiyo, wajumbe wote wa Kamti ya Ardhi, Maliasili na mazingira, saa 5.00 asubuhi, hii leo, Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea malalamiko kidogo kuhusu mpangilio wa Miswada kwamba kwenye orodha iliyotangulia ilikuwa inaonekana kama Miswada kwa jina fulani, jina la Muswada fulani, baadaye inatokea mabadiliko. Kwa kweli, kwa upande wetu Ofisi ya Spika ni vigumu kulazimisha Muswada fulani lazima uje kwa mpangilio ule ule kwa sababu Serikalini nao wanapatwa na mambo mengine.

Kwa mfano, Waziri mhusika anaweza kuwa amesafiri, ni dhahiri huwezi kuleta Muswada. Ndiyo maana kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Chiligati tulitanguliza Miswada yake kwa sababu kesho anatakiwa awepo China kwa kazi za Taifa.

Kwa hiyo, naomba tuvumiliane tu na nawasihi Waheshimiwa Wabunge mnapojianda kwa Miswada, unajiandaa kwa Miswada yote, yaani ukipata nafasi uweze kuchangia. Tukiwa na Miswada mitano au sita, wewe ukakaa tu na mmoja, umeng'ang'ania kabisa, sasa usipotokea katika siku ile inayohusika, inakuwa shida kidogo.

Lakini, mimi naamini wote mna uwezo mzuri tu. Kwa hiyo, tuvumiliane na tuisaidie Serikali katika kuona kwamba ratiba zao nao huwa zinaingiwa kutohana na matatizo mbali mbali.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama wa Mwa 2008** *(The Animal Welfare Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Act, 2008*) pamoja na Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*).

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuwasilisha Muswada huu, napenda nichukue nafasi hii kutoa shukrani nyingi kwa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uongozi na Uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo kwa kazi nzuri walizofanya katika kushauri na kutoa maelekezo mazuri wakati tukiuardaa Muswada huu wa *The Animal Welfare Act, 2008*.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda pia nitoe shukrani kwa wadau wa sekta ya mifugo na vyama mbali mbali vinavyohusika na masuala ya *Animal Welfare* kwa jinsi walivyoshiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba Muswada huu unafanikiwa.

Lakini pia, napenda nitoe shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Anthony Diallo aliyejewa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo pamoja na Naibu wake Charles Mlingwa ambao kwa kweli walishiriki kikamilifu katika hatua za mwanzo katika kuuandardaa Muswada huuna kazi zao zimefanikisha sana katika kuuleta Muswada huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Bill, 2008*) unakusudia kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia uzingatiaji na utekelezaji wa kanuni za ustawi wa wanyama katika ufugaji hapa nchini.

Aidha, Muswada huu una mahusiano ya karibu na ule Muswada ambao umepitishwa na Bunge unaohusika, Muswada wa Baishara ya Ngozi. Mheshimiwa Spika, sheria hii itawezesha kuondoa, kuzuia na kupunguza mateso na unyanyasaji wa wanyama. Mateso na unyanyasaji wa wanyama haswa kwa mifugo kisayansi hupunguza

viwango vya uzalishaji na ubora wa mazao yatokanayo na mifugo husani nyama, maziwa na ngozi.

Mheshimiwa Spika, Ustawi wa wanyama ni dhana pana kuliko ilivyo uzuiaji wa ukatili kwa wanyama na unapaswa kutofautishwa na Haki ya Wanyama (*Animal Rights*) ambao si kusudio la kutungwa sheria hii.

Aidha, dhana hii inapewa umuhimu mkubwa duniani hivi sasa na inasisitizwa kimataifa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*), Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organization*) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (*World Organization for Animal Health*). Ustawi wa Wanyama unalenga maeneo matano ya msingi yafuatayo kwa wanyama:-

- Kuwapatia chakula, maji na kukidhi mahitaji yao ya msingi;
- Kutowaogopesha na kuwasumbua;
- Kuwaondolea dhiki na mateso ya mwili;
- Kuwaondolea maumivu, majeraha, kuwakinga na kuwatibu; na
- Kuwapa uhuru wa kuonyesha tabia halisi.

Mheshimiwa Spika, sheria ya Ustawi wa Wanyama inayopendekezwa kutungwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 Ibara 3(19) inatamka kuwa:-

*“Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha, itaimarisha utoaji wa huduma na kuratibu utekelezaji wa misingi ya ustawi wa wanyama”.*

Mheshimiwa Spika, pia, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005-inatamka katika sehemu 32 (e) kuwahimiza wafugaji kutekeleza kanuni za ufugaji bora na kwa ujumla kuwawezesha kuingia katika ufugaji wa kisasa na 32 (f) kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia ufugaji endelevu usiohariblu mazingira, rasilimali muhimu kama ardhi na vyanzo vya maji kote nchini, hivyo inasisitiza uzingatiaji wa ustawi wa wanyama na udhibiti wa uzururaji wa mifugo. Kanuni za ufugaji bora zinapozingatiwa ustawi wa wanyama unaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya ustawi wa wanyama nchini kwa sasa nchi yetu ina mifugo ng'ombe milioni 18.8, mbuzi milioni 13.5, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.4, kuku milioni 53 na mbwa milioni 4.0. Uzingatiaji wa kanuni za ustawi wa wanyama

katika ufugaji hapa nchini ni hafifu hivyo kulalamikiwa kuwa wanyama huteswa, hunyanyaswa, kutokujaliwa au kutothaminiwa na wanao wamiliki.

Mheshimiwa Spika, Vitendo nya kuning'iniza kuku, kupakia mbuzi kwenye vitako nya baiskeli huku wamefungwa, kupiga wanyama kwa ukatili, kusafirisha wanyama kwenye buti za magari, kurundika wanyama wengi kwenye nafasi finyu ya nyumba au magari au mabehewa ya treni, kusafirisha wanyama umbali mrefu pasipo kuwapatia maji au malisho, kugombanisha wanyama na uwekaji wa wanyama katika mazingira ya mateso kama kuwa katika tope, kufungwa na kamba fupi au upigaji wa chapa sehemu kubwa ya mwili vimeenea sehemu kubwa nchini.

Aidha, uzururaji wa mifugo mjini na vijijini, ajali za wanyama barabarani na uchafuzi wa mazingira kutokana na uzururaji huu na mizoga ya wanyama inayoachwa bila kuondolewa mapema umekuwa kero na unahatarisha afya ya jamii.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kupunguza na kuzuia vitendo hivi zinakwamishwa na sheria zilizopo za *Animal (Protection) Ordinance Cap* 153 na sheria ya *Animal (Pounds) Ordinance Cap.* 154 ya mwaka 1930 kuwa na adhabu ndogo, kulenga vipengele vichache na hivyo kupitwa na wakati.

Sheria hizi za zamani zina mapungufu ya kutokuwa na mfumo mzuri wa usimamizi hususan wa kuwa na wakaguzi, kutokuwepo kwa chombo cha ushauri na kutobainisha mgawanyo wa majukumu kati ya Serikali kuu, serikali za mitaa na sekta binafsi na hivyo utekelezaji wake umekuwa hafifu.

Mheshimiwa Spika, Aidha, hali hii imechangiwa pia na elimu duni ya ufugaji, kutozingatia kanuni za ufugaji bora, usafirishaji na uchinjaji usio wa mateso na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo idadi ya jamii ya Watanzania inayojali ustawi wa wanyama imeongezeka na hii inadhihirishwa na idadi za asasi za kiraia zinazosimamia ustawi wa wanyama kuongezeka kutoka iliyokuwepo na kufahamika na wengi kama *Tanzania society for prevention of curerity of animals, (TSPCA)* hadi saba kwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, asasi hizo ni pamoja na:- *Tanzania Animal Protection Organisation, TAPO, Tanzania Society for Animal Welfare (TAWESO), Arusha Society for Protection of Animals (ASPA) Sea Sands Roots and Shoots na Dar es salaama Animal Heaven (DAH)*. Kutokana na mwamko huu mwaka 2006 Asasi ya Kimataifa ya ustawi wa wanyama *World society for protection of animal (WSPA)* imefungua ofisi ya Kanda ya Afrika nchini kwetu na hivyo kuihamisha kutoka Mombasa Kenya.

Mheshimiwa Spika, asasi hizo kwa pamoja zimekuwa zikifutilia na kuishauri Serikali na jamii kwa ujumla kujali na kuwaenzi wanyama kwa kuzingatia ustawi wao, hivyo msukumo wa kuwa na sheria mpya, pana umetokana na matakwa ya jamii, hadi sasa Watanzania wapatao 43,000 wameridhia kwa kusaini kampeni ya kutaka kuwepo kwa tamko la umoja wa mataifa juu ya ustawi wa wanyama *Universal Declaration of*

*animal welfare (UDAW)* Tanzania ikiwa ni ya pili Barani Afrika baada ya Afrika ya Kusini.

Mambo muhimu ya Muswada huu; mambo muhimu yaliyozingatiwa katika muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuundwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri wa Ustawi wa Wanyama (*Animal Welfare Advisory Council*) litakalotoa ushauri kuhusu masuala ya ustawi wa wanyama.
- (ii) Kuainisha aina za wanyama wa kufugwa na taratibu za namna ya kuwahifadhi, kuwatunza, kuwasafirisha na kuwahudumia wapatapo matatizo, pia taratibu za kuchinja wanyama pasipo kuwasababishia mateso.
- (iii) Kuainisha taratibu za kutumia wanyama katika kazi na michezo.
- (iv) Taratibu za upasuaji wa wanyama na matumizi ya wanyama katika tafiti mbalimbali za kisayansi zimeainishwa.
- (v) Kubainisha namna ya kuangalia na kuhifadhi wanyama wakali na wazururao.

Mheshimiwa Spika, matarajio baada ya kutunga sheria; Sheria hii itakapotungwa itasimamia kwa ufanisi utekelezaji wa kanuni bora za ufugaji sambamba na kuzingatia ustawi wao na hivyo kuongeza uzalishaji, ubora na tija katika sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, sheria hii inatarajia kuwa na matokeo yafuatayo:-

- (a) Tanzania kushiriki katika biashara ya mifugo na bidhaa zinazotokana na wanyama kimataifa baada ya kutambuliwa kuwa na viwango vya ustawi wa wanyama kulingana na masharti ya Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organization*) chini ya makubaliano ya Kilimo (*Agreement on Agriculture*) na nchi wanachama ikiwa pamoja na Tanzania.
- (b) Kuongeza uzalishaji wenyе tija wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo hususani nyama na ngozi kwa kupunguza uharibifu wa nyama utokanao na michubuko, kuumia kwa mifugo, mabadiliko ya kemikali kwenye misuli (*glycogen & lactic acid levels*) na chapa za moto kwenye ngozi.
- (c) Kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira, usumbufu na uharibifu kwa wananchi na mali zao kutokana na wanyama wanaozurura.
- (d) Kujenga mahusiano mazuri kati ya binadamu na wanyama.
- (e) Wanyama wataishi kulingana na hisia zao.
- (f) Sheria kuwa katika muundo mpya wa nyanja pana ya kujali wanyama kutoka kulinda (*Protection*) na kuzuia (*Prevention*) ukatili kwa wanyama.

(g) Italenga wanyama wanaofugwa hivyo kuondoa kuingiliana na sheria zinazosimamia wanyama wengine. Wanyama wafugwao ni pamoja na ng'ombe, mbusi, kondoo, nguruwe, ngamia, kuku, farasi, punda, mbwa na paka.

(h) Kuwepo kwa Baraza la Ushauri la Ustawi wa Wanyama.

Mheshimiwa Spika, mpangilio wa sehemu za Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu nane zinazopendekeza mambo mbalimbali kuhusu ustawi wa wanyama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza (vifungu 1-4). sehemu hii inaeleza jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria , matumizi yake, ufanuzi wa maneno na misemo yenye maana maalum katika sheria inayopendekezwa pamoja na kuainisha dhana na misingi ya ustawi wa wanyama.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili (vifungu 5 -10); Sehemu hii inapendekeza kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri wa Ustawi wa Wanyama na majukumu yake. Aidha sehemu hii pia inaeleza uteuzi , mamlaka na majukumu ya Wakaguzi (*inspectors*) wa Ustawi wa Wanyama.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu (vifungu 11-32 ). Sehemu hii inapendekeza masharti kuhusiana na usimamizi na utunzaji wa wanyama mbalimbali kama vile wanyama wa kufugwa mashambani na wanyama wa kufugwa majumbani. Aidha sehemu hii inaelezea taratibu za kuzingatia katika Usafirishaji wa wanyama, utunzaji wa wanyama walioumia na taratibu za kuzingatia wakati wa uchinjaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne (vifungu 33-36). Sehemu hii inahusu utaratibu wa kuwatumia wanyama katika kazi au michezo pamoja na kuzuia michezo ya kugombanisha wanyama (*Animal fights*).

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano (vifungu 37-48); Sehemu hii inapendekeza masharti katika upasuaji wa wanyama, utumiaji wa wanyama ktika teknolojia-viumbe pamoja na masharti katika uchunguzi wa kisayansi wa wanyama.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita (vifungu 49-58); Sehemu hii inapendekeza kuwepo kwa usimamizi, uhifadhi wa wanyama wakali na wanyama wazururao, Hatua za kuchukuliwa kupunguza tatizo la wanyama wazururao hovyo pia zimeainishwa.

Mheshimiwa Spika sehemu ya saba (kifungu 59). Sehemu hii inabainisha makosa na adhabu chini ya sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane (vifungu 60-64). Sehemu hii inahusu masuala ya ujumla kama vile:-

- (a) Mamlaka ya Waziri kutunga kanuni.
- (b) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Ustawi wa Wanyama kutoa adhabu kwa baadhi ya makosa (*compounding offences*).
- (c) Inafuta Sheria ya Kulinda Wanyama (*Animal Protection*) Na 153 ya Mwaka 1926 na Sheria ya Kuhodhi Sehemu Maalum Wanyama (*Animal Pound*) Na 154 ya Mwaka 1930.

Mheshimiwa Spika, Mwisho; muswada huu ulijadiliwa na kamati pamoja na wadau mbalimbali na kutolewa maoni na ushauri. Maoni na ushauri huu umezingatiwa na hivyo kuandaliwa jedwali la marakebisheso (*Schedule of Amendments*) ambalo linawasilishwa kwa ajili ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge na naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, sasa nitamwita Mwenyekiti, wa Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji au Mwakilishi wake naona ni Mheshimiwa Teddy Kasela Bantu kwa niaba ya Mwenyekiti karibu sana.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Spika Ahsante, kwa niaba yangu na familia yangu, na wananchi wa Jimbo la Bukene napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muweza wa yote kwa kutuwezesha kutulinda, tuongoza hadi kufikia siku hii ya leo, sifa na utukufu namrudishia yeye aliye juu, nasema Deogratius yaani tumshukuru Mungu kwa kila jambo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu muswada wa sheria ya ustawi wa wanyama (*The Animal Welfare Bill, 2008*).

Mheshimiwa Spika, Utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Gideoni Cheyo, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugona Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Bill, 2008*).

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Bunge Toleo la Mwaka 2007, Kamati ilipata fursa ya kuupitia na kuuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa Maoni na Mapendekezo, kwa Serikali juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Muswada huu, katika hatua za uchambuzi, umeshirikisha Wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wadau walioshiriki ni Wafugaji, Wachinjaji, Wafanya Biashara, Bodi na Viwanda vya Nyama, Vyombo vya habari na Wanasheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati inaridhika na Maudhui na Madhumuni ya Muswada. Kamati ilishauri Serikali kuzingatia baadhi ya Maoni ya Wadau na ilipendekeza marekebisho katika baadhi ya vifungu vya Muswada.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Maoni ya Kamati pamoja na yale ya Wadau yamezingatiwa katika Mabadiliko ya Muswada yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika hotuba yake ya kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Muswada; Wanyama, kama ilivyo kwa viumbwe wengine, wana haki ya kupata huduma muhimu wanazostahili, kama vile Matibabu, chakula, maji safi, muda wa Mazoezi na kutopigwa ovyo.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa Wanyama wamekuwa wakikumbana na matukio ya ukatili hususan wakati wa kuwasafirisha, jambo linalochangia kupata majereha na wakati mwingine kufariki.

Mheshimiwa Spika, Changamoto. Changamoto zinazoikabili Sekta ya Mifugo zilielezwa katika taarifa ya Kamati yetu tuliyoiwasilisha wakati wa kujadilli Muswada wa Biashara ya Ngozi. Hapa tunapenda kusisitiza machache kuhusiana na ustawi wa Wanayama.

(a) Wafugaji wengi hawawathamini wanyama wao na huwatesa kwa kutowapa makazi bora, lishe bora, maji ya kutosha na kuwapiga kwa fimbo zinazowaumiza, na kadhalika.

(b) Miundombinu ya usafirishaji wanyama ama ni mibovu au haipo na kwa hiyo wanyama husafirishwa katika mazingira magumu. Hali hii inaathiri ustawi wa wanyama.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; ili malengo na madhumuni ya Muswada huu yaweze kutekelezwa, Kamati inaona ni muhimu kwa Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kutokana na mila, desturi, na mazoe ya Wananchi walio wengi, dhana hii ya Ustawi wa Wanyama kama inavyoiezwa, katika Muswada huu ni ngeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo upo umuhimu mkubwa wa kuwa na mpango mahsus wa Elimu kwa Umma kuhusu maudhui ya Muswada huu. Wananchi waelimishwe kuhusu:-

- (a) Haki ya Kuishi kwa wanyama.
- (b) Kuwa na mazingira mazuri ya kufugia wanyama.
- (c) Kuzingatia matunzo mazuri na kuzuia ukatili wa Wanyama.
- (d) Kama ilivyo kwa Wakulima, Wafugaji nao waendelee kupewa ruzuku kwa pembejeo wanazohitaji.
  - (ii) Ili wafugaji waweze kufuga na kutunza mifugo yao kwa ubora unaotakiwa, ni muhimu kwa Serikali kuendelea kuboresha huduma za ugani hadi vijijini ambako wafugaji wengi wanaishi.
  - (iii) Ili sheria hii iweze kueleweka kwa wadau wote, ni muhimu mara baada ya kupitishwa, hatua za haraka zichukuliwe kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili.
  - (iv) Serikali za Mitaa watunge Sheria Ndogo ambazo zitaenda sambamba na sheria hii ili kurahisisha utekelezaji.
- (v) Serikali iajiri Maafisa watakaoshughulikia ustawi wa Wanyama.
- (vi) Kuwepo na Wakaguzi wa Mifugo kuanzia ngazi ya Kijiji ili kusimamia ustawi wa Wanyama.
- (vii) Serikali ihakikishe inahamasisha uanzishwaji na ufufuaji wa asasi za kiraia zinazoshughulikia ustawi wa Wanyama. Aidha, elimu ya Ustawi wa Wanyama itolewe mashulenzi na viundwe vyama (*clubs*) kwa Wanafunzi ili wapate makuzi ya kuwa na huruma kwa Wanyama.
- (viii) Wakaguzi wa Mifugo pamoja na askari wa barabarani (*Traffic Police*) wafahamu umuhimu wa kuwa na walinzi wa mifugo yaani wafanya biashara wa mifugo, katika magari wanayosafirishia.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kamati yangu inapenda kumshukuru sana Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu Waziri, Mhe. Dr. James Wanyancha, pamoja na wataalamu wao kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri kwa Kamati. Aidha, Kamati inawashukuru Maofisa kutoka kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wote walioitikia wito wa kushiriki katika vikao vya mashauriano na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao wametoa maoni katika

kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati, wakati wajumbe wengine ni Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallamam Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye na Mheshimiwa Said J. Nkumba. Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Charles N. Keenja na ,Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu ambaye ndiye ninayesoma taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Frank Mbumi na Ndugu Pamela Pallangyo kwa huduma zao kwa Kamati na kwa kuhakikisha kwamba maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mia kwa mia Muswada huu na naomba kuwasilisha (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji. Sasa ni zamu ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba iliyowasilishwa ya Muswada huu wa Ustawi wa Wanyama.

**MHE. MWADINI ABAS JECHA - MSEMADI MKUU KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Utukufu kwa kunipa uhai na afya njema siku ya leo, nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86 (6) toleo la mwaka 2007, kuhusu Muswada wa sheria ya Serikali, ya Ustawi wa Wanyama, *The Animal Welfare Bill*, 2008

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Wataalamu wote kwa ujumla wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu kwa kuleta Muswada huu wa Ustawi wa Wanyama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kuwa kwamba umezingatia umuhimu, na nafasi ya wanyama kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha nichukue nafasi hii nami kuwapongeza wadau mbali mbali waliojitokeza kutoa maoni yao kuhusu muswada huu, maoni ambayo yamekuwa na manufaa katika kuuboresha, bila kuwasahau Waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuupitia na kuujadili Mswada huu.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu amewaumba wanyama na kuwateremsha duniani kwa ajili ya matumizi ya Mwanadamu, Wanadamu kwa upande wao wamekuwa wanawatumia wanyama hao kwa manufaa yao tangu enzi ya zama za Dahri.

Mheshimiwa Spika, Baada ya Mwanadamu kujua faida ya wanyama akafanya maamuzi ya kuwasogeza karibu naye ili kupunguza usumbufu katika kuwatumia wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba Mwanadamu amekuwa anafaidika sana kutokana na wanyama hao, Faida hizo ni pamoja na nyama, maziwa, ngozi, manyoya, mabawa, nguvukazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana Mwanadamu haonyeshi shukrani kwa wanyama hao na badala yake wanyama wanaambulia kunyanyaswa, kuadhibiwa na kutopewa haki zao kama viumbe vyta Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tumekuwa na Sheria inayolinda haki ya wanyama, Sheria hii imekuwa ni ya muda mrefu na kwa kiasi kikubwa haikidhi makusudio ya Sheria yenye.

Mheshimiwa Spika, Katika kuliona hilo, Serikali imeandaa muswada huu wa Sheria wenye madhumuni ya kuweka mazingira bora ya matumizi ya wanyama, lakini kadhalika na kulinda haki za wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imepata nafasi ya kuupitia kwa kina muswada ulioko mbele yetu, na hatimaye kuandaa na kupata nafasi ya kuwasilisha maoni yake, ambayo kimtazamo hayapingani na maudhui ya muswada wenye, ila ni kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya I ya muswada huu, Ibara ya 3, inayotoa tafsiri ya neno “*Director*”, Kambi ya Upinzani ingependa kutoa angalizo kwamba huyo Mkurugenzi mwenye dhamana ya Ustawi wa Wanyama awe ni mtumishi aliyebobea katika fani hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa kuzingatia ukweli kwamba mambo mengi huwa yanapwaya kiutendaji kutokana na wanaopewa majukumu kutokuwa na uelewa wa kutosha wa fani husika, jambo linalosababisha kuwepo kwa udanganyifu mkubwa, hali inayosababisha kugubikwa na utendaji mbovu. Matokeo yake ni manung’unico na kudumaa kwa sekta husika.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, tunaishauri Serikali kuweka bayana sifa anazihitajiwa kuwanazo Mkurugenzi atakayesimamia Ustawi wa Wanyama, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya II ya muswada, Ibara 6, ibara ndogo ya (2) inayosema, ninanukuu “*....in the event that the Minister proposes to dispose of that matter otherwise than in accordance with the advice of the Council....*” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Baraza limeundwa kisheria na kwa kuwekewa vigezo vyote vinavyo stahili na ambavyo vimeonyeshwa kwenye “*schedule, made under section 5(2)*” kwenye muswada huu, Kambi ya Upinzani haioni sababu yoyote ya msingi itayopelekea Waziri kupinga maamuzi ya Baraza hilo. Muswada huu unapaswa kuziba vichochoro vyote ambavyo vinaweza kusababisha suitafahamu katika maeneo ambayo Baraza litayatolea ushauri, Kwa maana nyengine ni vyema Waziri akaonyesha kuliamini kiutendaji Baraza lake.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7, ibara ndogo ya (3) inayosema kuwa, nanukuu “*....and member of Police Force above the level of Inspector by virtue of his office shall be deemed to be an animal welfare inspector to act generally for the purpose of this Act.*” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na Ibara ya 8, ibara ndogo (1)(a) inayosema, ninanukuu “*ensure that any animal that is carried by sea, road, railway, air or inland water is fit for the journey....*” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina wasi wasi ni kwa namna gani *Police Inspector* anaweza kuisimamia vyema sheria hii pasi na kuwa taaluma ya aina fulani inayohitajika. Ukaguzi wa wanyama ni taaluma maalum ambayo anapaswa mtu kujifunza kwayo ili kuweza kuitekeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9, ibara ndogo (4) inayoruhusu, ninanukuu “*....the court may order that the animal be sold and that the proceeds of the sale be applied to the payment of such costs.*” mwisho wa kunukuu. Kambi ya Upinzani inaona ibara hii ina kasoro ndogo, kwa sababu hukumu yake imejielekeza kwa wanyama wakubwa kama punda, farasi, ng’ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika. Sisi tunauliza, hali hii inakuwaje pale inapomhusisha mnyama kama paka na vinyama vyengine vidogo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunadhani kwamba, adhabu zaidi ingelitolewa kwa mmiliki wa mnyama huyo, ikiwa ni pamoja na faini au kifungo au vyote viwili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya III ya muswada huu, Ibara ya 11, ibara ndogo ya (3) inayosema na ninanukuu “*The Minister shall prescribe minimum standards for*

*appropriate housing systems, animal carriers.....”* mwisho wa kunukuu. Kambi ya Upinzani hapingani na dhana nzima ya kuweka vigezo vinavyostahili kwa ustawi na ubora wa mifugo yetu, Lakini tunaona ipo hoja ya msingi ambayo inapaswa kutiliwa maanani pale ambapo kuna baadhi ya wananchi wanaishi ndani ya nyumba moja na mifugo yao, ni dhahiri kwamba ufanuzi wa kina unahitajika katika kuweka hivyo vigezo ukizingatia aina ya mfugaji na viwango vyao (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18, ibara ndogo ya (1) na Ibara ya 36 inayosema kuandaa na kushiriki mashindano ya ugomvi wa wanyama (*animal fights*) ni marufuku, Kambi ya Upinzani inaona hapa haki haikutendeka hasa ukizingatia kwamba kuna mashindano ya jadi yanayohusu mapigano ya mafahari (*bull fighting*), mapigano ya majogoo (*cock fighting*) na kadhalika, Michezo hii pamoja na kwamba ni ya kufurahisha bali pia huwapatia kipato wafugaji wa wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, iweje leo hapa Tanzania michezo kadhaa ya kupiganisha wanadamu ikiwemo masumbwi, karate, karate masumbi (*kick boxing*), *wrestling* na kadhalika inapata umaarufu mkubwa. Michezo hii ina washiriki wengi na inapendwa sana kama ambavyo inapendwa michezo ya kupiganisha wanyama, Ni kwa nini basi tunatunga sheria ya kupiga marufuku michezo ya aina hiyo kwa wanyama, lakini upande wa pili tunaimarisha michezo hiyo hiyo kwa wanadamu, tunadhani ipo haja ibara hizi kufanyiwa marekebisho na kuandaa utaratibu na kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha michezo ya aina hiyo kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada ibara ya 34(1) nanukuu: “*There shall be reasonable limitation on the intensity and duration of the work to be performed by a working animal, including satisfactory periods of rest and relaxation.”*

Mheshimiwa Spika, ibara hii ni muhimu sana kuwepo, isipokuwa inahitaji kufafanuliwa zaidi kwenye kanuni zitakapotungwa kama kuweka muda wazi, muda wa juu (*maximum hours*) ya mnyama kufanyakazi na ni katika mazingira yepi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni muhimu sana kupitishwa na Bunge lako Tukufu hasa ikizingatiwa kwamba, kumekuwa na uvunwjaji mkubwa wa haki za wanyama hapa nchini. Wananchi wamekuwa wanafanya haya ama kwa makusudi au kwa kutokujua, lakini anayeathirika ni mnyama na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutunga sheria ni jambo moja, lakini utekelezwaji wa sheria yenye ni jambo la pili na lenye umuhimu mkubwa. Sisi Kambi ya Upinzani, pamoja na mambo mengine, tunashauri yafuatayo:-

Lazima jamii ielimishwe vya kutosha kuhusu umuhimu wa Muswada huu na kuwa tayari kusaidia utekelezaji wake. Kwa kuwa suala la ufugaji lipo zaidi vijijini ni vyema basi Halmashauri zikaandaa utaratibu wa utekelezaji wa sheria hii, ikiwemo kutunga *bylaws* haraka iwezekanavyo na kuzisimamia ipasavyo. Wakaguzi waandaliwe wa kutosha na *police inspectors* nao wapatiwe mafunzo ya kutosha ili utekelezaji wa

sheria hii uwe wa ufanisi mkubwa. Jamii inayokereketwa na jamii na haki za wanyama, ijiunge katika vyama vya hiari kusaidia kuielimisha jamii kutetea haki za wanyama na kusaidia utekelezaji wa sheria yenyewe. (*Makofi*)

Serikali nayo kwa upande wake, ivihamashe vikundi hivi vya kijamii na kuvipa kila aina ya msaada ili viweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Nasi Waheshimiwa Wabunge, tukiwa wadau muhimu wa sheria hii, tuhakikishe tunasimamia vyema haki za wanyama kwa manufaa ya wanyama wenyewe, kwa ajili yetu sisi na vizazi vijavyo. (*Makofi*)

Mwisho, ningependa kuishauri Serikali kwamba, itamke bayana katika Muswada huu kwamba, Muswada huu utatumika Tanzania Bara tu na siyo Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwadini Jecha, kwa mchango wako huo. Waheshimiwa Wabunge, sijui tufanyeje maana yake wachangiaji kwa Muswada huu ni wawili; Mheshimiwa Job Ndugai ambaye ameomba achangie jioni, kwa sasa yupo mmoja naye hayupo ukumbini ambaye ni Mheshimiwa Suzan Lyimo. Kwa hiyo, wote wawili hawamo ukumbini.

Mheshimiwa Sanya, upo tayari? Basi kwa kuwa nimewatamka wale wengine pengine watakuwa njiani, nakuita Mheshimiwa Sanya. Ahsante kwa kutusaidia. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Spika, hii mpya leo. Mimi nilikuwa sikujiaanda hasa kwa kuwa Muswada huu kama ulivyoelezea mwanzo, ilikuwa usiletwe leo. Kama tulivyozungumza huko nyuma, kwenye Muswada wetu uliopita ule tulichelewa, lakini tumefika hapa ndiyo pa kuanzia.

Wanyama wana haki ya kuishi na wana haki ya kufanyiwa wema. Sisi Waislam katika dini yetu ya Kiislam, hata yule mnyama ambaye amedhalilishwa kwa ajili yetu, ukaruhusiwa umchinje utumie kitoweo chake na bidhaa zinazotokana na yule mnyama, basi kuna hukumu zake na sheria katika Dini ya Kiislam. Mimi nina hakika sana kwamba, vitabu vyote alivyovitayarisha Mwenyezi Mungu *Sub-hanahu Wataala*, hakuna hata kipengele kimoja au aya moja, inayomruhusu binadamu kumdhalilisha mnyama. Sisi tumeambiwa tumchinje tena kwa kisu kilichokuwa kikali. Umchinje mara moja aone raha ya kuchinjwa, kwa sababu unamchinja kwa vile umeruhusiwa na Mola wako kumchinja na kumtumia. Umchinje katika mazingira ambayo yanaruhusiwa kwamba, mazingira haya ndiyo anayotakiwa mnyama achinjiwe. Tena usimchinje kwa kumdhalilisha wala su kumfanyia istizai kama vile yeye hana haki ya kuishi. Kwa kuwa umeweka mbuzi, kondoo, ng'ombe au kuku, unaanza kumnadi kabla ya siku ambayo unataka kumchinja. Zote ni haki ambazo zimo hata ndani ya vitabu vya dini.

Leo Tanzania tuna sheria ambayo imepitwa na wakati, lakini wakoloni walikuwa wakiisimamia vizuri kuwawaka maofisa mbalimbali kufuutilia namna gani hati za

mnyama zinatendeka. Tumshukuru Mola kwamba, Serikali imeamka na fikra hizi za kuleta Muswada huu ili turekebishe hii sheria. Kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, Halmashauri na Muswada huu hasa huu ambao unamhusu mpaka mtu wa chini kabisa, anayewatia kuku katika tenga bila ya hesabu uwafikie na wajue sheria ikoje na wanaweza wakahukumiwa vipi, wakati gani ili kuku wale na mbuzi wanaosafirishwa au ng'ombe, wapate haki za msingi ambazo leo tunazipitisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara nyingi wasafirishaji wa wanyama hawa, mbali ya wafugaji wanapowaweka, lakini wanaosafirisha huwa wanasaferisha kwa njia ambazo haziridhishi kusafirisha. Mifugo hii mara nyingine husafirishwa hata nyakati za usiku. Je, tutahakikisha kwamba, wakati wa usiku au alfajiri wanapoingia sokoni au wanapoingia katika mji unaokusudiwa kusafirishwa, watakuwepo hao *inspectors* ambao wataangalia katika matenga hayo idadi ya kuku waliokuwemo?

Katika gari hilo ng'ombe waliochukuliwa, wamechukuliwa kwa masafa gani, walipumzishwa wapi na hapo walipopumzishwa kuna *certificate* gani ya kukuonyesha wewe kwamba, huyu ametoka Mbeya anakwenda Dar es Salaam, lakini kituo fulani amepumzishwa amepewa maji, kama kuna malisho kidogo amepewa ili aweze kumsaidia mnyama yule.

Ukienda mbali zaidi, hii nchi ina watu makatili sana kwa wanyama na siyo Tanzania tu; nchi nyingi duniani zinakuwa na watu ambao *mentality* zao zinawafanya waone kwamba, wanyama hawana hisia, hawana haki ya kuishi wala hawana haki ya kutendewa wema.

Mheshimiwa Spika, mimi ningetua mfanu mmoja mdogo sana, ambao ulinihuzunisha sana; katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania kuna hawa wanaojifanya eti waganga wa kienyeji, wengi wao wanakuwa ni wanafiki na ndiyo hao wanaoleta matatizo mengi hata ya kutaka viungo vya binadamu kuweza kufanya mambo yao ya ushirikina.

Alikuwepo bwana mmoja, alimchuka paka akamkata kichwa halafu akachukua sehemu ya mwili uliobaki akautia mdomoni akafyonza damu na akapigwa picha akaoneshwa kwenye vyombo vya habari mbalimbali hapa nchini. Eti kwa sababu ya uganga wake na ushirikina wake, ikaonekana kwamba ni furaha na tija kwa watazamaji, lakini iangaliwe kwamba kuna watu katika nchi hii na duniani humu wanaopenda paka, wanaopenda kuweka mbwa, wengine wanaweka kasuku, wengine wanaweka wanyama wengine tu. Wanawafuga wanaelewa wenyewe.

Kwa hiyo, haki ya mnyama ipo pale pale na inasemekana hata hivi karibuni katika kampeni za uchaguzi uliopita huko Tarime, kulikuwa na mjinga mmoja alichukua Bendera ya CCM akamvalisha mbwa. Huu ni ujingga na yeoyote aliyefanya ni mjinga tu. Huwezi ukamdhililisha mnyama kwa sababu ya kuinua hadhi ya chama chako au kwa sababu ya uchaguzi halafu akatokea mjinga mwingine mkubwa zaidi, ambaye inasemekana alikwenda kumuua yule mbwa; ana kosa gani yule mnyama? Wewe ndiyo

uliyechukua nembo ya chama ukamvalisha mnyama ambaye hajui kinachoendelea, halafu akatokea mjinga mwingine aliyezidi ujinga akaenda akamua yule mbwa; *what is this? No sense!*

Alikuwa atafutwe aliyemvalisha bendera ahukumiwe yeye na siyo mbwa. Unakwenda kumhukumu mnyama ambaye hana akili hayawani, anayetaka busara zako na hekima zako na hivi ndivyo tunavyowafanyia wanyama wengine. Unakuwa na mbuzi wako wewe mwenyewe unamdhilish; kwa nini umdhilishe wakati anakupa maziwa, anakupa kitoweo na anakupa tija katika maisha yako?

Kwa hiyo, mimi naunga mkono sana hii hoja ya kuweka mazingira mazuri ya kuwatunza wanyama wetu wote.

Twende mbali zaidi, hata biashara ndogo ndogo za wanyama wa mapambo au ndege wa mapambo, zipigwe marufuku nchini. Angalieni katika *data* za usafirishaji wa ndege wa mapambo kupelekwa Ulaya wanafika asilimia 50 na asilimia 50 hawafiki wanakufa kutokana na baridi iliyokuwemo ndani ya ndege. Wale tabia yao wanataka baridi fulani na joto fulani katika miili yao, ambapo wewe unafanya kwamba ni tija unapata *foreign currency*, lakini unamdhulumu mnyama na ndege ambaye unamsafirisha. Hivyo, raha ya macho yako na pambu la macho ukamdhilish ndege, mimi naona hata tungefika mbali zaidi, tukafuga ndege katika matundu tukaweka nyumbani tunawadhili tu. Unampa chakula lakini humpi uhai wake hasa wa asilia, unamfanya hawezu kupanua mbawa kuruka kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Ndege dume na jike hawawezi kukaa pamoja, unamuweka nyumbani unamuwashia taa kucha habainishi baina ya usiku na mchana. *Yes*, huyo ni *creature ameumbwa*, kuna Mungu ameumba wanyama wanaishi usiku na kuna wanyama wanaoishi mchana. Huwezi ukamchukua komba (*bush bird*), ukamuweka mchana mahali penye taa ukafikiri ndiyo unampenda au ndiyo anafanya michezo wakati siyo wakati wa kukaa ni wakati wake wa kupumzika, wakati wake wa kutoka, usiku ukifika bila ya kumwambia anatoka kama alivyo popo.

Kwa hiyo, mimi nasema huu Muswada umekuja wakati muafaka lakini je, sheria hii itatafsiriwa kwa Kiswahili kwanza? Tunajifanya Waingereza sana, kila kitu kwa Kingereza; watu wa chini Kiswahili ndiyo lugha yetu. Umfikie na Waraka wa Kiswahili, aweze kufahamu kuku nimbebe vipi, ng'ombe nimlee namna gani, nikimbebesha mzigo, mzigo uwe na uzito wa kiasi gani. Tuangalie punda kama walivyo Mexico katika historia yao na South America; mizigo yetu mizito tunabeba kwenye punda; punda tunawapa haki gani? Anabebesha matofali mangapi na miti mingapi?

Unambebesha punda paketi za sementi ngapi halafu na wewe unakaa juu yake, unachukua na bakora unamdunda; *what is this?* Anakutumikia, anakupa riziki yako, lakini wewe huonyeshi mapenzi yake.

Katika historia sisi tunatoka katika jimbo moja kule India linaliitwa Catchstate, lipo katika jimbo la Gujarat; wakati wa sherehe zozote zinazofanyika katika Gimbo la

Gujarat wale wenye punda ambao wanawasaidia kimaisha kupata riziki, hukoshwa na wengine wakawekwa mapambo. Ndivyo ulivyo ukweli wenyewe, wanawatia mpaka hina. Kwa mapenzi yao kwamba huyu ndio gari langu, huyu ndiye anayenipatia riziki, leo sisi tutampiga punda mpaka kwenye sehemu yake ya mgongo au sehemu yake ya tako, panakuwa na alama ya kuonyesha kwamba huyu punda au ng'ombe yupo katika madhira.

Mwaka jana, sikukuu kama hii ya mfungo tatu, nyumbani kulikuwa na matatizo ya nyama, ikabidi nimpigie simu daktari akaniambia nipo kwa Mzungu mmoja namtibia punda wake, mimi nikastaajabu sana nikamsubiri afike nimuulize ilikuwaje! Nikamuuliza huyu Mzungu aliyekuwepo hapa kama ni *expatriate* anaafuga punda? Akaniambia hapana, kamwona punda kapigwa mpaka kavunjwa mguu akamuokota anam-*treat* kwa gharama zake, kwa mapenzi yake na kumhurumia mnyama. Je, wewe binadamu unayepata riziki kutoka kwa mnyama yule?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote, hili suala tulikemee na lisiwepo. Tujue gari sasa inachukua mifugo mingapi, tengla kuku la size gani, linachukua kuku wangapi, tunawasafirisha vipi, wanaosafirisha vibali vyao viwe halali. Palikuwa na kisa kimoja hapa, waliondoka watu wakasafirisha ng'ombe kupeleka Comoro, matokeo yake Comoro kukatokea matatizo ya kutokuelewana ng'ombe wale hawakuteremshwa; nusu ya ng'ombe wale walikufa ndani ya meli. Waliporejeshwa kupelekwa Zanzibar, ng'ombe hao walipofika nusu yake nao walikufa kwa kukosa malisho ambayo yalikuwemo ya kuwafikisha Comoro na siyo tena ziada ya kuwarejesha Zanzibar.

Nani alihuksika na kadhia hii hatujui. Kwa hiyo, Serikali iwe makini kwamba, kila tunapotunga sheria, kila tunapoleta Muswada tuwe wafuatiliaji, tusiwe rahisi wa kupeleka makaratasi Bungeni tukayapitisha, tukayachangia halafu matokeo yake hatufuatilii. Tuliwahi kupitisha Muswada hapa wa Vidhibiti Mwendo mwaka 1995, bahati mbaya wakati ule hukuwa Spika wala hukuwa Mbunge, mimi nilikutangulia, tukatazame leo mabasi mangapi yana vidhibiti mwendo. Tukatazame Serikali imechukua hatua gani, ulikuwa ni mradi wa nani hatujui, kwa nini uliletwa? Ajali zimezidi, vidhibiti mwendo havipo; kwa nini tufanye hivi?

Tunapotunga sheria tuwe tayari kuifuatilia, tuwe tayari kuwaweka wafuatiliaji wa kweli na wajue nini maana ya sheria, ndiyo kama alivyosema Mheshimiwa Mwadini Jecha kwamba; je, hawa watakoopelekewa kesi hizi, wana ufahamu, wana elimu ya haki za huyu mnyama kama unaipeleka polisi au unaipeleka kwa Diwani au unaipeleka Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu, lakini twende mbele zaidi kwamba, utafsiriwe kwa Kiswahili, uteremshwe mpaka chini tufuatilie haki za wanyama, tujue punda anabeba matofali mangapi, anabeba sementi paketi ngapi; yes, ana *capacity* ya kuvuta lile gari, tazama uzito wa gari alilokuwa nalo, uzito wa sementi inayowekwa ndani, matofali au miti na wewe unakaa juu na badala yake unachukua na bakola yenye miba unamchapa punda yule, unategemea atakuzalishia, wewe unapata riziki kutokana na mgongo wa punda.

Umheshimu ng'ombe anakupa maziwa, ngozi, nyama na fedha za kuweza kuwalipia wanao karo za *school* na mambo mengine. Ng'ombe umheshimu kwa sababu ni sehemu ya mapato yako, unapomsafirisha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, mpe haki zake zote; mpe haki ya maji, majani na mpe haki ya kusafiri salama kama unavyosafiri wewe. Tusiwapakie ng'ombe tukawatia ndani ya mabehewa ya treni, tukawatia ndani ya mabehewa ya magari kwa kuwatesa katika barabara nzima kutoka mji mmoja kwenda mji mwingine. Ahsante sana. (*Makofsi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanya, kwa hotuba yako nzuri, ingawa ulisema hujajiandaa lakini mtu yejote ambaye amekusikiliza kwa makini kama mimi nilivyofanya, unaonesha moyoni unapenda wanyama. Umezungumza kwa hisia nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimemwona Mheshimiwa Suzan Lyimo amekwishaingia, nitampa nafasi yeye, atafutiwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Charles Keenja ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika Muswada huu wa Ustawi wa Wanyama.

Mheshimiwa Spika, labda nianze tu kwa kusema kwamba, kwa kweli sisi binadamu tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia utashi ambao tumekuwa tofauti na viumbe vingine. Vilevile ametupa uwezo wa kuweza kutawala viumbe vingine. Kumekuwa na matatizo mbalimbali, hasa jinsi gani binadamu tunaweza kutawala viumbe hivyo hususan wanyama.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, wanyama wafugwao hasa wale wanaotoa maziwa, ngozi, pamoja na mbolea, wamekuwa wakisaidia sana uchumi hasa kwa chakula. Wengi wamekuwa wanatumia mifugo hiyo kuweza kuwalipia watoto wao karo na mambo mengine ya kifamilia, lakini ni jinsi gani basi binadamu wameweza kuwakatili wanyama hao?

Mheshimiwa Spika, sote tunakubaliana kwamba, kwa kweli wanyama kwa muda mrefu wamekuwa wakikatiliwa sana na wale wanaowafuga. Wapo wanyama wa aina mbalimbali; kuna wale wanaotoa mazao hayo niliyoyataja, lakini kuna wale ambao wapo kwa ajili ya usalama kama vile mbwa, paka, ngedere na wengine wanafuga nyani kwa ajili ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini nikianzia na punda; punda ni mnyama ambaye amekuwa akisaidia sana hasa wakulima na wafugaji katika kubeba mizigo. Tumeona jinsi ambavyo punda hao wamekuwa wakibebeshwa mizigo, lakini pamoja na kubebeshwa mizigo hiyo, bado pia punda wale wamekuwa wakichapwa sana. Vilevile wamekuwa wakinyimwa haki yao ya msingi ya chakula au maji na ndiyo maana inafika mahali, punda wanakataa hata kwenda. Binadamu haoni kwamba, mnyama yule

amechoka au anahitaji labda maji au chakula, matokeo yake tumekuwa tukiwachapa bila sababu. Kwa hiyo, tunaona ni jinsi gani tumekuwa tukiwakatili wanyama.

Mnyama mwingine ambaye nilitaka kumzungumzia kwa kina ni mbwa; mbwa tumeona ni jinsi gani anatumika hasa katika suala zima la usalama. Polisi wamekuwa wakitumia mbwa, lakini vilevile binadamu ndani ya majumba yetu tumekuwa tukitumia sana mbwa kwa ajili ya usalama. Kwa kuwa hakuna sheria yoyote, imekuwa wafugaji wa mbwa hao hawana uwezo wa kuwapatia chakula, matokeo yake wanawaacha wale mbwa wanazagaa. Kibaya zaidi, mbwa wale wanaweza kuwa wamepata ule ugonjwa ambao tunauita kichaa cha mbwa. Kwa hiyo, unakuta ni tishio kweli katika jamii inayozunguka. Nadhani sheria hii imekuwa wakati muafaka ili wale wanaofuga mbwa waelewe kwamba, mbwa ni lazima afugwe ndani, lakini basi kama ni kwa sababu za kiusalama zaidi, labda usiku wa manane ndiyo waweze kufunguliwa ili kuweza kukimbiza wezi.

Vilevile ihakikishwe kwamba, yule mfugaji anampatia mnyama yule haki zake hasa chakula, lakini vilevile napouguwa aweze kumpeleka kwa *veterinary*. Imekuwa ni kawaida kwamba, kutokana na labda kutokuwa na sheria, wenye mbwa hata mbwa wale wanapouguwa, basi wanaachwa wanakufa na hakuna chochote kinachoendelea. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna haja kabisa ya hii sheria kuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini japo sikuwepo na sijui kama Mheshimiwa Sanya amezungumzia, kuna suala limejitokeza hivi karibuni, tulipokuwa kwenye kampeni kule Tarime, vyombo vya habari vingi vilionyesha uwepo wa mbwa ambaye alikuwa amevishwa vazi ya chama kimoja na baadaye tunaambiwa kwamba aliuawa.

Sasa sielewi sheria inasema vipi, kwa sababu mimi nijuavyo; hata kichaa kama amefanya kosa au ameua basi kichaa yule huwa anaachiwa; sasa mbwa hana akili na mimi naamini mbwa yule hakuva ile *t-shirt* peke yake ila alivalishwa. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea kama kuna sheria inayosema mnyama haruhuswi kuvishwa nguo, basi iwe wazi. Vilevile kama inasema hivyo, basi tatizo liwe ni la yule aliyemvisha na sio mbwa mwenyewe au mfugo mwenyewe.

Nadhani hii haipo kwa sababu tumesafiri sana nchi nyingi au tumesoma nchi za nje na tumegundua kwamba, kwa wenzetu nchi zilizoendelea, mbwa huwa wanavishwa hata viatu, wanavishwa mikufu, lakini sasa nilikuwa naomba tupate ufanuzi; kama ni kweli yule mbwa aliuawa tupate maelezo ya kina ni sababu zipi zilizofanya mbwa yule akauawa? Inaleta hasira kwa sababu ni *t-shirt* ya chama au sheria inasema nini, tulikuwa tunaomba tupate ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme pia kwamba, sasa hivi tuna tatizo kubwa sana, pamoja na kwamba, sheria hii inakuja lakini kuna tatizo kwamba hatuna barabara za kupitishia wanyama na sehemu nyingine zimekuwa wafugaji wakipitisha wanyama barabarani wanakamatwa. Vilevile tuangalie na ranchi; sasa hivi hatuna ranchi, sasa ukienda pale Vingunguti ukaona jinsi wanyama wanavyochinjwa, eneo ni chafu hakuna maji na bado tunaishi. Sasa hii sheria nilikuwa naomba kujua ni kwa kiasi gani

imeona suala hili la ranchi, lakini vilevile uwepo wa barabara za mifugo, kwa sababu hapa linakuja suala zima kwa nini wanyama wanasafirishwa kwenye mabehewa, kwa nini wanyama wanasafirishwa kwenye magari kwa wingi sana na sasa hivi imetokea kwamba hata kwenye haya mafuso au *pick-up* zeny chuma juu unakuta mbuzi wameufungwa kwenye chuma halafu watu wapo chini. Kwa hiyo, kwa kweli unaona huu ni ukatili mkubwa sana kwa wanyama. Sasa nilikuwa naomba kuuliza; Wizara ni kwa kiasi gani wamejiandaa kuwa na barabara nzuri za kuitishia wanyama lakini vilevile kuwa na ranchi ambazo zitasaidia sana wafugaji kuweza kupeleka mifugo yao huko lakini vilevile maji kwa sababu tunajua kuna suala zima la maji na uchinjaji unahitaji maji mengi. Sasa sijui ni kwa kiasi gani hii sheria imezingatia yale matatizo ambayo sasa hivi tunayo?

Mheshimiwa Spika, lakini suala la hawa wanyama wa kufuga hasa mbwa kwa kweli niseme tu kwamba, wenzetu sasa hivi hata jana nimesoma, kule Ujerumani wameanzisha hata migahawa kwa ajili ya kupeleka wanyama kwenda kula kwenye migahawa. Sasa hii sheria inapokuja Tanzania, tumejiandaa kiasi gani kwa sababu kwanza hata *veterinarian* wa wanyama hawa ni wachache, dawa ni chache lakini vilevile vyakula ukienda kwenye *markets* nyingi nchi zilizoendelea unakuta kuna *special place* ambayo ni kwa ajili ya vyakula vya wanyama wafugwao.

Sasa sijui hapa Tanzania kama tuna uwezo huo na Serikali itajitahidi kiasi gani? Kuna watu sasa hivi wamekuwa na uwezo, wale wa kundi la chini wamekuwa kundi la kati na kuna matajiri ambao wana mifugo yao wanayofuga ndani na inahitaji sana vyakula. Kwa kiasi gani Wizara au Muswada huu umezingatia vyakula hivyo, dawa na suala zima la salon kwa ajili ya wanyama hao.

Nchi zilizoendelea wanafanya hivyo, wanawapeleka *salon* wanaogeshwa, wanapakwa mafuta na kadhalika. Sasa je, hapa Tanzania watu tunaofuga hatupati hiyo *service*? Tulikuwa tunadhani Muswada huu pia ungeweza kusaidia ni jinsi gani wanawenza pia wakaandaa *salon* kwa ajili wanyama tunaowafuga. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia suala zima la wanyama hawa wafugwao kuzurura ovyo. Nimesema kuna hilo ambalo linaweza likasababisha watu kuanza kuogopa, kwa sababu kuna watu *naturally* wanaogopa mbwa, hasa watoto na watu wazima pia. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hii sheria itasaidia sana, lakini vilevile wenzetu nchi za nje wamekuwa na kawaida sheria inasema lazima mnyama unayemfuga awe amesajiliwa. Sasa sijui ni kwa kiasi gani hapa Tanzania tunaweza kufanya hivyo na labda sensa kwa ajili ya wanyama hawa kama pia inaweza ikafanyika ili mnyama anapofanya kosa labda amemng'ata mtu, basi ijulikane ni mnyama gani na ni wa mtu gani ili yule mtu aweze kulipa fidia au jinsi yoyote ambavyo adhabu itakavyotolewa.

Vilevile kutokana na suala la mazingira, wenzetu nchi zilizoendelea wanapotembea na mbwa wao barabarani, lazima wahakikishe kwamba, wana mifuko ya nailoni ili mbwa anapochafua mahali fulani anabeba. Lakini huku Tanzania na nchi nyingi za Afrika hilo halipo. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ifike mahali pia hayo yawemo

ili watu wajue pia suala la mazingira. Usafi wa mazingira ni suala la msingi sana katika kutekeleza suala zima la Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ambalo nilitaka kulizungumzia ni suala zima la vyakula. Suala la vyakula kwa wanyama tunaofuga, hasa wenzetu wafugaji wa mifugo kama ng'ombe na mbuzi, wakati wa ukame wamepata tatizo kubwa. Nadhani hukuwepo lakini umesikia kwamba, hapo Kilosa tu, juzi wakulima wameuwawa kutokana na masuala mazima ya sehemu ya kulishia mifugo. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hili suala Mheshimiwa Waziri, pamoja na Waziri wa Kilimo, mliangalie kwa sababu limeleta matatizo makubwa sana hasa migongano kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na nadhani haya yatazingatiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Kuna tangazo kwamba, Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, hivi sasa kikao chao kinaendelea wanahitaji waongezekere. Nadhani ni wachache sana na wanazingatia Miswada miwili; *Public Health Bill* na *Mental Health Bill*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, mnahitajika katika Ukumbi na 133 ili kuzingatia Miswada hii miwili iweze kuiva.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi nitoe mchango wangu katika Muswada huu wa Ustawi wa Wanyama.

Mheshimiwa Spika, labda nianze kama alivyoanza mwenzangu, Mheshimiwa Sanya kwamba, hawa wanyama wameletwa kwa ajili ya matumizi yetu sisi binadamu na wana faida kubwa na kwa maana hiyo kuwatunza vizuri ni halali yao. Muswada huu umetambua mambo mengi kuhusu wanyama, pamoja na kwamba, wanyama hawa wanatupatia vitoweo na hili ni jambo la busara kwa wanyama hawa. Nina wasiwasi na Muswada huu; je, umefafanua na umekwenda kwa undani zaidi kuhusu hawa wanyama kwa sababu ustawi wa wanyama au kuwatendea visivyo wanyama ni pamoja na kuchinja?

Mheshimiwa Sanya, umefafanua na umekwenda kwa undani zaidi kuhusu hawa wanyama. Ustawi wa wanyama au kuwatendea visivyo ni pamoja na kuchinja na kama Mheshimiwa Sanya alivyosema, kwa upande wa Waislamu tumepewa namna ya kuchinja.

Mheshimiwa Spika, wapo ambao labda wanachinja visivyo na ndio maana hata kidunia kuna matangazo ya nyama *halal*, wengine wabena tu. Sasa Muswada huu nina wasiwasi kama umeeleza kiundani kwamba, uchinjaji wa kubena hautakiwi. Vilevile nina wasiwasi kama umekwenda kiundani kwamba, wapo wanyama ambao ni halali yetu kula na wengine hawaliwi. Tunajua kwamba, kuna makabila na dini mbalimbali, lakini kwa ujumla kama ulivyoletwa huu Muswada; je, umefafanua kwa kesi ya Tanzania?

Wapo watu ambao hawali baadhi ya wanyama na kuna wengine wanakula. Kwa wenzetu Wachina, hatuoni tabu tunasikia wanakula nyoka, lakini je, Muswada huu umekwenda kwa undani au Mheshimiwa Waziri, utakapokuja hapa utatufafanulia? Wapo wenzetu ambao panya kwao ni kitoweo, wengine wanaharibu, lakini kuna sehemu nyingine panya ni wengi, wakikamatwa wakatengenezwa halafu wakapewa wenzetu labda itafaa. Muswada umefafanua nini kuhusu suala hilo? Inafaa utueleze.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuhusiana na utesaji wa wanyama ambapo Muswada huu ndio unapoondosha au unataka kulindwa kwa wanyama. Kuhusu usafirishaji, tunajua kwamba, binadamu anaposafiri kwa mfano kutoka hapa Dar es Salaam kuja Dodoma tu, tunaona mabasi yanasmama kwa chakula watu wanapewa nafasi ya chakula na wengine wanunua maji. Sijaona usafirishaji wa wanyama ambao unatendeka hivi sasa Tanzania ni wa mateso na kama ni wa mateso; je, Muswada huu utafafanua nini kuhusu usafirishaji wa wanyama mbali na kuwarundika katika behewa moja au lori kwa wingi? Je, huduma ndogo ndogo za majani, malisho, maji ya kunywa watazipata vipi? Je, Muswada umesema nini kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, ibara ya nane imezungumzia kwamba nanukuu: “ensure that any animal that is carried by sea, road, railway, air or inland water is fit for the journey.” Umesema hivyo, sasa je, leo Waziri katika kanuni ataweka kanuni gani kuhusu uwezekano wa hawa wanyama? Vilevile tukumbuke kwamba, hawa ni wanyama, wakati unamsafirisha na inasema yuko *fit* kwa mambo hayo, hawezi kupata maji ya kunywa, utawezaje sasa kumsafirisha kwenye lori na uweke tanki la maji kwenye lori na wanyama wengine wapo nyuma na gari lipo kwenye *movement* na huyu atoke nyuma aende mbele, itakuwaje hali hiyo?

Jamani Mheshimiwa Waziri, kwanza, inafaa elimu na utafiti wa kina ufanyike. Haya mambo kuyataja tu kwenye Muswada huu kwamba yatendeke ni rahisi, lakini utekelezaji wake una matatizo ya aina yake.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeshuhudia kwamba, mnyama ambaye anateswa na mnyama huyu ni halali kwa kula, basi hata ladha ya nyama yake inabadilika. Tumeshuhudia na sisi kwa upande wa Zanzibar, wapo ng’ombe wengi sana ambao tunawachukua kutoka bara. Ng’ombe wa Zanzibar ladha yao ni tofauti na ambao wanapata *variety* ya majani mbalimbali wanaotoka Bara au ng’ombe wa kulekule Zanzibar ambaye anatoka sehemu ambayo hakuna majani, wanaolishwa makaratasu tu basi ladha yao ni tofauti.

Kwa maana hiyo, katika kusafirisha hawa wanyama, Mheshimiwa Waziri, alingalie suala hili na kanuni barabara zitengenezwe, wanyama hawa wapate haki zao. Wanyama hawa wanaugua maradhi mbalimbali na ni kweli kwamba, Wizara inayohusika inajitahidi katika matibabu. Je, ni zahanati ngapi vijijini zipo kwa ajili ya wanyama? Sehemu za mijni tu ndio utakuta hizi zahanati za kutibu vinyama. Kwahiyo, kwa Muswada huu pia ni sehemu ya ustawishaji wa wanyama, ipo haja ya Wizara husika sasa kusambaza zahanati nyingi sana za kutibu wanyama, pamoja na madaktari husika.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aliuliza hawa *police inspectors* watakuwa na elimu gani kuelewa mnyama huyu yupo katika dhiki, anadhalilishwa au la? Tunajua polisi wanapewa mafunzo mazuri na wanawenza wakaongea na mbwa; je, polisi wanawenza wakaongea na ng'ombe na mbuzi? Kwa maana kwamba, hapa Kambi ya Upinzani inasisitiza kwamba, elimu ya hawa wanyama ni muhimu; ni muhimu kujua kwamba, huyu mnyama sasa hivi akilia mlion huu anahitaji kitu gani, akifanya hivi anahitaji kitu gani, kwa maana kwamba sio kuleta Muswadsa tu, lakini kwanza tuangalie na vitu muhimu hasa kwa wale wanyama maarufu, ambao tunawasafirisha mara kwa mara wakiwemo ng'ombe, kondoo na mbuzi, inafaa basi na lugha yao tuifahamu na tujue hali yao na katika barabara tunazowasafirishia, viwemo vituo tofauti vyatanya hawa kwenda kwenye tiba.

Mheshimiwa Spika, nige sehemu ya michezo. Bahati nzuri Muswada huu utatumika hapa Tanzania Bara tu na katika sehemu ya michezo kule Pemba sisi tuna michezo wetu wa ng'ombe. Historia ya michezo wa ng'ombe kwa hapa Afrika ni Pemba tu na kwa dunia labda ni Spain na Portuguese, wanao michezo huu wa ng'ombe. Sasa Muswada huu ukizuwia kitu kama hicho kwa sababu kuna kuzuwia michezo ya kupiganisha kuku, kupiganisha ng'ombe, lakini kuna huu michezo wa ng'ombe na binadamu. Sisi kwetu ni sehemu ya mila na utamaduni na hii ni Jamhuri ya Muungano, yapo mambo ambayo yalianzia visiwani lakini kwa sababu ya Muungano yameenea Tanzania Bara. Mfano, taarab tu hivi sasa inapendwa zaidi Tanzania Bara kuliko hata huko visiwani, lakini sana sana ilianzia kule. Sasa na huu michezo wa ng'ombe, ambao ni utamaduni wa sisi Wapemba, inafaa uthaminiwe na uenziwe na tutakapousambaza ukaja mpaka huku Tanzania Bara isiwe kikwazo.

Kwa hiyo, sheria hii kwa hili iangalie sehemu hiyo, wanyama ni sehemu ya michezo na waruhusiwe na iwe hakuna tatizo la michezo huu wa ng'ombe. Tunajua kwamba panya wanafanyishwa michezo, wanatumiwa katika tafiti tena muhimu sana mpaka za kutegua mabomu. Tunajua kwamba, mbwa wanatumiwa katika michezo na ni hodari tu na wanatumiwa katika kazi nyingine ambazo ni muhimu. Farasi wanatumiwa katika michezo, sasa na ile kupiganisha kuku kwanza inakuwa ni kuku wa kabilia, nao ni michezo. Muswada huu usichukulie ni kitu kibaya.

Mheshimiwa Spika, wapo watu ni fahari na isitoshe watu wote wanaopiganisha kuku basi wana matunzo mazuri kuhusu kuku wale kuliko kuku wa aina nyingine yoyote. Anapewa chakula vizuri, anaogeshwa, anatibiwa, yaani anatunzwa, kwa hiyo, kitu hiki sio haramu.

Kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kupiganisha watu inahalalishwa iwe kupiganisha kuku iharamishwe, basi ingeharamishwa kwanza kupiganisha watu; watu kupigana mangumi. Kwa hiyo, Muswada huu usizuwie suala la kupiganisha kuku.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitaunga mkono hoja ikiwa vipengele vile vyatanya kupiganisha kuku, vyatanya kutunza vizuri wanyama na vyatanya kutokuzuiliwa michezo

ya ng'ombe na kusambazwa huku Tanzania Bara, ikiwa kama hivyo havitawekewa vikwazo. Kwa maana hiyo ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Ilikuwa niseme tu Mheshimiwa Mnyaa kwamba, tunapopiganishwa binadamu huwa kuna kanuni zake, lakini kuku hawapewi kanuni zozote na hupigana mpaka kuuwana pengine.

Tunaendelea, Mheshimiwa Charles Keenja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika Muswada huu. Nianze kwa kukiri kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na kwa hiyo tulishapata nafasi ya kuuchambua. Napenda tu niongeze haya machache niliyokuwanayo.

Mheshimiwa Spika, yaliyomo katika Muswada huu siyo mapya kama alivyotueleza Mheshimiwa Waziri. Zilikuwepo sheria zilizotungwa tangu ukoloni na wale tuliopita shule miaka mingi kidogo iliyopita, tulikuwa na vyama vyaya kujifunza kutunza wanyama na tuna chama mpaka leo cha *TSPCA*, ijapokuwa naona ofisi tu sioni vitendo. Kwa hiyo, yaliyomo si mapya. Kilicho kipyta tu ni labda pengine tulisahau haya mambo ambayo yalikuwa yamewekwa kisheria, tukaacha kuweka utaratibu wa kutunza wanyama, labda wakati mwingine tukajenga tabia ya kuwatesa tu bila sababu. Kwa maoni yangu ni kwamba, baadhi ya vitendo hivi vinatokana ama na kutokujua; mtu hajui kwamba akimpiga mnyama na yeYe anaumwa kama mwadamu anavyoumwa.

Akimtesa bila kumpa chakula anateseka na kadhalika. Hapa Dodoma ukipita barabarani mpaka hata kituo kikuu cha polisi, utakuta watu wamebeba kuku wamewaning'iniza. Wanawafunga kuku wanane, watano, kwenye mkono mmoja wananing'inizwa. Mara nyingi sana utakuta wananing'inizwa kwenye baiskeli, sijui kama wale wanaowasafirisha kuku ni watu wanaojua kwamba vitendo hivyo wanavyofanya ni vitendo vyaya mateso kwa wanyama wale. Nafikiri wakati mwingine ni kutokujua.

Mheshimiwa Spika, wengine ni kutokujali, anajua kwamba yule mnyama anateseka lakini hajali kumtesa. Haya ni mambo ambayo itabidi baada ya Muswada huu kuwa sheria, kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba yanakomesha, kwa sababu tunatesa wanyama bila sababu. Wanyama wengi ni hawa ambaa tumeamua wenyewe kuwafuga, hatukulazimishwa na mtu.

Mheshimiwa Spika, wengi sana wanaofuga wanyama katika nchi hii hawawatendei haki, utakuta mtu amefuga mbwa hana utaratibu kabisa wa kumlisha. Huyu mbwa anatakiwa azunguke ajitafutie chakula. Utakuta mtu amefuga kuku wale wanaoitwa *free range*, hahakikishi kwamba hao kuku wanapata chakula cha kutosha ili nao waweze kuishi na kufanya lile ambalo mfugaji alikuwa anataka wafanye. Mimi nataka niseme kwamba, mtu ambaye hawezi kumtunza mnyama, asimfuge. Mtu ambaye hawezi kutunza kuku, mbwa, ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine asiwafuge, kwa sababu kuwafuga ni kuwatesa.

Mara nydingi sana hawana manufaa kwake, ni mateso zaidi kuliko manufaa. Kila mtu anayefuga mnyama ni lazima ahakikishe kwamba, anamlisha kiasi cha kutosha, anampatia makazi yanayofaa na sio kuwarundika tu wengi mahali pamoja. Awe anawatibu wanapougu. Ninapenda niseme kwamba, matibabu ya baadhi ya hawa wanyama wakati mwingine ni ghali sana. Ng'ombe wangu aliwahi kuugua, alinigharimu shilingi 350,000, yaani zaidi ya bei yake. Kwa hiyo, ukiamua kumfuga, akiugua ni lazima umtunze, kama hutaki kufanya haya basi huyo mnyama usimfuge. Ninapenda niseme hapa kwamba, mnyama ukimtunza vizuri, ukamlisha vizuri, ukampatia malazi mazuri, huyo mnyama anapendeza.

Mheshimiwa Spika, ukikuta mbwa aliyetunzwa vizuri anapendeza, ukikuta ng'ombe aliyetunzwa vizuri anapendeza, lakini ukikuta wameachwa bila matunzo yanayofaa, hawapendezi hata kidogo. Nami napenda niseme, mtu asiyeweza kumtunza mnyama asimfuge na wakaguzi watakaoajiriwa chini ya sheria hii wahakikishe kwamba, wanyama wote ambao hawatunzwi vizuri wanakuwa *impounded* na baadaye wanakuwa *disposed of*, kama itakavyoonekana inafaa. Niseme pia kwamba, wengi wanaofuga wanyama hawa ni kutokana na manufaa yao, unamfuga ng'ombe ili akupe maziwa, kuku akupe mayai, sasa ukimtunza vizuri huyu kuku atakupa mayai mengi zaidi, ukimtunza vizuri huyu ng'ombe atakupa maziwa mengi zaidi na usipomtunza haya hautayapata.

Juzi tulikuwa tunapitisha Muswada mwingine wa ngozi hapa na tuliona kuwa, kutokumtunza mnyama vizuri kunaharibu hata ile ngozi na pesa ambazo ungeweza kupata kutokana na mauzo ya ile ngozi hazitapatikana. Kwa hiyo, tunaomba kila mtu atakayeamua kutunza mnyama amtunze na hii tabia ya kuwapiga wanyama bila sababu, unakuta mtoto anapita anaokota jiwe anampiga mbwa ambaye hana sababu naye. Kuuwa wanyama bila kuwa na sababu ya kuwauwa, wakati mwingine tunapita na magari barabarani unakuta mnyama anavuka badala ya kupunguza mwendo apite unamkanyaga bila sababu. Hizi ni tabia mbaya sana, ambazo ni lazima tuachane nazo na Muswada huu utatusaidia kusimamia.

Mheshimiwa Spika, hili la michezo mtusaidie kulifafanua kidogo, lakini tunapoamua kupigana ngumi tunaamua wenyewe. Unakwenda kwenye ulingo unavaa *gloves* zako unakwenda kupigana na mwenzako na unalipwa. Tunapomchukua mnyama kwenda kumpiganisha na mnyama mwingine, hakuna ridhaa yake wala hakuna utaratibu wa kuhakikisha ya kwamba, anakuwa salama. Mimi nafikiri michezo ambayo tunaisema si mizuri ni ile michezo ambayo inasababisha mnyama kuumia au kuumizwa na mnyama mwingine au kuumizwa na mwadamu. Kama mchezo wenyewe hauna madhara kwa huyo mnyama, hata mimi sina matatizo nao na tuendelee na michezo hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni usafirishaji wa mifugo na kuna kipindi ng'ombe wamesafiri kutoka Mbeya mpaka Lindi wakitembea, ni mateso makali sana kwa wanyama hawa. Pia kuwarundika ng'ombe wengi au mifugo mingi kwenye gari ili kuwasafirisha kuwapeleka katika soko. Tunaomba hili suala la kusafirisha mifugo vilevile liangaliwe na kuwepo utaratibu utakaohakikisha kwamba, wanapata matunzo njiani.

Zamani tulikuwa na njia za kuitisha mifugo na hizi ziliwu na sehemu za malisho, sehemu za maji na sehemu za kuhakikisha kwamba mifugo inapumzika. Siku hizi nafikiri njia hizo hazipo. Utaratibu wa kusafirisha mifugo, unaweza ukaswaga tu ng'ombe kutoka Shinyanga mpaka Dar es Salaam, wanatembea. Kwa hiyo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba, hawa wasimamizi na wakaguzi chini ya sheria hii, wahakikishe kwamba, mifugo haitezwi kwa makusudi wakati wa kusafirishwa na wahakikishe kwamba, wanaweka masharti yatakayotuwezesha kusafirisha mifugo hii mpaka kwenye soko kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo machache na ninaomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SUSAN LYIMO:** Mheshimiwa Spika, wanyama wafugwao ni muhimu sana mara nyingine, kwa usalama wa binadamu na mali. Wanyama hawa ni kama mbwa, paka, punda, nyani, ngedere na kadhalika. Kwa kuwa wanyama hawa wamekuwa sehemu ya wanaowafuga ni haki yao kupendwa na kutunzwa. Ustawi wa wananyama hawa ni msingi, lakini kumekuwa na baadhi ya wamiliki wa mifugo hii huitesa kwa kutowapa chakula, kuwapiga na kuwafanyisha kazi ngumu.

Mfano wale wafugao punda, wamekuwa wakiwabebesha mizigo mizito na pale wanapochoka huwa wanachapwa sana.

Mbwa wamekuwa wakiishi na watu kwa muda mrefu na wamekuwa wakisaidia sana katika kuashiria wezi au jambo lolote la hatari linapotokea. Kwa wenzetu wa Ulaya na Marekani, mbwa wamekuwa hata wakifanya kazi za uokoaji. Mfano kuna mbwa aliweza kuokoa maisha ya bosi wake aliyeanguka kwa *stroke*, lakini mbwa yule akaenda kwa jirani kuwaita na kumuwashisha hospitali. Hapa nchini tumeona ni jinsi gani mbwa wa polisi wanavyofanya kazi ya kugundua silaha, dawa za kulevyaa na kadhalika.

Pamoja na kazi kubwa zifanywazo na mbwa hawa bado wamekuwa hawapati chakula bora. hata pale wanapougua hawapati huduma yoyote ya dawa vile vile wamekuwa wakifanyiwa ukatili wa hali ya juu mfano mzuri ni mbwa aliyeishwa fulana ya chama kimoja katika uchaguzi mdogo wa Tarime. Najiuliza hivi mbwa aliweza kuva mwenyewe? Sheria ipi inayokataza mnyama kuvishwa nguo? Hata kama ni kosa; je, mwenye kosa ni aliyeveaa au aliyeishwa?

Sote tunajua, Mwenyezi Mungu, alitupendelea binadamu kwa kutupa utashi na ndicho kinachotutofautisha na wanyama, wadudu na vyote vilivyomo duniani. Hivyo ni vyema tutumie uwezo huu tuliopewa na Mwenyezi Mungu wa kutawala viumbwe wengine wote duniani, kwa haki na busara. Vinginevyo, tunapotumia vibaya ndipo tunapopata matatizo kama ukame kwa kukata miti.

Lazima basi tuwatendee haki wanyama hawa kama ambavyo wanatulinda na kutufanya kazi. Huko Ulaya na nchi zilizoendelea, wanyama wamekuwa wakihudumiwa zaidi ya binadamu; mfano wa maduka yao ya vyakula, salon kwa ajili ya kuogeshwa, zahanati zao wanapougua, lakini kubwa zaidi wana migahawa yao kwa ajili ya chakula. Wanyama hawa wamesajiliwa na hata wanapopata ajali (kugongwa), huwa mwenye kosa analipa. Hata wanapotembezwa barabarani na wakajisaidia (kuchafua), basi mwenye mnyama huwa anatembea na mifuko ya *nylon* maarufu kama rambo, kwa ajili ya kuzoa uchafu huo; ukiacha unapewa *ticket/fine*.

Hapa Tanzania pamoja na kwamba, hatuna sheria/taratibu za kuhudumia/kusimamia wanyama hawa, kumekuwa na ukatili mkubwa dhidi ya wanyama hawa. Hivyo, naamini sheria hii itawabana wafugaji kuelewa umuhimu wa kuwapenda na kuwajali wanyama hawa. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa wafugaji kufuga wanyama wengi bila uwezo na hivyo kuwaacha wanyama wakizagaa ovyo wakitafuta vyakula jalalani na wakati mwingi hutishia usalama wa wananchi ikiwa ni pamoja na kung'ata, hasa mbwa anapokumbwa na ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Hivyo, sheria hii ikazie wafugaji wa wanyama hawa hususan mbwa wafungiwe na wafunguliwe usiku tili kuondoa usumbufu usio wa lazima.

Serikali vilevile ihakikishe wanyama hawa wanajiliwa na pale wanapofanya makosa, basi wenyewe mbwa/wanyama hao wafungwe au waadhibiwe.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa orodha yangu ya wachangaiji imekamilika. Nimemwandikia Mheshimiwa Waziri, inaelekea hahitaji dakika 60, kwa sababu hata hoja zilizotolewa ni chache. Ili tuutumie muda wetu vizuri, ni vyema nimwite sasa mtoa hoja ili tusilazimike kusogeza mbele muda. Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nitajitahidi kutumia muda mfupi sana. Ningeomba tu niwatambue wale waliochangia katika hoja hii; wapo sita na aliyechangia kwa maandishi ni mmoja. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na Mheshimiwa Charles Keenja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Susan Lyimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoona, Muswada huu ambaa tumeuwasilisha Bungeni leo, una uhusiano sana na Muswada ambaa ulipitishwa siku ya Ijumaa unaohusiana na masuala ya biashara ya ngozi. Bahati nzuri, Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia katika Muswada ule ambaa ulipitishwa siku ya Ijumaa, walikuwa pia wanagusiagusia Muswada unaohusiana na ustawi wa wanyama.

Mheshimiwa Spika, kama utakavyoona, Muswada huu ni katika mlolongo na katika utekelezaji wa Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, ambayo lengo kubwa ni

kuhakikisha kwamba, tunajenga biashara ya kisasa katika masuala yanayohusu mifugo. Hii ni kwa sababu Tanzania tumekuwa na mifugo mingi, ambayo kila mara nimekuwa nikitaja idadi yake; ngo'ombe karibu milioni 19, mbuzi zaidi ya milioni 13.5, kondoo zaidi ya milioni 3.6, mbwa wale ninaambiwa ni zaidi ya milioni 4, ikiwemo nguruwe zaidi ya milioni 1.4, kuku zaidi ya milioni 53 na kadhalika, mbali ya sungura na vitu vingine vidogo vidogo.

Sasa ili pato hili la mifugo mingi tuliyonayo liweze kukua na kujenga uchumi wetu kikamilifu ni lazima tuwe na sheria ambazo zitaweza kutusaidia. Sheria hii inayohusiana na ustawi wa mifugo, *actually* tumekuwa na sheria ambayo imekuwa ikitumika tangu mwaka 1926 na nyingine ya mwaka 1930 na leo tupo mwaka 2008. Kwa hiyo, unaweza ukakuta hizi sheria kwa ujumla zimekuwa zikipitwa na wakati na ndio maana palikuwa na umuhimu sana wa kuwa na sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, lakini kama utakavyoona kwa ujumla tu, tumekuwa na sheria ambazo tumekuwa tukiziendesha katika nchi yetu. Tunafahamu kuna Sheria Namba 8 ya Mwaka 2004 inayohusu maziwa, tumekuwa na Sheria ya *Verterinary* Namba 16 ya Mwaka 2003, tumekuwa na Sheria Namba 17 ya Magonjwa ya Mifugo ya Mwaka 2003, tumekuwa na Sheria ya Nyama Namba 10 ya Mwaka 2006 pamoja na ile Sera ya Mwaka 2006. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuwa na sheria nyingine zinazoendana na masuala ya mifugo kama kweli tunataka kubadilika na kama kweli tunataka sekta ya mifugo, badala ya kuwa inachangia 4.7% ichangie kwa asilimia kubwa kama ambavyo nchi nyingine zimekuwa zikichangia.

Tanzania tuna mifugo mingi, lakini Botswana mifugo yake ambayo ni karibu milioni 2.5 inachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa kuliko sisi tulio na mifugo mingi. Ndio maana katika kuleta maendeleo ya kweli na mabadiliko ya kweli ni lazima tuje hapa Bungeni kwa ajili ya kubadilisha sheria.

Mheshimiwa Spika, nawashurkuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, ambaye amechangia kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ujumla ametoa maelezo mengi na kwa kifupi sana. Ameunga mkono hoja na akatoa maangalizo ambayo kwa bahati nzuri katika *schedule of amendment* tumeyaweka yote kwa ajili ya kuwa *considered* kwenye Bunge hili. Kwa hiyo, ninamshukuru tu na ninapenda kuthibitisha kwamba, ushauri wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ni mzuri na tunaukulabali. Tunaukulabali pia ushauri mkubwa uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao ni wadau na tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwadini Jecha, naye ameunga mkono karibu yote tu na hii ndio imekuwa kawaida yake. Kama nilivyosema siku ya Ijumaa kwamba, Mheshimiwa Jecha, kwa kweli ni mtekelezaji mzuri sana wa Sera za Chama cha Mapinduzi na hasa hizo ibara ambazo zipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005, kwa sababu kila Muswada tunapoleta ye ye anaunga mkono na anaunga mkono kwa niaba ya Upinzani. Huu ni mwelekeo mzuri, kwa sababu maendeleo nafikiri hayana chama, maendeleo sote tukishirikiana kwa kuungana hivi na hasa sera hizi nzuri na Miswada inayoletwala kwa

upande wa CCM na ikapokelewa vizuri kwa mikono 100 na wenzetu, haya ndiyo masuala tunayoyahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawashukuru sana Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono Muswada huu. Amezungumzia suala la kugombanisha ng'ombe na mifugo mingine, hili suala halikuzuiwa ila limewekewa utaratibu. Ukiangalia kwenye ibara za 33 mpaka 36, zimetoa ufanuzi sana na Mheshimiwa Spika, tuungane na wewe ulivyotoa ufanuzi mzuri. Kwenye ngumi binadamu wanapopigana kwanza wanapimwa uzito, huwezi ukachukua mtu mwenye kilo 100 ukampiganisha na mtu mwenye kilo 50, lakini hivyo hivyo kwenye ng'ombe basi usichukue ng'ombe mwenye kilo 400 ukampiganisha na ng'ombe, mbazi, kondoo au mbwa. Lazima tuangalie ni utaratibu gani unawekwa katika kuwapiganisha hawa.

Kwa hiyo, suala la michezo katika mifugo limewekwa bayana na hasa katika ibara ya 35, ukiisoma vizuri imeweka utaratibu. Hata katika masuala ya utafiti, vyote hivyo vimewekewa utaratibu. Kwa hiyo, lengo ni kuweka utaratibu badala ya kuwafanya wapigane halafu baadaye wanakuwa na majeruhi au anatobolewa ngozi yake na baadaye ngozi inakuwa haina thamani tunaiuza kama *raw material* nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitu kikubwa ni katika kulinda maslahi ya hawa wanyama, lakini suala la kupiganisha na nini halijakatazwa lakini ni lazima liendane sasa na sheria hii mpya ya kulinda maslahi ya wanyama wetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jecha, usiupinge Muswada huu. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Mnyaa, atu-*support* kwa sababu haya yote yamekuwa *included* kwenye Muswada. Pia Muswada huu utumike Tanzania Bara tu na sio Tanzania Visiwani; wachangiaji wengine wameeleza kwamba, wanununa ng'ombe kutoka Tanzania Bara, lakini mimi nafahamu Muswada huu kwa sababu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ni ya Tanzania Bara tu, *automatically* ni kwamba, Muswada huu unatumika huku ingawa tuna nyama nyangi na ng'ombe wengi sasa hivi wanawala upande wa Tanzania Visiwani. Niflikiri nao wawalinde wanyama kule, hata kama Muswada huu haupo, kwa sababu wasipowalinda maana yake itakuwa kuna Wajumbe wengi na Wabunge wengi kutoka Tanzania Visiwani, basi wakatumie hii elimu watakayokuwa wameipata kutohana na Muswada huu katika kuwaelimisha wenzao waliopo Tanzania Visiwani katika kuwalinda wanyama. Nafikiri hiki ni kitu kizuri kwa sababu sisi sote ni wamoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sanya, amezungumza karibu yote tu yaliyomo kwenye Muswada na amechangia vizuri yu. Nami nampongeza, ametoa mfano wa yule mbwa aliqvishwa vazi moja la chama fulani. Sasa mimi simfahamu aliqvishwa na sifahamu kama hiyo kesi ipo mahakamani, kwa hiyo, sitaki kuifafanua zaidi. Inawezekana Muswada huu utasaidia pia katika udhalilishaji wa namna hiyo. Inawezekana tungkuwa na Muswada huu ambao umepitishwa mapema, masuala ya kudhalilishwa kwa namna hiyo kama yaliyotokea Tarime, yasingweza kutokea kwa sababu sheria zingeanza kuchukua mkondo wake.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Sanya na wale wote wanaopenda ustawi wa wanyama, basi Muswada huu tuupitishe kwa pamoja ili tuweze kulinda haki ya ustawi wa wanyama wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mengine yote aliyoyazungumza tunakubaliana nayo na bahati nzuri mengi yatasaidia katika kuboresha tutakapokuwa tunatengeneza *regulations* za Muswada huu wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama. Serikali iwe makini katika kufuatalia baada ya kupitisha Muswada; nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Sanya, Serikali itaendelea kuwa makini katika kufuatalia baada ya kupitisha Muswada.

Tujue punda sasa atabeba kilo ngapi na kadhalika. Michango yote hii mliyoitoa na iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, tutajaribu kuiangalia ni namna gani tunaweza tukaiboresha katika *regulations*, kwa sababu bado tuna *option* ya kuongeza baadhi ya mambo mengine katika *regulations* zetu katika kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa Muswada huu unakuwa kamilifu.

Mheshimiwa Susan Lyimo, naye ameunga mkono hoja na amezungumzia punda anavyosaidia katika maendeleo ya wananchi. Mbwa pia amekuwa akiteswa. Ametoa mfano wa mbwa ambao wanapata kichaa cha mbwa saa nyingine; yote haya aliyoyazungumza yamo kwenye Muswada na alikuwa anazungumzia katika kuboresha Muswada huu na kuhakikisha kwamba mambo yote yanaenda vizuri.

Amezungumzia juu ya kuwa na hatua za kupitisha mifugo, kuna sheria nyingine ambayo tutaileta itakayozungumzia juu ya *stock routes*. Sasa hivi pia kuna barabara za mifugo ambazo zipo *identified* kabisa katika Wizara. Tutajitahidi kuhakikisha kwamba, tunaziimarisha ili wafugaji wasiwe wanapata shida katika kusafirisha. Katika Muswada uliopitishwa siku ya Ijumaa, tumezungumzia namna nzuri ya kusafirisha mifugo yetu kutoka mahali fulani hadi mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, haya yote kwa bahati nzuri naweza nikasema, yamehusika vizuri katika Muswada uliopita, Muswada huu ambao tunaupitisha na Miswada mingine itakayokuja katika kuhakikisha kwamba, tunazalisha vyta kutosha katika hali halisi ya maendeleo ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Mnyaa, naye kama nilivyozungumza, kwa ujumla amezungumza yale yale ya kuunga mkono na kuboresha, ambayo kama nilivyoeleza yote haya tutayazingatia katika kuhakikisha kwamba tunaboresha.

Mheshimiwa Charles Keenja, ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji, naye pia ameongeza chachu zaidi katika Muswada huu. Ninapenda niwahakikishie kwamba, yale yote yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge, tutayazingatia na yale mengine tutyaweka kwenye *regulations* katika kuhakikisha kwamba, tunaboresha sekta hii inayohusiana na mifugo.

Mheshimiwa Spika, sipendi nipoteze muda mwingi kwa sababu suala hili limeeleweka kwa Waheshimiwa Wabunge, nina uhakika halitachukua muda mwingi hata katika kulipitisha wakati tutakapoingia kwenye Kamati.

Baada ya kusema haya, nakushukuru na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu tumeshirikiana naye vizuri. Ninawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara, ambao wametoa changamoto kubwa na wameshiriki kikamilifu katika kuandaa Miswada hii na pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wadau wote waliohusika katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maendleo ya Mifugo na Uvuvi. Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono kwa mujibu wa kanuni ya 56(2) na kwa hiyo, itatubidi sasa tuingie katika hatua inayofuata.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### **Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya Mwaka 2008** *(The Animal Welfare Bill, 2008)*

Ibara ya 1  
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4  
Ibara ya 5  
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7  
Ibara ya 8

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 9

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 10

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 11  
Ibara ya 12  
Ibara ya 13

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 14

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 15

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 16  
Ibara ya 17  
bara ya 18

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 19  
Ibara ya 20  
Ibara ya 21

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23

Ibara ya 24

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29

Ibara ya 30

Ibara ya 31

Ibara ya 32

Ibara ya 33

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35  
Ibara ya 36  
Ibara ya 37  
Ibara ya 38  
Ibara ya 39  
Ibara ya 40

(*Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 41

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 42  
Ibara ya 43  
Ibara ya 44

(*Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 45

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 46

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 47

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 48  
Ibara ya 49  
Ibara ya 50  
Ibara ya 51  
Ibara ya 52

(*Ibara zlizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 53

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 54

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 55

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 56

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 57

Ibara ya 58

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 59

Ibara ya 60

Ibara ya 61

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 62

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 63

Ibara ya 64

Ibara ya 65

(*Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mbadliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama wa Mwaka 2008**  
*(The Animal Welfare Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Act, 2008*), ibara kwa ibara na kuubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo kadiri ulivyorekebishwa na Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa  
Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kitendo hicho cha Katibu wa Bunge kuusoma Muswada mara ya tatu, nafurahi sasa kuutangaza kwamba, Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama wa Mwaka 2008 sasa umepitishwa rasmi na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge kwa leo, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutakuwa na chaguzi za Wajumbe amba ni Wabunge wa kuingia katika Mabaraza ya Vyuo vyetu Vikuu. Sasa hili ilikwishatangazwa na Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbusha kwa sababu saa kumi kamili leo ndiyo mwisho wa kurejesha fomu na uchaguzi huu utafanyika Jumatano keshokutwa. Mpangilio ni kama ifuatavyo:-

Kwa Baraza la Chuo Kikuu Huria, wanatakiwa Wajumbe watatu, nadhani kwa mchanganyiko amba ni tunauelewa unaowakilisha hali halisi ya Bunge letu. Kwa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili, anatakiwa mmoja lakini awe mwanamke. Inajazwa na Mbunge mwanamke baada ya Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya kuteuliwa

kuingia katika Serikali. Kwa hiyo, nafasi hii ni ya mwanamke kwa sababu ndivyo tulivyokubaliana.

Kwa hiyo, nawaomba wale ambao bado wanafikiria au wameamua kutaka kugombea nafasi hizo nne; tatu za mchanganyiko wa Baraza la Chuo Kikuu Huria na moja ya mwanamke kwa Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili, mwisho wa kuchukua fomu kwa Katibu pale ofisini ni saa 10.00 leo jioni na uchaguzi tutaufanya, mtaona sasa kwenye matangazo yetu. Utapangwa kwenye *Order Paper* kwa ajili ya Jumatano.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, muda uliosalia hauturuhusu kuanza kumwita mto hoja inayofuata, ambaye atakuwa ni Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana. Saa 11.00 jioni atawasilisha Muswada wa *Workers Compensation Bill, 2008*. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi wakati.

(*Saa 06.40 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Kutoa Fidia ya Wafanyakazi  
wa Mwaka 2008**  
*(The Workers Compensation Bill, 2008)*

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Kazi, sijui kwa nini waliweka Wizara nyingine; Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, mto hoja wa Muswada huu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa maelezo katika Bunge kuhusu Muswada wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi wa tarehe tatu leo hii. Vilevile ninaomba kunikushukuru sana kwa jinsi ambavyo uliweza kunisaidia kupanga ratiba na kuweza kuuweka Mswada huu kwa tarehe ya leo, kuliko iliyokuwa imekusudiwa pale awali. Ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unawasilishwa Bungeni kwa mara ya pili; mara ya kwanza uliwasilishwa katika kikao cha Bunge cha mwezi Januari, 2008. Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa sheria mpya ya fidia kwa wafanyakazi (*The Workers Compensation Act, 2008*). Muswada huu umeandaliwa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya jamii kwa sasa, hususan wafanyakazi, kufuatia malalamiko yao ya muda mrefu kuhusu upungufu uliomo katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 inayotumika hivi sasa. Aidha, sheria inayopendekezwa katika Muswada huu, inakusudia

kutoa mwongozo, kanuni na muundo bora katika kushughulikia madai ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kuwa na mwongozo, kanuni, muundo na mfumo mpya ulio wazi, mwelesi kueleweka na unaotekelvezeka kwa urahisi katika kushughulikia madai ya fidia kwa wafanyakazi. Sheria ya Fidia, Sura ya 263, kwa muda mrefu imekuwa ikilalamikiwa na wadau kuwa imepitwa na wakati na ina upungufu mkubwa unaoleta kero kwa wadau na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya upungufu unaoalalamikiwa ni pamoja na ufuatao: Viwango vya fidia visivyowiana na madhara yanayotokana na ajali au magonjwa; Sheria kutokuweka kinga ya kutosha kwa wafanyakazi wanapoumia au kuathiriwa na magonjwa yatokanayo na kazi wanazozifanya wakati wa ajira; utaratibu mrefu na usiotekelvezeka kwa urahisi katika kudai na kulipwa fidia; kutozingatiwa kikamilifu kwa matakwa ya Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation*), kuhusu fidia kwa wafanyakazi; na kutokuwepo utaratibu wa kuwatunza wahanga wa ajali au magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, upungufu huo unadhoofisha jitihada za Serikali kuondokana na majanga makubwa Kitaifa hususan umaskini na hivyo kuathiri ustawi wa wafanyakazi na familia zao.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa, upungufu wa sheria hii umekuwa ukishughulikiwa kwa kuifanyia marekebisho ya mara kwa mara, Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263. Kwa mara ya mwisho, Sheria hii ilirekebishesha mwaka 1983. Hata hivyo, marekebisho hayo bado yanaonekana kutokidhi mahitaji ya wadau kwa sasa. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, yanayoendelea hivi sasa Duniani kote, imeonekana kuwa kuna haja ya kuiboresha sheria hii ili iweze kukidhi matarajio ya wadau na pia iweze kuendana na mfumo mpya wa Kimataifa wa ulipaji fidia kwa wafanyakazi wanaopatwa na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, mnamo mwezi Oktoba, 2001, Serikali kupitia Wizara hii, ilifikia uamuvi wa kuunda Kamati Maalum, kwa ajili ya kupendekeza sheria mpya za kazi zitakazokidhi mahitaji ya sasa. Sheria ya Fidia ni moja ya sheria za kazi zilizoangaliwa upya na Kamati hii na hatimaye mapendekezo yametolewa na kukubaliwa kuwa itungwe sheria mpya ya fidia.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kutunga sheria hii, wadau wote wa fidia walishirikishwa kikamilifu kupitia mikutano ya wadau na Kamati ya Ufundii (*Technical Committee*), iliyoandaa rasimu ya sheria. Wadau walioshirikishwa ni pamoja na Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA*), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimibili, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Wizara mbalimbali, waajiri na wafanyakazi binafsi na pia taasisi mbalimbali za bima, kimsingi wadau wote walikubaliana na pendekemo la kutungwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Muswada wa Sheria hii ni matokeo ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Maalum iliyowasilishwa na kukubaliwa na Serikali, baada ya kushauriwa na Baraza la Ushauri la Kazi, Uchumi na Jamii (*LESCO*). Katika Muswada wa Sheria hii inayopendekezwa, mambo muhimu yafuatayo yamezingatiwa:-

Kuanzisha Mfuko Maalum wa Kujitegemea wa Fidia (Autonomous Compensation Fund); kuweka utaratibu utakaohakikisha kuwa viwango vya fidia vitakavyotolewa vinawiana na madhara yatokanayo na ajali na kwamba, muathirika au wategemezi wake wanalipwa mafao ya kutosha, yanayolenga kuwawezesha kujitegemea; kuweka utaratibu mzuri na ulio wazi katika kulinda haki ya mfanyakazi kudai na hatimaye kulipwa fidia; kuunda bodi ya mfuko wa fidia yenye uwakilishi wa wafanyakazi wa Serikali; kuzingatia viwango vya kazi na mikataba ya Kimataifa kuhusu fidia; na kuhakikisha kuwa waajiri na wafanyakazi wote wanahusishwa na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, chini ya mfumo unaopendekezwa katika Muswada wa Sheria hii, kutakuwa na mfuko wa pamoja, ambapo wafanyakazi wanaoumia au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi, watalipwa fidia na mfuko huo bila kupitia kwa waajiri wao kama ilivyokuwa katika utaratibu wa sasa. Mfuko utakuwa na wajibu wa kugharimia matibabu na kurejesha uwezo wa kufanyakazi kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata magonjwa yatokanayo na kazi na kulipwa pensheni ya kujikimu katika kipindi ambacho mfanyakazi atakuwa hafanyi kazi. Kwa upande wa waajiri, kama ilivyokuwa katika utaratibu wa sasa, wao watawajibikia kisheria katika kutoa taarifa za ajali kwa mamlaka husika, pindi zinapotokea katika sehemu zao za kazi na pia kuchangia mfuko wa fidia. Utaratibu huu utamhakikishia mfanyakazi malipo ya fidia pindi anapoumia na pia utampunguzia mwajiri mzigo wa kuwahudumia wahanga wa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo unaopendekezwa ni mwepesi kueleweka, unatekelezeka kwa gharama nafuu, umezingatia hali halisi ya Taifa kiuchumi na kijamii na pia Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), kuhusu fidia kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo na utaratibu unaopendekezwa utakuwa na faida kwa waajiri kama ifuatavyo: Kwanza, faida kwa waajiri; utawapunguzia usumbufu na gharama zinazotokana na kushughulikia migogoro ya fidia; hawatalazimika kutumia fedha na muda mwingi kuuguza waathirika wa ajali au magonjwa yatokanayo na kazi, jukumu hilo litafanywa na Mfuko wa Fidia; ari ya wafanyakazi kutekeleza wajibu itaongezeka na hivyo kuongeza tija katika sehemu za kazi; mahusiano baina ya waajiri na wafanyakazi yataimarika; waajiri watashirikiana katika kuwafidia wafanyakazi wao pale wanapoumia au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi kupitia Mfuko wa Fidia.

Mheshimiwa Spika, pili, faida kwa wafanyakazi, watakuwa na uhakika kulipwa mafao yao ya fidia kwa muda muafaka pale wanapoumia au kuugua wakiwa kazini; wataweza kulipwa viwango bora vya fidia ikilinganisha na vya sasa; waathirika wa ajili

au magonjwa yatokanayo na kazi watapata huduma zinazotosheleza tofauti na hali ilivyo sasa; watawezeshwa kuishi maisha ya kujitegemea pale wanapopata ulemavu kutokana na ajali au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi; baadhi ya waathirika watajengwa ili waweze kushiriki tena katika shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tatu, faida kwa jamii, heshima na utu wa mfanyakazi utaongezeka; mzigo wa kuwahudumia waathirika wa ajili au magonjwa yatokanayo na kazi utapungua; idadi ya wahanga wa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi yatapungua kutokana na kuimarika kwa usalama katika sehemu za kazi; mchango wa wafanyakazi katika maendeleo ya uchumi wa Taifa utaongezeka; mfumo huu utachangia umaskini katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu 13; sehemu ya kwanza ya Muswada inapendekeza masharti ya awali kama vile jina la sheria, matumizi ya sheria, madhumuni yake na tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika sheria. Sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ya haki ya kulipwa fidia. Sehemu ya tatu inapendekeza taratibu za kudai fidia. Sehemu ya nne inapendekeza makadirio ya ulipaji fidia na kuweka masharti ya ukomo wa madai ya fidia. Sehemu ya tano inapendekeza utaratibu wa kupata mafao ya matibabu. Sehemu ya sita inapendekeza kuwepo na mafao ya kujenga upya majeruhi. Sehemu ya saba inapendekeza majukumu ya mwajiri katika masuala ya fidia. Sehemu ya nane ya Muswada huu inapendekeza uanzishwaji na utunzaji wa Mfuko wa Fidia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa inapendekeza kuwepo kwa Bodi ya Mfuko wa Fidia. Sehemu ya kumi inapendekeza shughuli za utawala na usimamiaji wa sheria. Sehemu ya kumi na moja inapendekeza masharti ya utekelezaji wa sheria. Sehemu ya kumi na mbili inapendekeza upatikanaji na utoaji wa taarifa za kutokea kwa ajali, kanuni zinazohusu sheria na adhabu, sehemu ya kumi na tatu ya Muswada inapendekeza mambo mengineyo mfano mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni, haki ya kupata taarifa na kufutwa kwa sheria ya fidia kwa wafanyakazi, Sura ya 263 ya Mwaka 1949.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Bunge lako Tukufu liyakubali mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria hii ya Fidia kwa Wafanyakazi ili Muswada wa Sheria hiyo uweze kuitishwa na kuwa Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako.

**MBUNGE FULANI:** Hajatoa hoja.

**SPIKA:** Amekwitao hoja.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi/Kicheko)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana, ulimalizia kutoa hoja kwa sauti ya upole sana, lakini Spika alisikia. Sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ili tuweze kusikia Maoni ya Kamati na anakuja Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Muswada wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*)

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Na. 86(5), Toleo la Mwaka 2007, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyochangwa Muswada wa Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*).

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nitumie nafasi hii ya pekee, nimpongeze Mheshimiwa Charles Mwera, Mbunge wa Tarime, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo. Kwa niaba ya Kamati, ninamtakia kila la kheri na mafanikio mema katika kazi zake. Naamini atawatumikia wananchi wa jimbo lake kwa uadilifu mkubwa. Namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake aliyokabidhiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukutarifu kuwa, Kamati yangu iliweza kuchambua mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*), kwa muda uliopangwa. Katika vikao hivyo, Wajumbe wa Kamati, pamoja na Wadau, walijadili Muswada huo kwa makini. Aidha, katika taarifa hii, Kamati itatoa maoni na mapendekezo ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa taarifa ya ushiriki wa wadau katika Mchakato wa Kuandaa na Kuchambua Muswada. Kamati inapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kuandaa mapendekezo ya Muswada huu, wadau mbalimbali walishirikishwa kikamilifu kuanzia hatua za mwanzo za mchakato wa kuandaa na kuchambua Muswada huu. Kamati inaipongeza kwa dhati, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa kuwashirikisha wadau wote muhimu katika mchakato wa kuandaa Muswada. Ninaomba niwatambue na kuwashukuru baadhi ya wadau kwa makundi yao kama ifuatavyo; Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA*), Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhibili, Waajiri na Wafanyakazi binafsi na Taasisi nyingine mbalimbali zikiwemo taasisi za bima.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea nia njema ya Serikali ya uanzishwaji wa Sheria hii mpya, kupitia Muswada uliopo mbele yako. Kama nilivyosema hapo awali, Kamati imeridhia uanzishwaji wa Sheria hii. Kamati ilijadili malengo na madhumuni ya Muswada na kimsingi, imekubaliana kabisa na maudhui yake, ambapo Muswada umelenga kupendekeza kutungwa Sheria ambayo itatoa mwongozo wa kuratibu na kusimamia fidia kwa wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini, kwa kupata majeraha au maradhi wakiwa katika utekelezaji wa majukumu ya ajira zao.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba, Sheria inayotumika hivi sasa (*The Workmens Compensation Act*), ilitungwa mwaka 1949 na tangu wakati huo mabadiliko mengi ya kijamii na kiuchumi yametokea na hivyo Sheria hiyo kupitwa sana na wakati. Kamati inaona kuwa, kuleta kwa Muswada huu ni ukombozi mkubwa kwa nia ya kulinda utendaji kazi na maisha ya wafanyakazi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, upungufu uliopo katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi iliyopo sasa na amba ni kero kubwa sana kwa wananchi na hasa wafanyakazi ni pamoja na viwango vya fidia vinavyotolewa kutolingana na hali halisi ya maisha; thamani ya fedha na utaratibu wa kupata fidia ni mrefu sana kiasi kwamba, hautekelezeki kirahisi; na kusababisha baadhi ya wafanyakazi walioumia kazini kukosa fidia walizostahili kutokana na utaratibu mbovu; na upungufu mwingine amba umejitokeza na unaoendelea kuwepo katika Sheria ya sasa ambapo ukweli ni kwamba, huu ni sawa na uvunjaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Sura ya 263 ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, imekuwa ikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara. Kwa mara ya mwisho, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 1982. Hata hivyo, marekebisho hayo bado hayaendani na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria hii mpya umezingatia Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani kuhusu utaratibu wa kisasa wa malipo ya fidia ya wafanyakazi. Hivyo basi, Sheria hii itatoa sura nzuri ya kukabiliana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, yanayoendelea hivi sasa katika ulmwengu huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuleta Muswada huu ili Sheria ikitungwa, iweze kukidhi matarajio ya wafanyakazi na wananchi kwa ujumla na pia kuendana na mfumo mpya wa kimataifa wa ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi, majeruhi wa ajali kazini au magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Sheria hii, kunapendekezwa kuundwa kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, ambao utasaidia jitihada za Serikali za kujenga uwezo mkubwa wa kukabiliana na majanga makubwa yanayolikumba Taifa letu mara kwa mara, hususan katika majanga yanayotokana na ajali zinatokea mara kwa mara sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, fedha zitakazotokana na Mfuko huu zitakuwa chachu katika kupiga vita umaskini, kwani ziada ya makusanyo itatumika katika kuwekeza katika

miradi ambayo italipatia Taifa fedha na kutoa ajira kwa wazawa na Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo yaliyojitokeza wakati wa uchambuzi wa Muswada: Kwanza, Tafsiri ya Mambo Mbalimbali; Sehemu ya kwanza ya Muswada inapendekeza masharti ya awali kama jina la Sheria, matumizi ya Sheria na misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa. Kabla ya kuingia kwa undani katika kuujadili Muswada huu, Kamati ilipenda kupata ufanuzi wa mambo na maneno hayo. Kwa mfano, kifungu cha nne kimetoa tafsiri ya maneno mbalimbali. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba, neno *Workers* ambalo ndilo limebeba jina la Muswada halikupatiwa tafsiri, badala yake neno *employees* ndilo limepatiwa tafsiri na kupewa uzito wake, lakini Muswada huu unaitwa *Workers Compensation*. Kamati inashauri Muswada huu utoe tafsiri ya neno *workers* ili kuondoa mkanganyiko uliopo baina ya matumizi ya maneno *employees* na *Workers*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Waziri na Wataalam, Kamati iliridhika na maelezo ya Serikali kwamba, Muswada huu unaweka mahusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa katika suala zima la kulipa fidia, ili kuleta uzito ni muhimu litumike neno wafanyakazi (*workers*) badala ya waajiriwa (*employees*), kwani Kimataifa neno *workers* ndilo linalotumika na kutambulika. Hivyo, si vyema nchi yetu kупingana na utaratibu uliokubalika Kimataifa na unaosimamiwa na Shirika la Wafanyakazi Duniani (*ILO*), ambalo Tanzania ni Mwanachama hai.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kilichozungumzwa ni matumizi ya neno ‘*may*’ na ‘*shall*’ katika Muswada huu. Kamati inasisitiza kwamba, kwa kuwa Muswada umelenga kulinda haki za mfanyakazi ambaye ataumia, kujueruhwa au kufariki Dunia akiwa kazini; kutumika kwa neno ‘*may*’ katika masuala muhimu kunapunguza uzito katika kutekeleza Sheria hii, kwani neno ‘*may*’ linatoa mwanya kwa mwajiri kutolazimika kutekeleza matakwa ya Sheria hii. Wajumbe walitoa mfano wa kifungu cha 94(1), kinachohusu Waziri kutunga kanuni, neno ‘*may*’ limetumika na maana yake Waziri anaweza kutunga kanuni kama atapenda. Kamati imesisitiza na kuona kwamba ni muhimu neno hilo libadilike na kuwa *shall* ili Mheshimiwa Waziri, asichelewe kutunga Kanuni ambazo zitaweza kusimamia na kudhibiti mwenendo mzima wa Mfuko katika kutekeleza sheria hii ya kuwalinda wafanyakazi waumiapo.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tafsiri ya maneno pia, Kamati ilibaini kwamba, neno *formal hearing* limetumika katika Muswada huu, lakini hakuna tafsiri yake. Wajumbe wa Kamati, walisema neno hilo limetumika sana katika kifungu 41 hadi 42, lakini hakuna tafsiri ya neno lenyewe, hivyo Kamati ilipendekeza kwamba neno *formal hearing* lazima lipewe tafsiri yake liweze kuelewaka vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, katika sehemu hiyo ya kwanza ya Muswada kifungu cha 3 (a) -(d) ni eneo ambalo lilikuwa na mjadala mkubwa juu ya kuhusisha wafanyakazi kutoka Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe na Wadau walipendekeza vyombo hivyo kutohusika na Sheria hii, kwani vinafuata Sheria zao za ulinzi na usalama, kwa mfano, Sheria ya Ulinzi na Usalama ya Mwaka 1966 na Sheria nyinginezo za vyombo nya ulinzi na usalama na vyombo nya mambo ya ndani. Sheria hizo zinawapa mamlaka, Mawaziri wenyewe dhamana kutunga taratibu za malipo ya fidia, ingawa mpaka sasa Sheria hizo zote zimepitwa na wakati na kufanya wakati mwingine malipo hayo ya fidia kufuata Sheria kuu ya zamani yawe hayalingani na wakati wa sasa. Baada ya Kamati yangu kuwasiliana na vyombo husika, Kamati ilikubaliana na ushauri wa kuviondoa vikosi hivyo katika Sheria hii, pamoja na Sheria tarajiwa ya Fidia kwa Wabunge watakapoumia au kuugua wakiwa kazini, zinazoweza kutumika na kutungwa baadaye, kwa mfano, sheria ambayo itawaingiza Wabunge katika suala zima la kulipwa fidia na kuugua wawapo kazini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa changamoto kuwa Sheria za vyombo hivyo na Sheria za Taasisi na mihimili ya serikali itakayotajwa, zinazohusu masuala ya fidia zinatakiwa kuoana na viwango vilivyowekwa na Sheria Mama ya Fidia ya Wafanyakazi ili wafanyakazi husika na makundi mengine, walipwe fidia kwa viwango visiviyopungua na viwango vilivyowekwa na Sheria hii mama.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Fidia ya Wafanyakazi. Kamati ilitafakari suala la uanzishwaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na kuunga mkono mapendekezo ya Serikali ya Sheria hii juu ya kuundwa kwa Mfuko wa Fidia, utakaotumika kulipa fidia bila kupitia kwa waajiri wao, kama ilivyo katika utaratibu wa sasa. Mfuko huu utakuwa na wajibu wa kugharimia gharama za matibabu na kurejesha uwezo wa kufanyakazi kwa wafanyakazi walioumia na kupoteza uwezo wa kufanya kazi. Aidha, Mfuko utaweka utaratibu ambao utamhakikishia mfanyakazi kupata fidia pindi atakapoumia. Mfuko utampunguzia mzigo mwajiri katika kuhudumia majeruhi wa ajali zinazotokea katika sehemu zao za kazi. Kimsingi, Kamati inaunga mkono asilimia mia moja, uanzishwaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6(1), kinahusu zaidi uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Wajumbe pamoja na wadau, walibaini kwamba, Mfuko huu ni muhimu sana kutokana na ukweli kwamba, unagusa maisha ya wafanyakazi ambao wamepata matatizo. Hivyo, ni vyema mamlaka ya utawala iweke utaratibu wa kumpata Mkurugenzi ambaye ni makini, mzoefu, mwenye ujuzi, nidhamu na mchapakazi; kinyume na hapo Mfuko huu utaweza kafilisika au kutowanufaisha walengwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, Kamati ilikubaliana na maelezo ya Serikali kwa kiasi fulani, lakini bado inaona kwamba si vizuri kuweka katika Sheria. Kanuni zitakazotungwa na Waziri, ziweke wazi kwamba, mchakato wa kumpata Mkurugenzi Mkuu unaweza kuanzia katika Bodi, kwa sababu Mfuko huu lazima uendeshwe na mtu mwenye uwezo mkubwa; ni Mfuko mzito wenyewe kujumuisha utatu, yaani mwajiri, mwajiriwa na Serikali, lazima uangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho cha 6(1), kinampa madaraka Mheshimiwa Rais, kuteua Jina la Mkurugenzi na pia Sheria hii inampa mamlaka Mheshimiwa Rais kumteua Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko. Kimsingi, Kamati haina tatizo kwa Mheshimiwa Rais kuteua Viongozi hao Wakuu wa Mfuko, lakini kwa sababu za kiutendaji, kiufanisi na mazingira ya sasa. Kamati inashauri kuwa, kama Mwenyekiti atateuliwa na Mheshimiwa Rais, basi mchakato wa kumpata Mkurugenzi uwe ni wa kushauriana ama kwa kupitia Waziri au kwa kupitia Bodi katika picha ya utatu kwa kadiri itakavyoona inawezekana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kuundwa kwa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Fidia, pamoja kuainisha madaraka na shughuli za Bodi hiyo. Katika kujadili aina ya Wajumbe wa Bodi ya Mfuko, Kamati iliipongeza Serikali kwa kuzingatia uwiano wa jinsia mionganoni mwa Wajumbe. Kwa mfano, katika Jedwali la Kwanza, kifungu cha 1(b)(vi) na (vii), imependekeza moja kwa moja kwamba, kati ya Wajumbe watatu watakaowakilisha waajiri; mmoja au zaidi wawe wanawake na Wajumbe wengine watatu watakaowakilisha Vyama Vya Wafanyakazi, mmoja au zaidi wanawenza kuwa wanawake. Katika vipengele vingine, kuna uwezekano kwa Wajumbe wengine pia kuwa wanawake.

Hata hivyo, Kamati ilisisitiza kwamba, kwa siku za baadaye, lazima Serikali ianze sasa kuangalia namna ya kufikia 50/50, kwani hiyo ndio mikakati ya Umoja wa Afrika na nchi za SADC. Sheria zetu lazima ziseme kwamba, Wajumbe wa Bodi wawe na uwiano wa 50/50. Aidha, Kamati ilipendekeza kuwa, kiongezwe kifungu kidogo katika sehemu ya Tatu ya Muswada, kitakachoelezea muundo wa Bodi ya Mfuko na sifa za Wajumbe wa Bodi na kwamba, Waziri mhusika apewe mwongozo kuhusu vigezo vya kutumia katika kuwateua Wajumbe wa Bodi ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba, katika Wajumbe wa Bodi kuna upungufu unaoonekana; mfano, kati ya Wajumbe wote 14 waliotajwa katika Muswada, hakuna Mjumbe hata mmoja aliyetajwa kwamba ataingia katika Bodi kwa ujuzi wake. Uzoefu unaonyesha kwamba, mara nyingine Wajumbe wa Bodi, hasa wanaoingia kwa mujibu wa madaraka yao au ujuzi, katika mikutano hiyo ya Bodi, hawatumii utaalam wao kutokana na kuwa na maslahi ya mwajiri wa Serikali.

Wajumbe kutoka maeneo huru, kwa mfano, Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine huru, huwa huru zaidi katika kutoa hoja na michango yao katika Bodi. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa; na Wajumbe kutoka vyombo huru nao wapewe kipaumbele katika kuingia katika Bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilijadiliwa kuhusiana na Wajumbe wa Bodi ni kufanya marekebisho kidogo katika Jedwali la Kwanza, kifungu cha 1(1)(b) na (ii), badala ya Kamishna wa Kazi kuwa Mjumbe wa Bodi, ni vyema iwe Kamishna wa Kazi au mwakilishi wake. Hii ni kwa sababu katika Idara ya Kazi, Kamishna anaweza kuwa mtaalam wa masuala ya kazi, lakini anaweza asiwe mtaalam wa masuala ya majanga na fidia; hivyo, lazima tutoe nafasi ya mtaalam wa majanga na fidia kuwa Mjumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, sehemu hiyo ya Tatu pia inatoa mamlaka kwa Bodi, kuanzisha vyombo vyenye lengo la kupunguza ajali sehemu za kazi kama vile Taasisi ya *OSHA*. Kamati inashauri kuwa ni vyema Mfuko ukatamka, utambue na ikiwezekana kuwekwa mikakati ya kuviiimarisha vyombo hivyo, kwa sababu ya umuhimu wake katika kupunguza ajali katika viwanda; hivyo, kusaidia Mfuko kutotumia fedha nyingi katika kulipa gharama za fidia. Kamati inaipongeza Serikali kuweka kifungu cha 17(1), kinachoipa nguvu Bodi kuanzisha vyombo kama hivi.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vitasaidia katika kuhakikisha sehemu za kazi ni salama kwa kila mfanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne mpaka kumi na tatu, Muswada unatoa mwongozo na taratibu za madai pamoja na shughuli za utawala na fedha. Sehemu hii ni muhimu sana katika Muswada wa Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008, kwani Mifuko mingi inayofanana na malengo kama haya, huwa inapata sana matatizo ya kiutawala na kiutekelezaji. Kamati inashauri kuwekwa kwa misingi imara ya miundombinu ya utawala ili wanachama au wale wafanyakazi wote watakaoumia wakiwa kazini, wapate amani na waone kwamba, wanaweza kufidiwa na kupewa malipo yao kulingana na wakati na bila kupata matatizo yoyote ili wasijutie kuijunga na Mfuko huu. Mbinu zinazopendekezwa ni pamoja na Mfuko kuwa na Mpango Mkakati utakaotumika katika kutekeleza majukumu ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne inapendekeza makadirio ya ulipaji wa fidia. Sehemu hii inapendekeza pia kuweka masharti ya ukomo wa madai ya fidia. Katika kulinda haki ya mfanyakazi kudai fidia, madai yatazingatia *no fault principle* ili kuwepo haki za ushindani kati ya waajiri na wafanyakazi. Kamati inashauri kubuniwa kwa utaratibu madhubuti, ambao utatoa jibu la haraka, litakalowezesha kubaini jinsi ajali ilivyotokea na mapendekezo ya malipo ya fidia kwa majeruhi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano inapendekeza utaratibu wa kupata mafao ya matibabu. Kamati inashauri ubuniwe utaratibu ambao utakuwa ni rahisi, utakaowezesha wanaostahili kupatiwa matibabu wanapata huduma zote za kitabibu bila kisingizio cha kukosa dawa au huduma muhimu nyinginezo. Aidha, utabibu ufanyike popote penye huduma hiyo na Mfuko ugharimie gharama za usafiri kwa mgonjwa na wasindikizaji, kulingana na hali itakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza viwango vya fidia. Viwango vilivyowekwa hivi sasa ni vidogo sana kwa kuwa vinatagemea sana asilimia ya mshahara wa Mfanyakazi. Viwango vya mishahara hapa nchini ni vidogo sana ukilinganisha na gharama za matibabu na hali halisi ya ujumla ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba na ya nane ya Muswada huu, inapendekeza majukumu ya mwajiri katika masuala ya kudai fidia, pamoja na utaratibu maalum utakaoumika katika kumpatia tiba sahihi majeruhi ili aweze kurudi kazini kufanya kazi.

Uzoefu unaonyesha kuwa, Waajiri wengi hususan katika sekta binafsi, wamekuwa wagumu katika kushirikiana na Mifuko ya Jamii. Hivyo basi, Kamati inashauri hatua madhubuti zitakazowezesha kupatikana kwa ushirikiano kutoka sekta binafsi. Hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya kutosha kwa waajiri wote na wananchi kwa ujumla, kuhusu sheria hii na inashauriwa viwango ambavyo Mwajiri na Mwajiriwa watatozwa ili kuchangia Mfuko, visiwe vyta juu sana ili vivutie wanachama wengi kujiunga na Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, kifungu cha 83(a) na (b), kinatoa ruhusa kwa Mfuko kuwekeza ziada katika vitega uchumi mbalimbali ili kudumisha Mfuko na kuongeza mapato. Kamati inashauri ziada ya Mfuko itumike katika kuwekeza katika maeneo hayo bila kuathiri mafao ya wanachama wa Mfuko huo. Ili kuvutia zaidi wanachama, ni vyema Mfuko utoe kipaumbele katika kutoa mikopo kwa wafanyakazi au ufanye miradi ya pamoja na wafanyakazi au waajiri ambao wana miradi inayoleta faida.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho ya Muswada huu inapendekeza mengineyo kama vile Mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni, haki ya kupata taarifa na kufutwa kwa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (*The Workmen Compensation*). Katika Suala hili la utungaji wa Kanuni, Kamati inashauri kwamba, neno ‘shall’ katika kanuni litasababisha Sheria baada ya kupitishwa na Bunge na kusainiwa na Mheshimiwa Rais, haitaweza kutumika mpaka kanuni zitungwe, wakati kuna maeneo mengi sana ya Sheria yanaweza kutekelezeka bila hata kutunga kanuni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Serikali, Kamati bado inasisitiza kwamba, kama kuna umuhimu wa kutunga kanuni, basi tuweke neno *shall* ili kuwawezesha Mawaziri waweze kutunga kanuni, kwani tunaweza kumpata Waziri wa namna ya pekee; anaweza asitunge kanuni hata baada ya kupita miaka mitano na hata zaidi na msiweze kumpeleka mahakamani kwa sababu Sheria inasema kwamba, anaweza kutunga kanuni au la kadiri atakavyoona yeye inafaa. Wakati umefika sasa, lazima Waziri awekewe katika Sheria, hata kama neno *may* litatumika, basi awekewe muda labda baada ya miaka miwili lazima kanuni ziwe zimetungwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilijadiliwa ni Miswada kuletwa kwa Lugha ya Kiingereza; Kamati inashauri serikali kuleta Miswada katika Lugha ya Kiswahili, kwa sababu Watanzania walio wengi kama si wote, wanazungumza Kiswahili. Wabunge wakati wa Kamati na hata Bungeni, wanajadili Miswada kwa Lugha ya Kiswahili na Mahakamani kesi zinaendeshwa kwa Lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, wakati umefika Kiswahili kiweze kutumika katika uandaaji wa Sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali endapo Muswada huu utapitishwa kuwa Sheria ni vyema basi Sheria iwe kwa Lugha ya Kiswahili ili wananchi walio wengi waweze kuilewa vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Kamati yangu inaliona bado linajirudia rudia ni tatizo la matumizi ya neno “he”. Limetumika mara kwa mara katika Sheria zinazoletwa Bungeni. Kamati inashauri Miswada kukwepa neno hilo, ikiwezekana

mabadiliko yafanyike ili neno “she” na “he” yatumike sambamba katika Sheria zetu ili kuleta usawa katika kijinsia.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kuna sheria mbalimbali zinatumika hivi sasa katika kuwapatia matibabu wafanyakazi wa Sekta ya Umma na Binafsi. Kwa mfano, wafanyakazi wengi wa Sekta ya Umma, wanapata mafao ya fidia kupitia Sheria Na. 8 ya Mwaka 1999 ya Mfuko wa Bima ya Afya. Kamati inaishauri Serikali kuleta mapema marekebisho ya sheria hizo ili zisilet mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria inayokusudiwa kutungwa.

Mheshimiwa Spika, viwango viliwyopangwa kwa ajili ya majeruhi aliyepoteza kiungo chake au uwezo wa kiungo cha majeruhi, havina uhalisia kabisa. Kwa mfano, majeruhi aliyepoteza kabisa uwezo wa kusikia, anapewa asilimia hamsini badala ya mia moja. Kamati inashauri jedwali hilo litazamwe upya ili marekebisho yaweze kufanyika kwa kuzingatia uhalisia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kumpongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga na Katibu Mkuu wake, Dr. S. Komba, kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati Kamati hii ikifikiria Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza wataalam wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha kazi hii. Napenda kuwashukuru sana na kwa dhati kabisa, wadau wote walioshiriki katika mchakato huu na Kamati iliyoandaa Muswada huu kwa ushiriki wao katika kazi ya kuuchambua Muswada. Kwa kiasi kikubwa, Kamati imetumia maoni na ushauri walioutoa katika vikao vyote.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa namna ya pekee, kumshukuru Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu, kwa kuendesha vikao vyta Kamati na kumisaidia kwa ufanisi mkubwa hasa katika kujadili Muswada huu. Ninamshukuru na ninamwomba Mwenyezi Mungu, ampe maisha marefu na ufanisi katika kazi zake za kila siku. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Lawrence Robert Makigi, Ndugu Brown Mwangoka na Ndugu Joshua Chamwela, kwa kuihudumia Kamati kwa umakini na ufanisi mkubwa, ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima, sasa naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, walioshiriki kuuchambua Muswada wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*) kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Othman Ally, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah,

Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Salum Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Dr. Gertrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Kaimu Katibu wa Bunge - DKt. Thomas Didimu Kashililah, kwa ushirikiano wenu mnaotupa katika kutekeleza shughuli za Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni na ushauri huo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, imechambua kwa kina Muswada huu na kwamba, imeona maslahi makubwa ya wafanyakazi na nchi kwa ujumla, yamezingatiwa kwa kiasi cha kutosha katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa niaba ya Kamati hii, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wachambue Muswada huu na hatimaye waupitishe kuwa Sheria ili maslahi ya wafanyakazi hao yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhangama, Mwenyeekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu rai ya Kamati kwamba, tuangalie upya meno “he”, sijui tutumie meno lipi, lakini ningependa kukumbusha tu kwamba, chini ya Sheria zetu; *the interpretation of Laws and General Clauses*, “he” inajumuisha “she”. Kwa hiyo, wanaharakati waoataka mabadiliko, wajielekeze kwenye Sheria hiyo, ndiyo inayotoa tafsiri na siyo kumpa kazi Waziri wa Kazi hapa, Sheria zote nchini zinafuata hii *interpretation of Laws and General Clauses* na kwa Kiingereza inasema *He embraces She*. Ahsante sana.

Tunaendelea na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, tupate mawazo ya Kambi ya Upinzani kwa Muswada huu.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, nikiwa mzima wa afya na kuweza kutoa mtazamo wa Kambi ya Upinzani katika hoja ilio mbele ya Bunge lako ya *Workers Compensation Act, 2008*, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kufikisha salamu za Wananchi wa Jimbo la Tumbe kwa Mheshimiwa Charles Mwera, kwa ushindi wake katika uchaguzi mdogo uliofanyika Wilayani Tarime. Sambamba na hilo, nawapongeza Wana-Tarime, pamoja na Watanzania wote, wanaopigania haki na demokrasia ya kweli katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, pamoja na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge hili na kulijengea heshima katika jamii yetu ya Kitanzania na nje ya Tanzania. Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Naibu wake, pamoja na timu nzima ya Watendaji wa Wizara hiyo, kwa kuleta Muswada huu wa fidia kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, natoa salamu za pole na kumtakia afya njema, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, aliyefanyiwa upasuaji mkubwa kule India. Mwenyezi Mungu, amrejeshee afya njema. Aidha nawapa pole wale wote waliopata misukosuko katika kipindi hiki. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kutoa baadhi ya mambo ambayo Kambi ya Upinzani inaona kama yatarekebishwa, Muswada huu utatekelezwa vizuri na asasi ambazo tayari zimekwishaanzishwa na wakati huo huo Serikali haitaingia gharama za uanzishwaji wa muundo na mfumo mpya wa kiutendaji kama Muswada unavyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo kuu la Serikali ni kutoa huduma bora kwa wananchi *at a minimum cost*; hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona utekelezaji wa Muswada huu ungeingizwa katika mfumo mzima wa hifadhi za jamii kwa kuundiwa Idara katika Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii, badala ya kuunda kitu kipyabisa.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa muundo na mfumo huu mpya kama Muswada unavyopendekeza, utahitaji miundombinu na rasilimali watu kubwa. Aidha, uundwaji wa bodi ni jambo ambalo badala ya Serikali kupunguza gharama za uendeshaji, inaongeza gharama hizo.

Kambi ya Upinzani inashauri Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ana Mamlaka ya kutunga Kanuni, pamoja na taratibu za uendeshaji, ingekuwa ni rahisi kutoa miongozo kwa Mifuko ya Hifadhi za Jamii jinsi zitakavyoanzisha Idara zitakazokuwa zinashughulikia fidia za wafanyakazi kutoka kwa waajiri ambaao ni wanachama wa Mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, hoja yetu ya hapo juu inapewa nguvu na madhumuni ya Muswada huu, ambayo ipo katika ukurasa wa 66 na ninaomba kunukuu: ““Madhumuni ya Muswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria, ambayo itatoa mwongozo kuratibu na kusimamia fidia, mahitaji ya mfumo mpya wa kisheria wa hifadhi ya jamii, ambaao utalenga mageuzi katika usimamizi na uratibu wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa upande wa Tanzania Bara.”

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2(2)(a), kinachohusu matumizi ya Muswada huu kinasema; Waajiri na Waajiriwa wote waliomo katika Utumishi wa Umma Serikali ya

Tanzania, lakini Tanzania Bara. Kambi ya Upinzani, inaona kifungu hiki hakijatilia maamani watumishi wa umma wanaofanya kazi katika Wizara ambazo ni za Muungano, lakini Ofisi zao zipo Tanzania Zanzibar kama vile Idara ya Uhamiaji, Watumishi wa Shirika la Posta, Watumishi wa Hali ya Hewa, Watumishi wa Baraza la Mitihani la Taifa, Mahakama ya Rufaa, Ofisi za Msajili wa Vyama vya Siasa na kadhalika. Ingekuwa ni vyema kama Muswada ungetamka kuwa matumizi ni kwa Waajiri na Waajiriwa wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bila kubagua wapo Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha nne, tafsiri ya neno *actually* imetolewa na kifungu cha 86(1) cha Muswada. Ukisoma kifungu hicho tajwa, hakielezi maana ya neno *actually*. Kambi ya Upinzani inaona mtindo huu wa kufanya *cross interpretation*, hautoi ufahamu uliokusudiwa kwa neno husika.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri ya maneno pia neno *employer* limetolewa tafsiri kuwa ni *any person who employs an employee*. Kambi ya Upinzani kwa kuzingatia tafsiri hiyo, inamtaka Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge hili ni kada ipi ya wafanyakazi ambayo haihusiki na Muswada huu; vinginevyo neno *any person* liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 46(1), 21(3), 96 na 97(2) vya Muswada huo, vinahusu adhabu. Vinapendekeza viwango vya juu vya adhabu kwa yejote atakayekuwa na hatia kwa mujibu wa Muswada huu wa Sheria. Naomba kunukuu: “*Not exceeding...*” kama ilivyojifafanua.

Kambi ya Upinzani inaona kwa kutoa kiwango cha juu cha adhabu, inampa mwanya yejote kupima lengo la kutenda kosa na adhabu atakayopata, yaani *cost benefit* na pia inamnyima Hakimu kutoa hukumu kwa kuangalia mazingira na madhara mengine yanayoweza kusababishwa na kutendeka kwa kosa. Tunashauri sheria itaje kiwango cha chini tu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 47(1)(b), kinachohusu ukomo wa fidia kuwa ni kwa yule mfanyakazi aliyerudia kufanya kazi ambayo alikuwa akiifanya kabla ya ajali kutokea au ugonjwa aliquopata kutoptana na mazingira ya kazi. Kambi ya Upinzani inataka ufanuzi; je, fidia ni pamoja na matibabu ya mgonjwa au ni pale mwathirika anaposhindwa kurudia katika hali yake ya kawaida au Muswada huu unamtoa mwajiri katika kugharimia matibabu ya mtumishi wake?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kifungu cha 81(c), kinachohusu matumizi ya Mfuko kuwa ni pamoja na gharama za uchunguzi wa kitabibu kwa mfanyakazi. Kwa maana nyingine ni kuwa, mwajiri anaondolewa jukumu lake la msingi la kuhakikisha na kutunza afya ya mfanyakazi wake. Hii inatokana na ukweli kwamba, baadhi ya magonjwa yaliyoordheshwa katika *occupational diseases* yanatibika na mtu anarudi katika hali yake ya kawaida. Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri, atoe ufanuzi kuhusiana na hili kwani waajiri wanaweza kutumia kifungu hiki kukwepa majukumu yao ya msingi na hivyo kuafilisi Mfuko kwa kugharimia matibabu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 62(3) cha Muswada huu kinasema kuwa; pale Mkurugenzi Mkuu atakapoamini kuwa matibabu zaidi yanaweza kusaidia kupunguza ulemavu kwa mfanyakazi anayeweza kulipia gharama zaidi za matibabu.

Kambi ya Upinzani, tunaona kuwa mwenye mamlaka ya mwisho Kisheria kuhusu kukoma au kuendelea kwa matibabu ni Daktari na hakuna kifungu kinachomhusisha Daktari katika kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu kadhia hii. Tunamtaka Waziri atueleze kama Mkurugenzi Mkuu ana uwezo wa kuchukua nafasi ya Daktari kwenye maamuzi yanayohusiana na athari ya mwathirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa mawazo hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofī*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa eneo hili. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, nimepokea wachangiaji saba, nitawataja ili wajiandae tu. Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary.

Sasa tutaanza na Mheshimiwa George B. Simbachawene, atafutiwa na Mheshimuwa Prof. Idris Mtulia, wakati huo huo Mheshimiwa Mwichoum A. Msomi ajiandae. Mheshimiwa Simbachawene karibu tafadhalii.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Kazi, kwa kuleta Muswada huu katika kipindi ambacho mabadiliko ya ajira yamekuwa ni mengi nchini na duniani, hasa kutokana na uwekezaji mbalimbali unaofanywa na wageni. Zamani mwajiri mkubwa alikuwa Serikali, lakini sasa hivi ni Sekta Binafsi ndiyo inatoa kwa kiasi kikubwa cha ajira. Kwa hiyo, tunapokuwa na sheria nzuri na iliyoandalialiwa kwa umakini kama hii, basi ni fahari na pengine ni ukombozi kwa waajiriwa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri ninaousemea wa Sheria hii, lakini nina mambo matatu ambayo ningependa na mimi nieleweshwe au nichangie katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Mifuko mingi hapa nchini ya jamii kama ilivyoanzishwa kwa madhumuni ya kuanzishwa kwake na kama ulivyo huu ambao tumeuanzisha sasa, kwa nia ya kufanya fidia kwa watu wanaoumia na kuugua maradhi yanayotokana na kazi malengo mahususi ya Mifuko hiyo ni kwa ajili ya kuwasaidia watumishi. Mifuko hii

inapoteza maana yake halisi, pale inapokwenda kwenye biashara zaidi hata kuacha jukumu lake la msingi la kuhudumia watu kama ambavyo tunaianzisha katika sheria zake. Hili ni tatizo.

Katika Kanuni za kawaida, *International Laws*; 15% inatumika kwa administration, 85% inakuwa ni kwa ajili ya kufanya fidia au msingi wa uanzishwaji wa Sheria hii. Wasiwasi wangu hapa ni je, hivi ni kwa kiasi gani sheria hii ina-fall kwenye ile Sheria tulioianzisha ya *Regulatory Authority* ya hii Mifuko mingine ya jamii au hii ipo tofauti? Ninapenda nipate ufanuzi, nimejaribu kusoma lakini sijapata *connection* kama inaitaja ile *Regulatory Authority* ambayo tulizungumza na tulitunga Sheria hiyo, nafikiri ni katika kipindi cha Bunge lilopita.

Sijaona kama Sheria hii nayo ina *fall* kwenye ile, lakini msingi wangu mkubwa hapa ilikuwa ni wasiwasi wangu juu ya Mifuko hii mingi ya jamii ambayo tunaianzisha, ambayo kwa kiasi kikubwa ina *over invest* na kufanya shughuli nyingine kuliko hata shughuli ya msingi ambayo imetungiwa Sheria.

Kwa mfano, ukichukulia hali ya kusuasua kwa *NIC* sasa, inatokana na *over investment*; wamejipeleka kwenye biashara zaidi na kuacha kazi ile ya kulipa *insurance* watu wanapokuwa wamepata ajali na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa na mimi nilichangie ni suala zima la wanaoathirika makazini, kutokana na magonjwa yanayotokana na kazi wanazozifanya. Zipo baadhi ya kazi kwa *nature* zake tayari 100% unajua hapa utakayefanya kazi hii ni lazima utaathirika kwa *nature* ya kazi hiyo. Lazima utapata matatizo ya kifua au kansa na kadhalika. Sasa kazi kama hizi, kwa kuwa kwa *nature* yake ni kwamba mtu anayeamsa kwenda kufanya kazi ile ni kama amejitosa kwenye kifo, lakini afanye nini kwa sababu inahitaji afanye kazi ili aweze kuishi. Mimi nilidhani kwamba, Sheria hii basi iwachukulie tofauti na *inge-treat* kazi za namna hiyo tofauti. Kilichoelezwa hapa ni aina ya magonjwa, lakini haikuelezwa aina ya kazi ambazo zenyewe kama zilivyo ni hatari kwa maisha ya binadamu. Ni vizuri sheria hii i-address hilo suala waziwazi.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya tu kwamba, kulingana na wajibu wa Kamati zetu nyingine, tunashindwa kushiriki katika *process* za Miswada hii, inapokuwa imeingia kwenye Kamati zetu za Bunge kwa sababu tuna Kamati nyingi na tuna majukumu ya Kamati nyingine pia. Nilidhani ni vizuri tujaribu kuona, kwa *nature* ya kazi unakuta ni lazima tu huyu mtu anayefanya kazi hiyo atapata madhara ya kiafya, basi iwe *addressed* na malipo yake yawe *exceptional* kwa sababu huyu mtu ni kama amejitoa mhanga.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulisema ni pale kwenye fidia, kwa mfano, kifungu cha 19(2), anazungumzia suala la fidia kwamba tatizo ambalo litampeleke mtu alipwe fidia ni lile tu ambalo litatokana na kazi anayoifanya na akiwa yupo katika utekelezaji wa jukumu lile la kazi ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu hapa sikuweza kupata tafsiri yake vizuri na ninaomba ninukuu: “*Where an accident is attributable to the serious or willful misconduct of the employee, no compensation shall be paid unless; (a) the accident results in permanent total disablement; or (b) the employee dies as a result of accident, leaving a dependant wholly financially dependent upon the employee.*”

Mheshimiwa Spika, Sheria tunayoitunga siyo tu kwa ajili ya kuwasaidia waajiriwa, lakini Sheria hii pia ni lazima iwalinde waajiri, maana bila mwajiri kuwepo hakutakuwepo mwajiriwa. Sasa inapokuwa mimi ndiye mwajiri, nimemtuma mfanyakazi wangu abebe mzigo kwenda Urambo Tabora, akageuka na hiyo gari akaeleke Morogoro, halafu akapata ajali akakatika miguu yote, maana mimi sikumtuma Morogoro bali nimemtuma Urambo; sasa inapokuwa amepata ulemavu ambao unapelekea *permanent disabled* basi alipwe?

Mimi naona hapa si *fair*, labda ingesema tu kwamba, auguzwe na mwajiri na mambo kama hayo, lakini siyo kumlipa fidia kwa sababu hiyo. Maana wakati mwingine waajiriwa nao wana uzembe wa moja kwa moja, unaambiwa huwezi kuendesha mashine hii ukiwa umelewa, lakini yeye anakuja kazini amelewa na akalazimisha kufanya hivyo. Sasa lazima Sheria hapa itoe *favour* kwa pande zote za mwajiri na mwajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la mwisho ambalo nataka kulisema ni pale inapotokea kwamba, mfanyakazi ameumia na ameshakuwa *declared* kwamba, yeye ni *permanent disabled*, anaweza akalipwa. Wako wengine ambao kwa *nature* ya maumivu waliyonayo, ndiyo wanatakiwa kupata matibabu katika maisha yao yote, yaani katika maisha yote yeye anatakiwa aendelee kupata yale matibabu; kama ni *consultation* ya KCMC. Nikichukulia *case* ya mzee mmoja aliyekuwa akifanya kazi Idara ya Maji na akavunjika mgongo akiwa yupo Moshi na sasa hivi ni miaka zaidi ya minane yupo, lakini hajiwezi kabisa anatembelea balskeli; anaitwa Mzee Hango anaishi hapa hapa Dodoma maeneo ya Chang’ombe. Aliwahi kuja kuniomba nimsaidie, lakini nimejaribu jitihada zangu zote zimeshindikana kwa sababu ya msimamo na namna Sheria ilivyo.

Mheshimiwa Spika, maumivu aliyonayo yanampelekea yeye kuendelea kupata matibabu mpaka mwisho wa maisha yake. Sasa katika aina hii ya *injury*, hapa hapa Sheria lazima ingesema huyu mtu anaendelea kupata nini, analipwa malipo gani, maana *compensation* ameshakuwa *declared* kwamba yule yeye ni *permanent disabled*, maana yake sasa wanamlipa mara moja *then* basi. Sheria hapa ni vizuri ingeeleza kwamba, huyu mtu mwenye *permanent disabled* lakini anatakiwa kuendelea kupata matibabu, atapataje.

Yule Mzee Hango, anatakiwa kuwa anakwenda KCMC kila baada ya miezi sita, lakini ameendelea kwenda mpaka uwezo umeisha na leo hii hana fedha ya kwenda KCMC. Kwa hiyo, anakaa tu nyumbani anangojea majaliwa ya Mwenyezi Mungu, lakini angekuwa anakwenda kumwona Daktari, pengine angeongeza siku zake za kuishi. Je, katika hali hii sheria inasema nini?

Nimejaribu kuangalia *provision* hapa, karibu nyingi zinajaribu kama mazingira ya kumalizana nao watumishi wanapokuwa wanapata matatizo na baada ya hapo sijaona, labda pengine mimi sikuweza kuiona kuna *oversight*. Kwa jitihada zangu nilizozifanya, sikuweza kuona na pengine ni vizuri nikapewa ufanuzi katika mazingira ya namna hiyo kama yanayomkabili Mzee Hango anayeishi Chang'ombe hapa Dodoma; sheria inamsaidia namna gani?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kama nilivyo sema kwamba, Muswada huu ni mzuri na umekuja wakati muafaka na ni vizuri ukapita haraka ili uweze kuwasaidia wengi ambao wanapata matatizo.

Baada ya kusema haya, naomba kuunga hoja mkono hoja. Ahsante sana.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene. Sasa namwita Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, wakati huo huo Mheshimiwa Suleiman Kumchaya ajiandae.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Hakika baada ya kumpongeza Mheshimiwa Charles Mwera, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge, nataka niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu muhimu katika Bunge hili. Kama mnavyoona, sheria ya mwisho ilitungwa mwaka 1949; nadhani wengi wetu tulikuwa vijana. Sasa mambo muhimu ni kwamba, sheria hii inataka nini? Inataka kuhakikisha kuwa, mtu ye yote atakayeumia kazini atalipwa haki zake, atatibiwa na kama kwa bahati mbaya atakufa, familia yake ipate manufaa au fidia.

Mheshimiwa Spika, utaona watu wengi katika nchi yetu hii, wanaweza kuumia kazini maumivu madogo madogo wala hawajali wanakwenda zao tu. Hata maumivu makubwa saa nyingine haki kuitafuta inakuwa tabu. Hiyo inaonyesha umuhimu wa Muswada huu kuletwa Bungeni sasa. Jambo moja kubwa ni kwamba, maumivu kazini hatuna takwimu zinazotueleza kiuwazi na takwimu sahihi hazipatikani. Wenzetu Zimbabwe walilitazama tatizo hili na wakaona kwamba, hakika shughuli zote za kibinadamu iwe kilimo, *mining, construction, manufacturing* na usafiri, vilikuwa ndio vyanzo vikubwa vya kuleta maumivu kazini.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu na nchi zote zinazoendelea, tatizo la kuwa tunatumia mashine za zamani sana huko, ambazo nchi za Ulaya na Asia zimeshaacha sisi ndio tunatumia, hizi zinatufanya tupate *accident* mara kwa mara. Mara nyingi maumivu haya yanawafikia watu kichwani, katika mwili wenye, katika mikono na miguu au *system* ya mwili wenye unavyofanya kazi. Wenzetu Zimbabwe wamefanya takwimu na uchunguzi na kuona kwamba, kwao wao asilimia 25 ya ya maumivu yalileta *permanent disability* ilipatikana kwa ajili ya *machinery injuries*.

Wenzetu vilevile wakaenda wakatazama asilimia 23 ilipatikana kwa wale wagonjwa wanaoumwa sana au kupoteza maisha na katika magari, yaani *motor vehicles accident*.

Mheshimiwa Spika, kule Sweden wao walitazama *nature* ya maumivu yenyewe wakasema, wameona aina tatu ya maumivu nayo ni kuanguka kutoka juu kwa umbali mrefu, kupondwa na kitu kizito wakati wa kazi au *motor vehicle accident*; hivi vitu vitatu *accident* ya magari kuangukiwa na kitu kizito au kuanguka kutoka juu imekuwa ndio chanzo cha kuumia kazini na hata kupoteza maisha ya asilimia 65 ya majeruhi wote. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri, atakuwa na *section* itakayotengeneza takwimu ya kutuonesha na sisi tuje hapa kwetu watu wetu wanaumiaje na kwa asilimia ngapi?

Vilevile maumivu kazini yapo ya namna mbili hata tatu; kuna wale wanaoumia yaani unakwenda kazini unaumia, wale ndio wanaopata maumivu ya mwili. Lakini kuna maumivu ya polepole (*insidious*), yaani mtu anafanya kazi anajiona ana afya tu, lakini baada ya miaka 20, 30 huyu mtu anaonekana ana magonjwa. Magonjwa makubwa hasa ni ya kansa ya ngozi au mapafu (*Dust Lung Diseases*). Magonjwa ambayo yanapatikana kwa mtu kuvuta hewa yenyе vumbi nyingi sana. Kwa hapa nadhani tuseme tu watu wanaochimba madini iwe mkaa, iwe madini hayo ya dhahabu, wanayo matatizo hayo kwa wingi. Aidha, wanaofanya kazi katika mashine zinazochambua pamba, wanayo matatizo hayo kwa wingi. Naomba Muswada huu uwe na sehemu inayoonyesha kwamba, kutakuwa na taratibu zinazotumika dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutakuwa na *contract* kati ya mtu mwenye kazi, *employer* na *employee* inayosema kazi yako wewe ni hivi na hivi, lakini inaeleza pale pale kila miezi sita utapima uwezo wa mapafu ya wafanyakazi. Kwa hiyo, kila miezi sita wafanyakazi wote wanapimwa mapafu na kila miezi sita wanaendelea wale ambao wamefikia *level* ambazo hawawezi tena kufanya kazi, wanasimamishwa kazi na wanapewa *permanent disability benefits*, sasa utaona hapa kwetu hii inaweza ikawa ngumu, lakini nadhani wakati huu umeshafika sasa tuenze.

Vilevile tunaona kwamba, pale zamani nadhani hata sasa wapo, kulikuwa na taratibu za *Labour Officers* na sheria za viwandani kwamba kuwepo na vitu vinavyomfanya mtu ajilinde wakati anafanya kazi. Kuna *fire extinguishers*, kuna dawa zile za kumwagia mtu kama amepata sumu au kumwagikiwa dawa, kufanya mambo ambayo yanatakiwa katika Muswada huu yawepo kwa sababu hivi leo kuna matatizo makubwa katika suala hili. Utakuta ujanja ujanja wa *employers*, kwanza anaweza kabisa akakwepa hata kujjandikisha katika mfumo huu na kufanya kazi kinyemela. *Employer* mwingine is just negligent, hajali kuweka mazingira bora ya kazi unless sheria hii inaonyesha mazingira bora ya kazi katika sehemu mbalimbali ya kazi ili tuwalinde wafanyakazi wetu. Mwingine na hii ndio imekuwa tabu sana, anaweza akawa rafiki wa Madaktari; wagonjwa wanaumwa sana lakini yule Daktari hatoi ED, mwingine anaweza kabisa akawa Daktari yule anayetoa ED nyingi anamkwepa haendi pale anapelekwa kwa Madaktari wake, sasa hapa lazima tutumie utu na tutumie namna ya kulazimisha waajiri wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingine pakitokea *accident*, inatakiwa zitazamwe *factors*; vitu gani vimeleta *accident* hii. Je, ni *negligence* ya mwajiri hakuweka mazingira ya kazi vizuri na kama hivyo ndivyo, zaidi ya kupewa malipo ya fidia, huyu mwajiri hupewa adhabu kwa kukosa kuweka mazingira bora katika sehemu ya kazi. Kwa upande mwingine, kuna matatizo kwa wafanyakazi nao vilevile; yapo masuala ya kughushi, yaani kabisa mtu hata haumwi analeta mambo yake tu, anawalipa Madaktari kidogo.

Tuwaambie wafanyakazi wetu na Vyama vya Wafanyakazi waelezwe kwamba, huo sio uadilifu na unaleta tabu kabisa katika kuuhudumia Mfuko huu.

Mfanyakazi mwingine hata kama haumwi anajidai anaumwa. Kuna mfanyakazi mwingine anaumwa sana anajidai mzima, anaogopa kufukuzwa kazi. Kwa hiyo, kungekuwa na kawaida ya kupima wafanyakazi wote katika sehemu zote ya kazi. Wabunge nao sijui itakuwaje, inafaa tucheki afya zetu ili wale ambao wataonekana afya zao si nzuri wapate matibabu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna mambo ambayo ni muhimu katika sheria hii na katika mfumo mzima wa kutoa fidia. Kwanza, lazima kuwepo na *training*. Wafanyakazi wafundishwe namna ya kutumia *machinery* hizi, kuwe na ujuzi wa *technology transfer* ambayo mashine hazifanyi kazi tu ila kwanza ujue namna ya ku-handle na ndipo uanze kutumia.

Halafu kuwe na *good management*, yaani *industrial safety management*, ambapo kule kiwandani inafahamika tarehe kadhaa ilitokea *accident* kadhaa, fulani aliumia akafanyiwa hivi na hivi na ikaonekana kwamba *improvement* gani ifanywe katika ile *industry* ili pasitokee tena maafa hayo.

Jambo lingine ni *frequent inspections* ziwepo, hizi ndizo zinazoweza kutuonyesha kwamba, kiwanda fulani kina nafasi kubwa ya kuleta athari kuliko viwanda vingine.

Mwisho, nadhani Serikali bado ilazimishe kwamba, kila sehemu ya kazi kuwepo na *first aid box* na vilevile kuwe na *dispensary* kama tuliyonayo hapa Bungeni na pale inapowezekana tuweze kabisa kuwa na hospitali. Sote tunajua *Tanzania Occupational Health Hospital* ilijengwa kwenye miaka 1970, wakati ule kulikuwa na msimamo mkali sana wa Serikali kuangalia *Welfare* ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Mtulia, nakutakia upate ahuweni kwa sababu ulikuwa unakohoa na sidhani ni kosa la *air condition* ya Bunge.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mohamed Missanga, aliyeomba mwanzo kabisa asubuhi alikuwa Mheshimiwa Mohamed Missanga. Kwa hiyo, baada yake tu ndipo nitamwita Mheshimiwa Kumchaya. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa

Mwinchoum na wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote na mimi nachukua fursa hii, kuupongeza Uongozi wa Wizara hii, kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wote. Nawapongeza kwa kuleta Muswada huu wakati muafaka wa mageuzi wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. (*Makofit*)

Nina machache ya kuchangia. La kwanza, naomba kutoa wito kwa Wizara kuiongezea nguvu OSHA, kwa maana ya *Occupational Safety Aid Healthy Authority* ili iweze kutoa mchango mkubwa kuviezeshwa viwanda kuepuka ajali, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili Mfuko uwe endelevu vya kutosha. Viongozi wetu wa OSHA hivi sasa wapo wanafanya kazi vizuri, lakini ningeomba Wizara itoe msukumo zaidi kuipatia nyenzo iweze kufanya kazi hizo kwa nguvu inayohitajika.

La pili, baada ya OSHA kupita viwandani, maofisini, wao wanatoa taarifa zao ambazo inabidi zifanyiwe kazi. Lakini kwa bahati mbaya, wakati mwingine waajiri wanapuuza taarifa za OSHA. Sasa nilitaka kuelewa kwa sheria hii; je, adhabu gani zinaweza kuchukuliwa dhidi ya wale ambao walipuuza taarifa za OSHA na hatimaye katika taarifa zao walizotoa awali na janga likitokea mionganoni mwa taarifa hizo; je, uzembe huo ukitokea hatua gani zitachukuliwa taasisi kama hizi? Pia ningeomba ulipaji wa fidia uwekewe kikomo cha muda wa malipo, kwa maana ya kwamba, nimeona mwajiri amewekewa muda wa kuweza kushughulikia matatizo ya mwajiriwa na DG pia, lakini kwa bahati mbaya hakuna kikomo kinachomwezesha huyu Mkurugenzi Mkuu kumpa fidia yake mfanyakazi. Je, mchakato ule uchukue muda gani hatimaye mfanyakazi aweze kupata malipo yake kwa mujibu wa stahili ya sheria yetu hii ambayo tutaipitisha baadaye muda wa kuumia hadi malipo?

Hali kadhalika, nilikuwa naomba vilevile Wizara itoe mafunzo ya mara kwa mara hasa kwa wafanyakazi viwandani juu ya usalama kazini, kwa sababu uelewa wao utasaidia Mfuko wetu huu kuwa endelevu. Nakumbuka Kamati yetu tulikwenda kiwanda kimoja, wafanyakazi wanapewa vifaa watumie kwa ajili ya usalama wao wenywewe lakini hawavitumii. Sasa kuna haja kubwa ya kufanya mipango ya kupita hapa na pale ili wafanyakazi waelewe umuhimu wao binafsi juu ya usalama kazini. Kama walivyosema wenzangu, katika sheria nyingi zilizopita ukiacha hii, pia ingekuwa ni busara sheria yetu hii itakapopita nayo itafsiriwe kwa Lugha ya Kiswahili ili wananchi wengi wa Tanzania waweze kuifahamu na kuitumia vizuri.

Nilikuwa na wasiwasi pia, nini wajibu wa mwajiri baada ya mfanyakazi wake kupoteza uwezo wa kufanya kazi? Naomba kuelewa hilo, Mheshimiwa Waziri, utakapopata nafasi kwenye majumuisho utujulishe. Hali kadhalika kwenye maeneo ya maumivu, bahati mbaya sana sijaona maeneo nyeti. Inaweza kutokea kwa bahati mbaya, hatuombei hivyo, sehemu nyeti zikaharibika, sehemu ambazo zinakufanya uitwe

Mwinchoum, uitwe Sitta na zile sehemu zinazokufanya uitwe Jenista, uitwe Anna au Mwanahamisi. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwinchoum, usimtaje Mheshimiwa Spika kwenye mifano ya namna hiyo.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Sawa sawa Mheshimiwa Spika. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba radhi. Sasa sehemu kama hizi hazijatajwa, sijui zitaingia kwenye kanuni au vipi lakini yanaweza yakatokea mambo yakafikia huko? Namwomba Mheshimiwa Waziri, alitazame hili kwa unyeti wake. Naomba pia kuelewa uhusiano wa Mfuko na Kamisheni ya Kazi. Tunawategemea sana *Labour Officers* kwa ajili ya kusaidia Mfuko huu katika kufanya kazi zao za kila siku. Je, mahusiano ya Kamishna wa Kazi na Mfuko huu utakaoanzishwa yatakuwaje?

Vilevile kwenye baadhi ya sumu sijaona sumu ambazo zinaletwa na viumbe wa baharini. Mheshimiwa Mudhihir hapa, mwenzangu anafahamu zaidi mambo ya bahari; kuna mnyama yule anaitwa taa au nyenga, akimpiga mtu hawezi kufanya kazi, ana sumu kali sana. Je, hizi sumu zinazosababishwa na viumbe vyta baharini zinachukuliwaje kwenye sheria hii?

Mheshimiwa Spika, kuna haki ya mwajiri kumlipa mwajiriwa anapopata ajali na ikasababisha chombo au kifaa cha kufanya kazi kuharibika na jambo hilo pengine lingetokea kwa uzembe tu, je, mwajiri pale anahuksika vipi au atafaidika vipi na sheria hii? Mfuko utakuwa na wajibu gani wa fidia?

Mafunzo ya usalama kazini nimeshazungumza ni muhimu sana, naomba Mheshimiwa Waziri, ulitiile mkazo hili la vyombo ambavyo vipo chini ya Wizara yako. Ninaamini unawenza kulisimamia na kulifanya kazi hili, likanufaisha viwanda, maofisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache, lakini naomba sana suala la viumbe vyta bahari kama ulivyojua jimbo langu linahusika sana na bahari, nijue wapiga kura wangu wanaweza kufaidika vipi na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwinchoum. Sasa namwita Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kumchaya simwoni humu, yupo? Aah ndio anaingia, basi ni vizuri ajiandae baada ya Mheshimiwa Missanga, wakati huo Mheshimiwa Halima Mdee awe tayari.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa haki yangu na stahili yangu ya kuchangia Muswada huu ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu kama nilivyokuwa nimeyafikiria. Nampongeza sana Mheshimiwa

Waziri Kapuya, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Kazi, kwa maandalizi mazuri ya Muswada huu, pamoja na wadau wote ambao wametajwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika kwamba, waliwashirikisha wadau kadhaa na kazi iliyofanyika inaonekana kwamba imezingatia maoni mengi ya wadau.

Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wenzake, lakini pia naipongeza Kamati kwa kazi nzuri ya kuwahusisha wadau wengi. Kazi nzuri aliyoifanya Waziri Kapuya, sitaki kumsema vibaya lakini nimpe pole kwa mambo mengine, nadhani hajatetereka na anatuwasilishia Muswada vizuri tu, pole sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijakwenda kwa undani, niseme yafuatayo: Wataalam wa falsafa ya afya wanasema, kinga ni bora kuliko tiba. Mimi ningetaka kusema kwamba, pengine ni vizuri wakati tunafikiria watu watakaoathirika walipwe fidia, lakini nadhani kubwa zaidi Muswada huu au kanuni ziangalie namna ya kuzuia watu wasipate ajali zaidi, mkazo uwe watu wasipate ajali zaidi kuliko kufikiria zaidi kuja kuwapatia kinga, ingawa wakishapata hiyo ajali lazima wapate kinga. Kwa hiyo, nasema ile falsala ya kinga kabla ya tiba na kwa ajili hiyo nisisitize yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, lipo suala la *safety regulations* katika sehemu za kazi, ambazo ndiyo muhimu sana. Uzoefu na ushahidi upo wa mazingira ambao unaonyesha kwamba si waajiri wote wanazingatia hizi *safety regulations* na kwa sababu ya uhaba na uchache wa nyenzo ya wale wanaosimamia kama wenzenetu wa OSHA basi unakuta viwanda vingi havizingatii na matokeo yake ndiyo maana ajali zinakuwa nyingi watu wanaumia wanakatika miguu, wanakatika mikono na wengine wanafariki. Kwa hiyo, nadhani hilo la kwanza liangaliwe.

La pili, ambalo linastahili kuangaliwa ni *medical check up* kwa wafanyakazi, pawe na *routine* hasa wale wa viwandani ambao kwa *nature* ya kazi zao, yapo maradhi ambayo yanapatikana; kwa mfano, wale wa viwandani, katika migodi na kadhalika. Acha wale wa maofisini, lakini hasa wa viwandani na kwenye magereji ni vizuri kuwa na utaratibu unaoeleweka, ambao unaweza ukaangaliwa na hawa watu wa OSHA na wengine kuona kwamba, kuna utaratibu wa kawaida wa kuangalia kwa mfano, Kifua Kikuu (TB) na kadhalika, yale maradhi ambayo yanafahamika yanasaababisha uharibifu wa afya kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu ni ile elimu kwa wafanyakazi wetu, wajue umuhimu wa kujikinga wao wenyewe na umuhimu wa kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu. La nne, ni suala la vifaa vya kinga. Wakati fulani nilikuta watu wa Manispaa moja kule Dar es Salaam, sitaki kuitaja, wanashughulikia maji machafu ambapo kuna kinyesi, lakini hawakuva *gloves*, hawana viatu yale makubwa yale yaani hawana kifaa chochote cha kukinga afya zao.

Sasa nilidhani haya ni mambo muhimu kuyaangalia kwanza na kuwe na utaratibu maalum katika sheria au katika *regulation* ambayo Mheshimiwa Waziri, atayasisitiza ili

kupunguza matatizo haya ya kulipa fidia hapo baadaye. Ili haya yatekelezeke, kama alivyosema Mheshimiwa Mwinchoum pale, Kitengo chetu cha OSHA kwa kweli ni lazima kiimarishe. Kwa mnasaba wa sheria hii ni lazima kiimarishe ili kiweze kufanya kazi sawa sawa

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka huu kama kumbukumbu yangu ipo sawa sawa, wamepata bajeti ya shilingi milioni tano kwa mwezi au shilingi milioni 60 kwa mwaka; hivi shilingi milioni 60 kwa mwaka Dar es Salaam peke yake, watatembelea kiwanda gani watakwenda Manispaa gani, watakwenda Wilaya gani kwa mwaka mzima huu? Sasa unajua wakati mwingine tunaweka vitu hivi kwa masihara hivi, tunaonekana kama tunafanya lakini *we are not serious*. Kama tunataka kuamua kunya kitu tufanye kitu, *seriousness* ioneokane. Kwa hiyo, ili haya niliyoyasema ya utangulizi yafanyike, watu wanaostahili kuhakikisha kwamba haya yanafanyika, ndugu zangu hawa vijana wetu OSHA, naomba waimarishwe, wapewe nyenzo na wapewe bajeti ya kutosha kulingana na majukumu ambayo wanatakiwa wayafanye.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, niende kwenye Muswada wenye. Sheria hii Mheshimiwa Jenista Mhagama alisema ni ya mwaka 1949, lakini mimi kumbukumbu zangu zinasema ni ya mwaka 1948 na ilifanyiwa marekebisho ya kwanza mwaka 1949, mara mbili kabla ya ukoloni. Baada ya kupata uhuru imefanyiwa marekebisho mwaka 1966, 1967, 1969, 1971 na mwisho ni ya mwaka 1983. Kwa hiyo ni sheria ya siku nyingi na kwamba, toka imefanyiwa marekebisho ya mwisho mwaka 1983, sasa hivi takribani miaka 25; ni muda mrefu sana. Hapa nataka nitoe wito kwa Serikali, hebu kuweni na utaratibu maalum unaojulikana *m-review* hizi sheria ili tusiendelee kupiga kelele, sheria imesema imepitwa na wakati, wakati inadhihirika.

Sasa Sheria kama hii ambayo inawagusa watu moja kwa moja, miaka 25 haijakuwa *reviewed* wakati inarekebishwa mwaka 1983, ndipo ilipowekwa kile kifungu au kima cha shilingi cha shilingi 83,000 kwa mtu aliyefariki na shilingi 108,000 kwa mtu ambaye amepata *total incapacitation*. Sasa hebu zitafsiri shilingi 83,000 kwa dola; leo zingestahili kuwa dola ngapi? Wakati huo ni kweli inawezekana ilikuwa pesa ya maana, lakini kwa leo sio pesa. Kwa hiyo, unaweza ukaonekana unawakejeli, unawaonea au unawadhulumu. Tumia neno lolote unaloweza kutumia, ambalo linaonekana Serikali ilikuwa haitendi haki kwa wafanyakazi hawa.

Kwa hiyo, Sheria hii ilirekebishwa mwaka 1983 kwa viwango vyaa sasa; shilingi 83,000 kwa mtu anayefariki na shilingi 108,000 kwa mtu ambaye amepata *total incapacitation*. Ndipo unaenda pale unasema mimi Missanga kwa niaba ya wananchi wote hawa, nimekuja kutoa rambirambi ya shilingi 83,000. Hivi na kitumbo changu chote kweli naweza nikatoa maneno kama hayo? Haiji. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana na maudhui ya kurekebishwa kwamba imepitwa na wakati. Huko nyuma kabla ya mwaka 1983, hiyo miaka niliyoitaja utaratibu ulikuwa ni kutumia mishahara ya miezi kadhaa. Kwa mfano, hii ya mwaka 1966 ambayo alisaini Mzee Rashid Mfaume Kawawa, akiwa *Vice President* hii hapa ninayo, ni Sheria

Namba 60 ya Mwaka 1966, ndiyo iliyorekebisha utaratibu wa kutoka kwenye miezi kadhaa na kwenda kwenye utaratibu huu au ilikuwa unaendelea na utaratibu wa miezi kadhaa na mwaka 1983 ndiyo ikabadilishwa.

Kwa mfano, *section six* ilitoka kwenye malipo ya miezi 36 kwenda miezi 41 kwa mtu aliyefariki na kifungu namba saba kimeondoa miezi 48 na kwenda miezi 52 kwa mtu ambaye amepata *permanent total incapacitation*. Ndiyo utaratibu ulivyokuwa wa miezi kadhaa. Sasa mimi nilifikiri kwamba, tunaboresha kwa kuondoka miezi 54 tunakuja miezi 60 au 70 ya mshahara. Sasa haya tuliyoyakuta hapa, kidogo napata kigugumizi tunakwenda wapi? Makosa yalifanyika mwaka 1983, wakati Sheria iliporekebisha kile kifungu namba sita na saba kwa kuweka vima vya shilingi 83,000 na shilingi 108,000. Sasa tumelia siku zote hapa Sheria irekebishwe, Sheria imekuja; suala la msingi la kujiuliza ni je, imekidhi haja na kuondoa tatizo tulilokuwa tunalilia kwamba shilingi 83,000 ni kidogo?

Sasa katika kifungu namba 46, tunaambiwa hapa kwenye Muswada huu kwamba, muhusika atalipwa asilimia 70 ya mshahara wake. Hapa wametumia neno *earnings*, ingawa pale kwenye ukurasa wa tisa kuna tafsiri maana yake ni nini, hivi *earning* ya mfanyakazi wa chini itakuwa nini?

Mheshimiwa Spika, kima cha chini tunachokijua sasa hivi ni shilingi laki moja; ana makando kando gani huyu yatakayomfanya *earning* yake ya kila mwezi iwe ya kutosha? Zaidi ya ile shilingi laki moja ambayo maskini ya Mungu amesamehewa, hana kodi ndiyo kitu atakachopata. *Overtime* kama atapata hawezi kupata hata shilingi laki moja. Kwa hiyo, maana yake hapa *70 percent* ya huyu ni shilingi 70,000. Huku alikuwa anapata 108, leo unamrudisha shilingi 70,000; sasa *justification* iko wapi? Huyu anapata mara mbili ya shilingi 70,000 ni shilingi 140,000, sasa umeongeza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza la msingi hapa je, Muswada huu umekidhi haja? Mimi maoni yangu ni kwamba, Muswada haujakidhi haja kwa sababu viwango tulivyoletewa hapa ingawa vimefumbwa, lakini kama ni maana ya asilimia 70 mimi nasema hazitosh; ni kama tunawadhihaki wafanyakazi kwamba tunawarekebisha Sheria kumbe *infact* hapa *there is nothing that we are doing*. Tunatwanga maji kwenye kinu.

Huko mbele nimesoma mahali anasema, Mheshimiwa Waziri ndiyo anapewa kazi ya kuweka *minimum* na *maximum*. Sisi kama Wabunge hapa tunapitisha nini? Mheshimiwa Profesa Kapuya, samahani kumtaja jina, atakwenda kuweka nini? Anawenza akaweka shilingi 85,000 au shilingi 90,000, anaweza akaweka shilingi 110,000. Bunge lako hili Tukufu liambiwe tutahakikisha vipi kwamba, hayo Mamlaka aliyopewa kwenye Kanuni ataweka *minimum* na *maximum* ya *amount* gani; si ndiyo tuna mnunua mbuzi kwenye gunia? Yaani hapa tunasema tumepitisha Muswada, naulizwa na mfanyakazi nikiumia mikono yangu yote miwili ikikatika nalipwa nini? Nabaki kumwambia Mheshimiwa Profesa Kapuya atakwambia. Hii tunafanya dhihaka. Mimi nasema ni afadhali turudi kwenye utaratibu ule wa zamani miezi kadhaa, miezi sitini; vinginevyo hapa tunafanya dhihaka.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Waziri ni mwadilifu, lakini kesho tutampata Waziri X ambaye si mwadilifu, hana *commitment*, atafanya mambo ya ajabu ajabu maana yake tusintazame mtu. Kapuya, *Alhaj*, Muumin, Simba mzuri; tusintazame mtu namna hiyo. Tuangalie atakuja mwingine ambaye hafanani na uadilifu wake; je, huyu atatuwekea nini? Kwa hiyo, nasema hapa tunanunua Mbuzi kwenye gunia. Mimi ningependa kupata maelezo mazuri ya kutosheleza, vinginevyo kwa kweli Muswada haujakidhi kilio cha wafanyakazi na sisi Wabunge turekebishe Muswada baada ya kukaa miaka 25, baada ya kufanyiwa marekebisho ama kwa sababu ya *total incapacitation* ama *cases* nyingine ambazo zinatokea. Ingawa kimsingi mimi nashukuru katika Muswada huu yapo mambo mengine mazuri.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kusema pande zote mbili; kwa mfano, suala la Mfuko, ni jambo zuri kwa sababu lina uhakika sasa mfanyakazi atakayeumia hatababaishwa na mwajiri. Kutakuwa na Mfuko ambaao ni endelevu, utaendelea kumlipa. Hilo nasema ni sawa; Muswada pia unaleta utaratibu wa kwamba, malipo haya yatakuwa endelevu, sio unapewa shilingi 83,000 inakuwa basi, hapana. Malipo yatakuwa endelevu kwa wale ambaao watapata *temporary* au wale watakaopata *permanent* na utakuwa unalipa katika utaratibu wa pensheni ambaao umeelezwa vizuri huko mbele. Hilo nalo ni jambo zuri; lakini vilevile jambo lingine zuri ni suala la *lump sum*. Kwenye *total incapacitation* pale mtu ameshapata kile cha kudumu miguu, mikono na nini, familia ile inaweza ikaomba *lump-sum* labda kwa sababu moja ama nyingine. Huo utaratibu naona upo, nasema pia naupongeza unaweza ukasaidia. Tatizo langu mimi ni pale mbele ambapo nimesema kwamba, naona bado sijaridhika labda nipate maelezo ya kutosheleza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, vilevile Sheria inatoa haki ya matatibu. Huko nyuma hii haikuwepo, lakini sasa mfanyakazi anayeumia atakuwa anastahili haki ya matibabu kutoka kwenye Mfuko huu. Nasema hilo nalo ni jambo la kulipongeza, ni jambo zuri ila yapo mambo ya kuzingatia kwa Mheshimiwa Waziri. La kwanza, limeelezwa na Kamati kwamba, huyu *DG* ni mtu muhimu kweli kweli. Mimi nafurahi katika *schedule of amendment* wamesema atapeleka majina matatu ya watu waadilifu kwa Mheshimiwa Rais.

Nataka nikazie hapo, Mheshimiwa Waziri tunamtegemea kufanya kazi nzuri na apatikane huyu *DG* kutokana na hawa watatu ili Mheshimiwa Rais aweze kuamua. Lakini pili urasimu usiwepo katika hili na tatu baya zaidi, tuache *technicalities* kwamba umechelewa, ilikuwa uje jana hukuja. Mtu kakatika miguu unamletea *technicalities*. Angalia yale maudhui yenyewe, huyu amekatika miguu yake yote na huyu amekatika mikono yake yote anastahili kupata hizi, asaidie huyu. Tuache visingizio vingine vyta kijinga jinga ambavyo vinaweza kupoteza haki ya mtu. Tuangalie hasa kama huyu anastahili kupata kwa kuumia. Haya ndiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri ayazingatie.

Mheshimiwa Spika, kifungu namba 82 kinatoa haki ya kukata rufaa, lakini hakielezi anakata rufaa kwenda wapi; anakata rufaa kwenda kwa Mkurugenzi kwanza au

anakata rufaa kwenda kwa Waziri? Naomba hapa lazima kuwe na *paragraph* ambayo inaeleza hii haki ambayo imetolewa katika kifungu cha 80(2), ilelezwe hii rufaa inakwenda kwa nani kwa Waziri au Mahakamani. Ninafurahi kwamba, kifungu cha 74 pale kinaleza kwamba, mwujiru atachangia kulingana na *risk*. Waajiri wengine ni wakorofu; wanaweza wakapiga mahesabu wakasema kumlipa Missanga hapa ni shilingi milioni 30, wakagoma kulipa na wakatafuta njia za ujanja, rushwa kwa marafiki zangu hawa watu wa OSHA, si wote lakini baadhi yao ni dhaifu, ile kesi ikaisha hivi hivi.

Naomba hili nalo litiliwe umakini sana, wanapiga mahesabu sana hawa waajiri. Hivi kweli nitoe milioni 100 au 50 kumlipa huyu? Ataona afadhali atoe rushwa ya shilingi milioni 10 au milioni 20 ili kuondoa utaratibu wa kumlipa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri au Serikali kwa ujumla waliangalie, wapo hawa watu ambao wanaweza wakatuharibia mambo yetu katika hali kama hiyo. (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, nafurahi pia kwamba upo utaratibu kwa mtu atakayeumia wakati akiwa njiani. Maana yake moja ya udhaifu wa Sheria iliyopita ni kwamba, mimi nimeingia kwenye gari la Bunge nakuja hapa Bungeni naumia katikati hapa, Sheria inasema kwamba wewe hukuumia kazini. Sasa nafurahi hilo limewekwa hapa bayana kwamba, mtu anayeumia akiwa anakwenda kazini au anatoka kazini, iwe ndani ya gari ya mwajiri au gari lingine kama nimeelewa sawa sawa, ningependa Mheshimiwa Waziri anihakikishie. Naupongeza Muswada huu. (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofu*)

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo katika Muswada huu. Napenda kuwapongeza wenzetu wa Wizara ya Kazi, kwa kuuleta Muswada huu kwa wakati muafaka, pamoja na mabadiliko yote. Mmefanya kazi kubwa, nia na dhamira ni kutaka kumsaidia mfanyakazi ili aweze kufanya kazi kwa uhakika, akijua kwamba kama ataumia basi anaweza kulipwa ama atalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, mimi nilishawahi kuzungumza huko nyuma kuhusu Sheria za kazi na nilizungumza kutokana na uzoefu ambao niliupata wakati nikiwa Msaidizi wa Rais pale Ikulu. Nilikuwa na utaratibu wa kuwasikiliza wananchi kila Jumatano. Moja kati ya matatizo ambayo nimekuwa nikiyapata ni suala la wafanyakazi kunyimwa haki yao, pamoja na fidia. Wasiwasi wangu ni kwamba, Sheria hii leo hapa tunaitunga lakini kama hali itaendelea kuwa hivyo hivyo, wafanyakazi wataendelea kutokusikilizwa katika vyombo vyote vya nchi hii; itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja wa Kampuni ya kigeni ambayo imekuja nchini kwa utaratibu wetu wa kuwekeza, imewaajiri watu wetu lakini Kampuni hii ilikuja ikageuka ikawa kazi yake ni kuwatesa wafanyakazi. Hawalipwi mshahara unaotakiwa kulipwa wa kima cha chini, hawalipwi saa za nyongeza na hiyo habari ya fidia sahau kabisa, walikuwa hawaijui lakini kazi inafanyika wao wanapata faida. Ninachoomba katika Sheria hii, haya Makampuni ya nje haya yatazamwe sana. Mimi huwa najiuliza;

hivi haya makampuni yanapokuja kuwekeza katika nchi yetu hayaelezwi taratibu za nchi yetu, Sheria za nchi yetu na nia na madhumuni ya kukaribisha ama kufungua milango ni Watanzania kufaidika na makampuni haya yanayokuja kuwekeza. Sasa leo inapokuja kuonekana kwamba, haya makampuni yanaendesha mambo yake kwa utaratibu wao wenyewe, bila kujua kwamba yapo hapa kwa niaba yetu, mimi inanishangaza kweli kweli.

Huwa najiuliza; pale *Tanzania Investment Centre* hakuna kitengo cha Kazi ama hakuna kitengo kinachotoa utaratibu wa Sheria za kazi katika nchi yetu; kwamba Kampuni za nje zinapokuja kuwekeza katika nchi yetu ziambiwe pale pale kwamba bwana wewe unakuja kuwekeza katika nchi yetu, hatuna matatizo hata kidogo lakini uwekeze ukijua kwamba hizi ndizo Sheria zetu. Anaweza awekeze, hawezি aondoke. Haiwezekani hata kidogo, tuwakaribishe wageni waje kutukandamiza katika nchi yetu. Haina maana hata kidogo na hata hiyo maana ya uwekezaji haipo. Kwa hiyo, mimi naomba Wizara ya Kazi suala hili wasilifumbie macho. Lazima walitizame kwa undani wake, hasa makampuni ya kigeni. Sitaki kusema kwamba, hakuna makampuni yetu ya ndani ambayo hayaendeshi shughuli zake kwa kufuata Sheria za nchi yetu hata kidogo, yapo. Mimi ninakuwa nina uchungu mkubwa sana, pale ninapoona wenzetu kutoka nje hawataki kufuata Sheria zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi za wenzetu wao ndio wanashika mpini, mwekezaji anashika makali. Anaambiwa wewe unataka kuwekeza katika nchi yetu, sheria yetu ni hii hapa kama unataka malighafi hii hapa, utakapotengeneza bidhaa zako nenda kaenze kuuza katika nchi yako huko huko. Hiyo itasaidia kuthibitisha kwamba, hicho unachokitengeneza kweli kina thamani. Katika nchi yetu hii, yanatokea mambo ya ajabu ajabu kabisa mpaka unashindwa kupata majibu. Hivi ni nini? Tumepewa vitu gani vya ajabu ambavyo vinashindwa kutupa mawazo kwamba sisi tunafanya haya kwa niaba ya Watanzania? Nataka niungane na kaka yangu Mheshimiwa Missanga, sina kipingamizi hata kidogo cha kumwachia Waziri wa Wizara husika atoe kiwango cha fidia.

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo wanapoweza kutumia waajiri ambao hawana dhamira nzuri kwa wafanyakazi na hawa wa mataifa ya nje na watafika mahali wataanza kuzungumza maneno ya ajabu ajabu kwamba, huwezi kunibabaisha Bwana Serikali yako nimeiweka mkononi. Nimeyasikia maneno haya, ninazungumza kwa ushahidi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kazi, aeleze hapa hapa kwamba, fidia hii kiasi kadhaa, ukikatwa shingo kiasi kadhaa, ukiumia unakwenda kazini kiasi kadhaa. Hii ya kumwachia tu kwamba Waziri atatoa kiwango anavyoona yeye, mimi nina mashaka kabisa. Nina mashaka hata kama Waziri anasema atakuwa na Wanasheria, sijui atakuwa na wataalam wengine watakaomshauri, lakini hawa watu ni wajanja kweli kweli.

Hata kama patakuwa na watu kumi pale, anaweza akacheza nao akawarubuni; aliyekatwa kichwa akapewa shilingi 50,000 mambo yanamalizika na akipanda ngazi akienda juu huko Sheria inamkataa. Anarudi nyumbani mlemauvu maskini, hana uwezo hata kidogo wa kuendesha maisha yake; ni hatari sana. Tusije tukajiandikia historia kwamba, Bunge lile ndilo lililoweka sheria ya kumkandamiza mfanyakazi kiasi hicho. Mimi sipo tayari hata kidogo na wewe Mheshimiwa Spika, unajua tumetamka katika

Ilani yetu ya Chama chetu kwamba, nchi hii ni ya Wafanyakazi na Wakulima. Kwa hiyo, lazima tufanye kila linalowekezana, kulinda maslahi ya mfanyakazi na sote tunajua tunapozungumzia kukua kwa uchumi, tunazungumzia mchango wa mfanyakazi na mkulima. Iweje katika Sheria hii ambayo tunaitunga leo iwe na mapengo ambayo yanaweza yakamfikisha mfanyakazi mahali pabaya? Mimi nasema kama tunawenza tukarekebisha hapa hapa tufanye hivyo. Tusitoe mwanya hata kidogo, tumlinde mfanyakazi ambaye ni mvuja jasho, anayelitumikia taifa letu na sisi sote hapa tutafaidika.

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho, tujitahidi sana kuzuia mianya ya rushwa ambayo baadhi ya makampuni yanaweza kufanya kwetu sisi wenyewe. Sheria hii itufikishe mahali, inawezekana pengine mionganini mwetu humu tuna vijikampuni vyetu humu; ifike mahali kwamba mtu anapoanzisha kampuni lazima ajue kwamba naanzisha kampuni hii nikijua kwamba kama mfanyakazi ataathirika hii ndiyo fidia ambayo natakiwa kuitoa. Naomba katika eneo hili, Wizara ya Kazi, ifanye kazi kweli kweli. Yapo makampuni mengine ni makampuni bubu hayajasajiliwa lakini yanafanya kazi, yanaajiri wafanyakazi, naomba Wizara husika ifanye kila linalowezezana kwa kutumia utaalam wao, kwa kutumia misaada mingine wayafahamu makampuni haya na wawafahamu wafanyakazi wanaofanya kwenye makampuni haya ili litakapokuja kutokea wasije wakageukwa, maana wanaweza kusema sisi hatujui wewe unafanya kazi kwenye kampuni gani, mbona hapa haipo, mbona haikusajiliwa, mbona hivi! Watu wanaumia. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Kazi ijiridhishe, iwe na uhakika kwamba, haya ndiyo Makampuni yanayoajiri wafanyakazi katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisema nichangie eneo hilo tu maana lilikuwa linanikera kweli kweli. Ukienda katika nchi za wenzetu huwezi kucheza na mfanyakazi, mfanyakazi anaheshimika. Leo ilipokuja Sheria hii nikasema hapa hapa. Ni matarajio yangu kwamba, ndugu yangu, mwana-Simba mwenzangu, Mheshimiwa Profesa Kapuya na kaka yangu Mheshimiwa Dr. Mahanga, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, mtakaa chini myazingatie haya tunayoyazungumza ili tukitoka hapa, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunatetea maslahi ya wafanyakazi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Kwa kuwa ndiyo nachangia kwa mara ya kwanza katika kipindi hiki; nachukua fursa hii kumpongeza Mbunge wetu wa Jimbo la Tarime, Mheshimiwa Mwera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kiasi fulani ni mdau kwenye Wizara hii, kwa hiyo, ni muhimu ni-*declare interest*; kama mnavyofahamu, nipo likizo tu ya miaka mitano na nategemea Ubunge wangu ukiisha, nitarudi kwa Mheshimiwa Profesa Kapuya kama atakuwepo pale. Sasa nina machache ambayo ninapenda kuchangia kutohana na Muswada huu:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi, mimi sikubaliani na huu Muswada si kwamba sitaki maslahi ya wafanyakazi ambao wanaumia wakiwa kazini yasitekelezwe ama yasiboreshw, ninapingana na Muswada huu kwa sababu ninaona unaendeleza urasimu

badala ya kutatua tatizo ambalo lipo hivi sasa. Ninazungumza hili kwa sababu nimefanikiwa kupitia Muswada, sijapitia mara tatu tatu, kama Mheshimiwa Mama Malecela anavyofanya, lakini mimi nimepitia Muswada. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Sheria ya zamani, tatizo la msingi la Sheria hiyo lilikuwa kwamba, *compensation* ilikuwa imepitwa na wakati kwa mantiki kwamba, Sheria ilikuwa ya mwaka 1949. Sasa *maximum compensation* ilikuwa inazidi shilingi laki moja. Kwa hiyo, unakuta kwenye mazingira ya sasa hivi, hii *compensation* ni ndogo sana. Kwa hiyo, sasa kilichotakiwa kuboreshwa ni yale maslahi ya mfanyakazi anapokuwa ameumia kazini, badala ya leo hii tunaletewa Muswada kama tuna-establish institution nyingine. Hapa kuna *Director General*, katika Sheria ya zamani na ninaamini ilikuwa na dhamira ya dhati kabisa, ofisi za *Labour Officers* zipo hadi Wilayani na zipo mpaka walipo wananchi.

Sasa hapa tunaambiwa kuna mtu huyu anaitwa *Director General* na tunaambiwa kwamba malalamiko ndiyo anapewa yeye. Huyu yupo hapa juu, hakuna *structure* yoyote ambayo ipo huku chini inayoweza kusaidiana nayo. Ukiangalia huu Muswada, hajatajwa *Labour Officer* hata mmoja. Sizungumzi hivi kwa sababu nina maslahi, ila lazima mwisho wa siku tuwe wahalisia. Sasa tunakuwa tunajiuliza; huyu *Director General* ambaye tunaambiwa kwamba kutakuwa na hicho kitu kinachoitwa *Fund*, ambacho yeye *Director General* atakuwa na wataalam; watakuwa na *capacity* gani basi ya kuweza kujua mwananchi wa kule Rukwa, mwananchi wa kule Urambo, mwananchi wa kule Kigoma na kuweza kujua wananchi wa maeneo mengine ambao wamepata ajali na anahitaji kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna tatizo; kuna Mbunge jana alikuwa anachangia akasema kuna Miswada inaletwa kwa ajili ya miradi ya watu. Sasa Muswada kama huu, unaweza ukawa unaleta picha kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunaona kabisa kwamba, Sheria hii hii inaonyesha kwamba, *employer* ndiye anatakiwa aripoti kwa *Director General*. Ikumbukwe kwamba, hapa kuna *conflict of interest*; mimi ni mfanyakazi nimeumia, kimsingi *employer* ndiye anayetakiwa ani-compensate mimi kwa sababu nimeumia nikiwa kazini. Sheria inasema yeye ndiyo anayetakiwa apeleke taarifa kwa *Director General*. Sasa unapokuwa na mazingira kama hayo na sote tunajua waajiri wetu wakoje, lazima tuwe *realistic*, tusiwe tunapitisha sheria kama sheria za nchi zilizoendelea. Tupo katika nchi ya Tanzania ambako kuna urasimu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, sasa unakuta mazingira kama haya ni mabovu sana. Sauti jamani!

**SPIKA:** Pole sana, pole sana!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, inabidi niwe naletewa maji.

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia kitu kingine; ukija kwenye kipengele cha 46(1) cha sheria hii kinazungumzia kiasi cha *compensation* ambacho mfanyakazi anatakiwa apewe. 46(2) inaenda mbele, inasema kwamba, katika mazingira fulani Fulani, kama itakavyoamuliwa na *Director General*. Sasa mazingira kama haya, yanakuwa yanatengeneza kitu kinachoitwa rushwa, kwa sababu unapokuwa unampa mtu madaraka makubwa sana yatakayokuwa yanamfanya yeye aweze *ku-determine* ni kiasi gani kinachoweza kuwa *equitable* kwako wewe katika mazingira fulani, hii ni rushwa. Tunajaribu kutengeneza mazingira ambayo tunaweza tuka-*attract* rushwa.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala zima la mkanganyiko wa sheria, wenzangu hapa wakati wanachangia wamezungumzia sana kuhusu *OSHA*, wamezungumzia sana kuhusu *Labour Officer*. Ukweli ni kwamba, kitu kinachoitwa *OSHA* hapa hakitambuliki na mtu anayeitwa *Labour Officer* hapa hatambuliki, kimeundwa kitu kingine tofauti.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria hapa kwa ajili ya masuala ya *Occupasional Safety*. Mwaka 2004 ikapitishwa sheria ya *Employment and Labour Relations Act*. Sheria ya *Employment and Labour Relations Act* inaanzisha watu wanaoitwa *Labour Inspectors*. Hawa *Labour Inspectors* ambao wanaenda kwenye viwanda kuangalia kama...

*Hapa (Mheshimiwa Halima J. Mdee) Aliletewa Maji*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nashukuru sana! Wanaenda kwenye viwanda kuangalia kama waajiri wanatekeleza ile sheria ambayo inawataka waweke wafanyakazi katika mazingira yenye afya ili wasiweze kupata magonjwa. Sheria ya *Occupational Safety and Health Act (OSHA)*, inazungumzia mazingira ambayo, kwanza imekuwa *introduced Authority* na hiyo *Authority* ina mamlaka ya kuhakikisha kwamba, masuala kadhaa yanayohusiana na afya ya mfanyakazi yanatekelezeka.

Sasa ukija kuangalia na sheria hii hapa, kuna vitu ambavyo unakuta kuna mkanganyiko wa kisheria. Kuna hizi *Institutions* mbili zimeanzishwa, ambazo kwa kiasi kikubwa sana zinashughulikia kuangalia maslahi ya kiafya ya mfanyakazi, lakini huku zimepuuzwa. Sasa utakuta sheria zipo, lakini kunakuwa kuna mgongano mkubwa sana wa sheria. Kwa hiyo, mimi nadhani Mheshimiwa Waziri, akaliangalie hili ili tuweze kupata sheria iliyo bora na tuweze kuwasaidia hawa wafanyakazi wetu, kuliko kuwa na urasimu ambao sasa hivi ni mkubwa kuliko ambavyo ilikuwa kwa *Labour Officers*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu, hiki kinachoanzishwa sasa hivi hakitofautiani na Mifuko ya Pensheni; hizi NSSF, PPF na PSPF. Mimi naona ni bora ili kufanya mambo yaende vizuri, tuwe *practical*. Bora tuhakikishe kwamba, *position* ya *Labour Officer* kama ilivyokuwa zamani, ukizingatia kwamba wao wapo mpaka Wilayani, siyo huyu *Director General* ambaye yupo huku juu, anafanya kazi yake kama ilivyo na haya malipo kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, yanatakiwa

yapitishwe kwenye hizi *Social Security Institutions*, kuliko kuanzisha kitu kingine ambacho katika hali ya kawaida, kitakuwa hakitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, kama haiwezekani, basi hiki kitengo chetu cha *OSHA* kiboreshw. Nasema hivi kwa sababu *OSHA* imeanzishwa mwaka 2003, lakini mpaka leo hii, unaenda kwenye makampuni mbalimbali, unakuta hakuna watu ambao wanakwenda kufanya *inspection*.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa pale Wizara ya kazi kwa mwaka mmoja, tulikuwa tumepewa kitambulisho kikubwa hivi chekundu, kinatisha kweli kweli kwa ajili ya kwenda kufanya *inspection*. *I can tell you*, mwaka mmoja nimefanya pale, hatujaweza kwenda kufanya *inspection*, hakuna vitendea kazi! Mfanyakazi unapanda dala dala, halafu unaenda kwenye kiwanda cha Mhindi pale, unamgongea geti, unamwambia nataka *ni-inspect*; kwanza, anakudharau, yaani hata hakusikilizi. Kwa hiyo, mimi nadhani lazima tuziwezeshe hizi *institutions* ambazo zipo hapa, tukishaziwezesha ndio tuseme kwamba haziwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwa kuzingatia kwamba, hizi *institutions* zimeshindwa kutekeleza kazi zake, naambiwa kule Mererani, vijana wetu wa Kitanzania ambao wameajiliwa na makampuni ya Wazungu, kila siku ya Mungu wanapitishwa kwenye mashine za *X-Ray*. Namaanisha hapo siku saba kwa wiki, siku 364 kwa mwaka. Sasa inabidi tujiulize, hawa watu *future* yao ikoje? Mwekezaji anakuja pale, wameingizwa kwenye *X-Ray* mwaka mzima, wanaacha vijana wetu wanateketetea. Kwa hiyo, unakuta ni mazingira kama haya, *OSHA institution* ambayo imeundwa haina vitendea kazi, *Labour Inspectors* hawana vitendea kazi, wamekaa tu pale ofisini, matokeo yake sasa ndio hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia nilifanya ziara Kigoma kwenye Kiwanda cha Chumvi cha Uvinza. Unakuta watu wanavuna chumvi na ubao, matokeo yake unakuta mtu akivuna chumvi kwa muda mrefu mikono inachubuka na inakuwa kama ina *fungus*. Kwa hiyo, ninashauri, kuliko kutunga hivi vitu, kila siku tunaletewa sheria hapa, tunachanganyikiwa, leo ukimwambia mtu a-trace sheria za kazi, ni nyingi mpaka zinajaa. Ni muhimu tuwe na sheria chache ambazo kama Wabunge wanavyosema, zikiwa *interpreted* kwa Kiswahili, basi kutakuwa na *booklet* ndogo inayoleweka, itakayomsaidia huyu mfanyakazi huku chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi mchango wangu ndio huu. Naomba Mheshimiwa Waziri auzingatie na baada ya miaka mitano nitarudi pale, usije kunifungia mlango. Nitarudi ili tushirikiane pamoja kuweza kusaidia wafanyakazi wetu. Nashukuru sana. (*Makofifi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Kwa kweli ipo kila sababu ya kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kuwawekea sheria nzuri zinazotekelzeza ambazo zinaweza zikawasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini ninapoutazama Muswada huu, mwanzo kabisa unanipa mashaka makubwa sana kwamba, umetoa madaraka makubwa yanayochupa mipaka kwa *Director General*. Unapousoma Muswada huu, mambo mengi ameachiwa *Director General* kuyafanya maamuzi ikiwa ni pamoja na viwango vya fidia.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuthibitisha mamlaka haya ambayo amepewa *Director General*, ukiangalia kifungu cha 62(3) cha Muswada, kinampa mamlaka huyu *Director General* kuchukua nafasi ya Daktari. Hii ni hatari sana kwamba, mamlaka anayopewa na sheria kwamba, *Director General* anaweza akaamua hata bila kupata ushauri wa Daktari. Kwa hiyo, ni vizuri kwanza tukaangalia haya mamlaka na madaraka aliyopewa *Director General* tunayawekea kikomo. Bado nina mashaka pia kwamba, tayari tunazo sheria nyingi ambazo zinawahusu wafanyakazi na mara ya mwisho nakumbuka tulipitisha sheria juu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia hifadhi, mimi kwa mtazamo wangu ina tafsiri pana ambayo inabeba pia masuala ya fidia na matibabu ambayo tunadhani sasa ipo haja ya kutengeneza sheria nyingine. Nilikuwa nadhani kwa mujibu wa sheria hii inayopendekezwa, tunaendelea kutengeneza nafasi ya kuongeza gharama ambazo tunapaswa sasa hivi tuzipunguze kutokana na hali ya uchumi ilivyo katika Dunia na hali ya majukumu inayoikabili Serikali yetu, badala yake tunaongeza kufungua Mifuko ambapo Mifuko iliyokuwepo ingeweza kukasimiwa madaraka haya ya kusimamia na ingeweza kufanya kazi vizuri tu.

Ninaamini kwamba, ingetengenezwa Idara ndani ya Hifadhi ya NSSF ili iweze kushughulikia hili suala ambalo sasa linataka litengenezewe Wakurugenzi, Bodi ya *Directors*, ambao wote hawa watahitaji mishahara, vifaa, posho na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri ipo haja ya makusudi, kwanza, kuiangalia sheria ambayo inataka kufutwa ya *Workmen Compensation* ambayo ni ya muda mrefu. Kama ilivyokuwa imeelezwa katika utangulizi wa sheria hii kwamba ni sheria ya mwaka 1949, lakini namshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Missanga amesema kwamba, mara ya mwisho ilifanyiwa marekebisheso mwaka 1983.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ni nzuri, isipokuwa tu ni kwamba, tumekuwa na tabia katika nchi yetu ya kutokuzipitia sheria na kuzifanyia marekebisheso kila inapobidi. Inaonekana sheria mbaya kwa sababu tu ya viwango ambavyo sasa hivi havikubaliki. Lakini imepita muda mrefu bila kufanyiwa mapitio na kuangalia hali ya mabadiliko ya mishahara, vipato na maisha katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ni sheria hiyo hiyo tu ambayo tungeweza kuitazama mahali ambapo panataka kufanyiwa marekebisheso ikafanyiwa marekebisheso, kuliko kuanzisha kitu kingine kipywa kwa sababu sheria hiyo inatoa kabisa mchakato ni namna gani mtu anaweza kulipwa fidia. Fidia zimeainishwa ndani ya sheria hiyo, pamoja na kwamba viwango vinaweza vikabadiishwa kama yalivyo mapendekezo hivi sasa au yakaboreshwazaidi. Unapotengeneza sheria kama hii, Idara ya Kazi ukaiondoa kabisa, nashindwa kuelewa kwa sababu gani Serikali inaendelea kujitoa katika shughuli za usimamizi!

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kwamba, Serikali inapojiondoa kabisa katika kusimamia, inatengeneza chombo huru, inamwachia mwajiri tu anayeshughulika na kile chombo bila Afisa wa Serikali kama mtu wa kati kati kulismamia suala hili. Inanitia mashaka sana, kwa sababu katika Muswada huu, nafasi ya *Labour Officer* sikuiona. Nilikuwa nadhani bado upo umuhimu wa makusudi kabisa wa kuweza kuangalia kwamba, nafasi ya Afisa wa Kazi inapewa nafasi kama tutakubali kuipitisha sheria hii; vingenevyo, sikuona hata umuhimu wa hii sheria kwa sababu naona haikidhi, pamoja na kwamba ipo haja ya kuangalia viwango vya fidia kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hii unapokwenda kwenye tafsiri ya maneno, unakuta neno *employer* ni “any person who employs an employee.” Kwa hiyo, *employer* ni yule mtu ambaye anaajiri mtu. Sasa ukija kuangalia vifungu; kifungu cha 71 na 72 vya mapendekezo ya Muswada huu, vinambana mwajiri ambaye kwa mujibu Muswada huu, ni mtu yejote; hata mwenye mgahawa tu akimwajiri mtu kuchoma *chips*, basi anapaswa kwa mujibu wa sheria hii kuwa amepeleka taarifa ya watu aliowaajiri kwa *Director General* na asipofanya hivyo, faini yake ni shilingi milioni 50.

Sasa tutazame sheria hii na faini hizo zinazopendekezwa za shilingi milioni 50, kwa mtu ambaye atashindwa ndani ya siku saba kupeleka orodha ya majina ya wafanyakazi wake inamlenga nani? Ni kwamba, huyu *employer* mwingine mdogo mdogo hayumo, haguswi na sheria hii? Tafsiri ya maneno ndani ya Muswada huu ni kwamba, mtu yejote aliyeajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri hata hizi faini, ni vizuri tukaziweka ili kuhakikisha sheria inatekelezwa. Suala la kucheleva tu kupeleka taarifa ya watumishi, unawajibika kulipa faini ya shilingi milioni 50. Kifungu cha 72, kama hukuziweka tu hizo kumbukumbu, *Inspector* akija akakuta huna kumbukumbu, faini yako ni shilingi mioni 20. Tutazame hapa, faini za viwango hivi zinaashiria nini? Ni dhahiri kwamba, zinatengeneza nafasi ya Maafisa Wakaguzi waweze kupewa rushwa.

Mwajiri kama kwa bahati mbaya, hakuweza kutekeleza matakwa ya sheria, badala ya kulipa faini ya shilingi milioni 50, atakuwa tayari kumkatia huyo Mkaguzi shilingi milioni tano, ambayo ni asilimia sijui moja au kumi ya faini ambayo Serikali ingeweza kupata. Lazima pia tungalie viwango vya faini tunavyoviweka ndani ya sheria, viwe vyenye uwiano na uhalisia wa hali ilivyo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninataka kuzungumzia kuhusu fidia na matibabu. Wapo wale ambao wanastahili kupewa fidia moja kwa moja, kutokana na maumivu waliiyoyapata pengine yamewafanya wasiweze tena kufanya kazi. Yupo mtu mwingine ambaye anahitaji matibabu ya muda mrefu, kabla hajafikia kutangazwa kwamba sasa anastahili kupata fidia. Haya matibabu ya kipindi ambacho huyu mtu anaugua ni nani anawajibika kulipa? Mwajiri hawajibiki kumlipia matibabu mfanyakazi wake ambaye ameumia wakati akiwa kazini, lakin bado hajafikia mahali pa kuhitaji fidia. Kipindi hiki cha mpito ni nani anamlipa huyu mfanyakazi? Sheria haijasema bayana na ninataka

nipate ufanuzi kama wajibu wa kumlipia gharama za matibabu mfanyakazi kwa mwajiri sasa zinaondolewa, zinapelekwa kwenye Mfuko.

Bado Mfuko huu kwa mfumo wa utaratibu na Muswada uliofikishwa mbele yetu ni kwamba, hauna mtiririko wa kuweza kumfikia mfanyakazi aliyeo huku chini, hasa maeneo ya vijiji katika ngazi za Wilaya na kushuka chini. Anayeratibu shughuli zote za Mfuko huu ni *Director General* na tunaamini kabisa kwamba, huyu *Director General*, hawezi kukaa Dodoma, atakuwa Dar es Salaam. Kwa maana hiyo ni kwamba, maamuzi yote yanahitaji *attention* ya *Director General*. Muswada haujasema huyu *Director General* atafanyaje kazi zake ili aweze kupata taarifa kutoka huku chini ziweze kumfikia. Kwa hiyo, ningependa pia nionyeshwe kama ipo, pengine sikuiona vizuri. Kama upo huo mtiririko wa namna ya kuweza kufanya kazi na kumrahisishia huyu mfanyakazi aweze kupata fidia yake kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adiha, eneo lingine ambalo ninataka litazamwe ni muda wa kushughulikia hizi fidia inapotokea kwamba, mfanyakazi anataka alipwe fidia. Sheria inatoa mwanya wa kukata rufaa na inampa fursa *Director General*, kuweza ku-review maamuzi yake, lakini bado haijamfunga muda gani anatakiwa awe amefanya hiyo review. Hali kadhalika hata Waziri hajafungwa na sheria kwamba, anatakiwa atoe majibu ya rufaa ndani ya muda wa siku ngapi toka alipopokea malalamiko ya rufaa. Kwa hiyo, inaweza ikakaa katika Ofisi ya Waziri, kwenye Ofisi ya *Director General* hata miezi sita au mwaka.

Kama tunavyofahamu kwamba, matatizo haya ya urasimu katika nchi yetu, yanawanyima sana wafanyakazi haki zao. Kuna shauri ambalo nalifahamu, leo lina zaidi ya miaka kumi, pamoja na maamuzi ya Waziri, lakini Mkurugenzi anashindwa kutekeleza maagizo ya Waziri.

Sasa huo ndio uhalisia katika nchi yetu kwamba, maamuzi yanapuuzwa, lakini mwathirika ni mfanyakazi. Kwa hiyo ni vizuri tukawafunga, tukawawekea kipindi maalum cha kuweza kutoa mamuzi kuliko kuiacha tu sheria inampa nafasi isiyokuwa na kikomo mpaka atakapofurahi, ndipo anapotoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani eneo hili tukilisimamia vizuri, litatoa haki katika muda muafaka, kwa mwathirika yeoyote kutokana na ajali zinazotokea tukiwa kazini. Kwa hiyo, maeneo haya yikitazamwa, nadhani tutakuwa tumeangalia na tumejali maslahi ya mfanyakazi.

Mheshimiwa Spika, bado narudia kusema tena kwamba, sheria hii ambayo inapendekezwa na imeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, haijakidhi matakwa. Sheria hii ina upungufu mwingi, imetoa mamlaka makubwa sana yasiyokuwa na kikomo hata katika maeneo ya fidia, mtu mmoja tu anaweza kufanya maamuzi, huyu akamlipa milioni 50, huyu akamlipa milioni tano, huyu akamlipa milioni moja, kwa kadiri alivyoamka na anavyoona yeeye inafaa. Kwa hiyo, hii hatuwezi kusema kwamba ni sheria nzuri, maadam

imeshindwa kutamka bayana viwango sahihi na vinavyostahili kutolewa kwa mtu ambaye ameumia akiwa kazini, pia viwango kwa ajili ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani bado sheria hii haijafikia mahali pa kuweza kumnufaisha mfanyakazi wa Tanzania. Nakushukuru sana. (*Makofî*)

*(Hapa kulitokea hitilafu ya umeme)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii si hali ya kawaida, mwanga wa namna hii hatustahili kuendelea na shughuli. Sasa ili kuwapa muda wataalam wa Idara ya Ufundî ya Ofisi ya Bunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho asubuhi saa tatu asubuhi. Tutaanza na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na wale wengine wote ambao wana mawazo mazuri, Muswada huu naona umevutia sana, bado kuna nafasi ya wawili/watatu, kwa hiyo tunaweza kuendelea hapo kesho.

*(Saa 01.32 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 04 Novemba, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*